ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/ Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28..Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45..Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55. Mhe.Mohammed Said Mohd	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58.Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe.Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheit Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 24 Oktoba, 2011

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika, Pandu Ameir Kificho (alisoma dua)

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora ndani yake. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora ndani yake. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 36

Jengo la Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Pemba

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:-

Tume ya Uchaguzi Pemba inafanya kazi katika Jengo la Wizara ya Biashara ambalo linatarajiwa kuvunjwa wakati wowote kuanzia sasa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Pemba.

(c) Je, Serikali haioni sehemu ilipo ofisi hiyo sio salama kwa kazi za Tume.

Mhe. Waziri wa Ardi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali kwa kujua kuwa ofisi ndogo ya Tume ya Uchaguzi Pemba inaendesha shughuli zake katika makaazi ya muda, tayari imeshapata kiwanja katika eneo la Mfikiwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi mpya za ofisi ndogo ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(c) Mhe. Spika, Serikali imechukua juhudi hizo baada ya kuona kuwa ofisi ndogo ya Tume Pemba inafanyakazi katika sehemu ambayo haipo salama kwa shughuli za Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

a) Je, Mhe. Waziri ni kasoro gani hasa ndio kikwazo cha matatizo yanayojitokeza wakati wa uchaguzi.

b) Pia ni hatua gani zinazochuliwa kuondosha kasoro hizo.

Mhe. Waziri wa Ardi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu kasoro gani zinazojitokeza wakati wa uchaguzi mimi naliona suala hili halina mnasaba na suala mama, pamoja na hayo napenda kulijibu swali lake Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kasoro zinazojitokeza katika uchaguzi uliopita ni nyingi zikiwemo za watu walioacha kadi zao za uraia katika ofisi ya uchaguzi ambazo mpaka leo hawajenda kuzichukua, na hiyo ikasababisha wapiga kura wakawa kidogo mwaka 2010 kuliko walivyokuwa mwaka 2005. Hiyo ni kasoro kubwa ya msingi.

Mhe. Spika, kuhusu hatua gani zinachukuliwa kurekebisha kasoro hiyo ni kuhakikisha kwamba kila mwenye haki ya kujiandikisha kwa kufikia umri na makaazi kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi ataandikishwa. Kasoro hiyo ni muhimu na inachukuliwa hatua ya kuondolewa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza Mhe. Spika, katika jibu lake Mhe. Waziri amesema kwamba anaelewa kuwa wanafanyakazi katika nyumba ambayo sio yao na ndio wizara tayari imeshatafuta kiwanja katika sehemu ya Mfikiwa naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja lenye (a), (b) na(c) .

a) Mhe. Spika, kwa sababu tume hii ilikuwa inafanya kazi katika majengo haya kwa muda mrefu sana, na kiwanja ndio kwanza kimetafutwa hivi sasa na wanasema kwa sababu walikuwa wanajua kuwa wanafanya kazi katika jengo ambalo sio lao. Je, hiki kiwanja kilipatikana lini na ni hatua gani zinachukuliwa ili kuhakikisha ujenzi huo unajengwa.

b) Kwa sababu ya umuhimu wa kazi zake hili jengo kubakia Mfikiwa sio usumbufu.

c) Mhe. Spika, la mwisho ni kuwa Mhe. Waziri alisema tatizo kubwa ni kwamba kuna watu mpaka leo hawajachukuas vitambulisho vyao vya uraia, katika Zanzibar hii kweli kuna vitambulisho vya uraia.

Mhe. Waziri wa Ardi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu kiwanja kimepatikana lini, nimesema kwamba kiwanja kimeshapatikana na kipo tayari kuanza ujenzi na kimepatikana kiasi ya miezi mitatu iliyopita.

Mhe. Spika, suala lake la (b) linazungumzia kwamba tuliona kuna tatizo la tume hii kukaa katika ofisi ya kuazima ni hatua gani imechukuliwa. Mhe. Spika, suala (a) linajibu kwamba kiwanja kimepatikana sasa hiyo ndio hatua iliyochukuliwa ya kuliondosha tatizo hilo.

Mhe. Spika, vile vile kuhusu ujenzi utaanza lini ni kwamba ujenzi utaanza mara tu fedha zitakapotiwa katika kasma ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Na suala jengine linazungumzia hivi Zanzibar kuna vipande au kuna kadi za uraia. Mhe. Spika, hiyo ilikuwa ni kuteleza kwa ulimi lakini ni kadi za Mzanzibari Mkaazi ambazo ndizo zinazoutmika katika kupiga kura.

TAARIFA.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, ni kwamba suala moja sikujibiwa nilisema kuwa umuhimu wa kazi za taasisi hii na huko jengo litakapowekwa huko Mfikiwa haionekani kuwa itakuwa ni usumbufu mkubwa kwani hapana sehemu nyengine karibu zaidi.

Mhe. Waziri wa Ardi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kwamba Mfikiwa sio pahala mbali sana na Mjini Chake Chake eneo hili liko katika Wilaya ya Chake Chake katika Jimbo la Wawi, liko karibu sana Air Port kwa upande

Kusini na liko karibu sana barabara kubwa inayoendea Chake Chake na Mkoani kwa upande wa Kaskazini. Ni eneo ambalo gari zinaweza kufika wakati wowote Kiangazi na Masika na hatukuona haja ya kutafuta eneo jengine wakati lile eneo limeonekana lipo na zuri na linatosha kwa ujenzi wa ofisi.

Nam. 76

Kituo cha Afya Uwanja wa Ndege

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Abeid Karume International Airport ni sehemu muhimu kwa kukuza uchumi wa Zanzibar, kwa kupokea watalii, mizigo na wasafiri wengine. Hata hivyo, huduma za afya kiwanjani hapo hazipo katika kiwango cha kwaida kwa vile sehemu ya huduma hizo ni eneo dogo sana.

(a) Mhe. Waziri, kutokana na maendeleo ya ujenzi wa jengo jipya la abiria wizara yako kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ina mpango gani wa kuwapatia eneo kubwa kituo cha Afya hapo air port.

(c) Ni taasisi gani ambayo inawajibika katika upatikanaji wa huduma za afya na za kibenki katika uwanja wetu wa ndege.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ni kituo muhimu kwa kukuza uchumi wa Zanzibar kwa kupokea ndege, watalii, mizigo na wasafiri wengine, na ni kweli huduma za afya Kiwanjani hapo hazipo katika kiwango cha kuridhisha kwa mujibu wa hadhi ya uwanja wetu. Kwa kawaida katika Kiwanja cha Ndege kinapojengwa wajenzi wanatakiwa kufuata viwango vya *ICAO* vinavyowiana katika viwanja vya ndege mbali mbali duniani. Hivyo, hata nchi yetu italazimika kufuata viwango hivyo. Kwa bahati mbaya ujenzi wa jengo letu haukuzingatia suala hilo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

(a) Kutokana na maendeleo ya ujenzi wa jengo jipya la abiria, wizara ina mpango wa kutenga na kuwapatia eneo linalokidhi kwa ajili ya kituo cha afya hapo jengo hilo litakapomalizika mwaka 2013. Ni imani yetu sehemu hiyo itatengwa na itakidhi mahitaji hayo.

(c) Taasisi inayowajibika kutoa huduma za afya ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kwa huduma za kibenki ni benki husika itakayoweza kufanya biashara hiyo katika Uwanja wa Ndege kwa kufuata taratibu zitakazopangwa na Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mamlaka tunapenda kutoa wito wa kuwataka watoa huduma hizo za kibenki kujitokeza kwa wingi kwa kutambua kwamba vigezo na masharti yatazingatia viwango na miongozo ya kimataifa kuhusiana na shughuli za utawala na uendeshaji wa huduma za viwanja vya ndege.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa fursa hii asubuhi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, namwambia Mhe. Naibu Waziri atakubalana na mimi kwamba usipojenga ufa utajenga ukuta kwani kichochoro cha afya kilichokuwepo air port hivi sasa kwa muda mrefu kimetoboka na kinawapa usumbufu watendaji wa afya. Je, mheshimiwa una mpango gani kwenda kuziba kwenye kichochoro hicho. Na vile vile kitanda cha wagonjwa hao huwa kimetandikwa maboksi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Wizara ya Afya katika jengo la uwanja wa ndege wanacho chumba ambacho kiko salama wanakitumia kwa ajili ya huduma za kiofisi, na pia ipo sehemu ambayo imekatwa kwa kutumia vyoo wanaitumia kwa ajili ya kutoa huduma. Mhe. Spika, ni kwamba sikubaliani na taarifa anazotoa Mhe. Mwakilishi kwamba wanatumia uchochoro na uchochoro huo ni mbovu.

Nam. 47

Huduma za Afya Katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Afya ina nia njema na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, na kwa kuwa Hospitali hiyo inao upungufu mkubwa wa wafanyakazi kuanzia *nurse, orderly* hadi Walinzi, na kwa kuwa Hospitali hiyo pia ina upungufu wa dawa na sindano muhimu kama "*Modicate*"; na kwa kuwa hospitali hiyo ina ufinyu mkubwa wa bajeti ya chakula.

(a) Ni lini Wizara ya Afya itaweza kuipatia hospitali hiyo wafanyakazi wa kutosha ili huduma zinazotolewa hospitalini hapo ziweze kutolewa kwa ubora na ufanisi zaidi.

(b) Kwa kuwa sindano muhimu sana za "*Modicate*" hazipatikani kwa karibu nusu mwaka sasa. Je, Wizara inawaambia nini wananchi walio wengi ambao wanaitegemea hospitali hiyo katika kutibu wagonjwa wa afya za akili.

(c) ©Kwa kuwa chakula ndicho kinachojenga afyana kwa kuwa afya bora ni miongoni mwa tiba, ni lini Bajeti ya chakula katika hospitali hiyo itaongezwa ili wagonjwa waweze kupatiwa chakula cha kutosha.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Hospitali ya Wagonjwa wa Akili – Kidongo Chekundu ina upungufu wa wafanyakazi kama zilivyo hospitali nyengine. Wizara itahakikisha kwamba kila inapopata wafanyakazi itaongeza hasa sehemu zenye upungufu mkubwa kama Hospitali ya Kidongo Chekundu.

Kwa kuthibitisha hilo wizara imewapeleka katika hospitali hiyo ya Mental wafanyakazi watatu wenye taaluma ya kuwahudumia wagonjwa wa akili, waliorudi masomoni hivi karibuni wenye kiwango cha *Advance Diploma*. Aidha, wanafunzi wa Uuguzi wanaosoma fani ya Afya ya Akili wanaingia kazini kwa utaratibu wa zamu chini ya uangalizi wa wafanyakazi wazoefu ili kuongezea nguvu na utendaji. Aidha, kwa upande wa walinzi wizara imeajiri walinzi wapya wawili kwa mkataba.

(c) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba sindano aina ya "*Modicate*" imekosekana kwa muda mrefu na hii inatokana na ukweli kwamba dawa hiyo haipo nchini katika ghala kuu la dawa Dar-es-Salaam (MSD) ambako ndiko tunakoagiza dawa zote. Wizara ilifanya jitihada za kumtafuta wakala wa kuagiza dawa kwa bahati mbaya nae pia ameshindwa kuzipata. Hata hivyo, kuna dawa inayofanya kazi kama hii ya "*Modicate*" ya aina ya vidonge ndizo zinazotumika. Mhe. Spika, ni kwamba tatizo lilopo ni kwamba hii

vidonge haipendwi kwa sababu inabidi ule kila siku ile nyengine ni ya sindano unapigwa kila mwezi.

(c) Mhe. Spika, maelezo ya Mhe. Mwakilishi ni sahihi na sadakta kwamba chakula ndicho kinachojenga afya na kuwa afya bora ni miongoni mwa tiba. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Bajeti ya chakula katika Hospitali ya Kidongo Chekundu imeongezwa kuanzia mwezi wa Septemba mwaka huu kwa asilimia 67 kutoka milioni moja mpaka milioni moja na laki nane.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana naomba kuuliza maswali matatu ya nyongeza.

a) Mhe. Spika, kwa uchunguzi nilioufanya mimi kuhusu sindano ya *modicate* ni kwamba sindano hiyo inapatikana, mimi nashangaa huyo wakala wenu sijui ni sababu zipi ata akasema sindano hii isiweze kupatikana.

b) Bajeti hii wameiongeza kiasi gani kutoka milioni moja na laki mbili kwa mwezi nataka kujua ni shilingi ngap zimeongezwa kutokana na wagonjwa wale kuwa wanapata mlo mmoja tu kwa siku.

c) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa Hospitali ya Ugonjwa wa Akili wana kilio cha muda mrefu sana cha usafiri na kinawasumbua katika utendaji wao wa kazi hawana gari hata moja. Mhe. Waziri kwa jitihada zako unazozifanya ni lini wategemee kupata usafiri huo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wakati tukiitafuta dawa hiyo ilikuwa haipo na kama Mhe. Mwakilishi amegundua ipo basi tunaomba aje wizarani tushirikiane jinsi ya kuipata.

Mhe. Spika, pia nimemueleza Mhe. Mwakilishi kwamba bajeti yao imeongezwa kuanzia mwezi wa Septemba imeongezwa kwa asilimia 67 kutoka milioni moja mpaka milioni laki nane. Kwa hivyo, hili nimeshalijibu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la usafiri ni kwamba tunalishughulikia kama vile tunavyoshughulikia masuala mengine, naogopa kuwaahidi ni lini kwa sababu ni suala la kutafuta.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri amesema

kwamba bajeti ya kitengo hiki imeongezwa kwa asilimia kubwa na kwamba anaashiria kuwa hakuna tatizo la chakula pale Kidongo Chekundu. Mhe. Spika, ni kwamba mimi na Mhe. Jaku hivi karibuni tumekwenda pale tumewaona wahusika wa pale wanakopa binafsi madukani kwa watu, kwa sababu ya ukosefu wa fedha za serikali.

Mhe. Spika, pamoja na Baraza kupitisha fungu la Kidongo Chekundu pia serikali huwa haitoi fedha ile.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wawakilishi wanisaidie sitaki kuwalaumu wafanyakazi wa sehemu hiyo, lakini kama ni kula chakula cha kawaida ni miliono moja na laki nane wanakula, lakini kama ni kula mayai, matunda na maziwa hilo halijawezekana na sina habari kwamba watu wanakopa madukani, naomba taarifa hiyo anifikishie ili niweze kulichunguza ipasavyo.

Nam. 87

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Dunia daima haitosahau mchango wa Mzee Nelson Mandela wa Afrika ya Kusini katika nyanja tofauti zikiwemo zile za uhuru, usawa, uchumi na kadhalika. Miongoni mwa mambo muhimu yanayothibitisha uwezo, ari na mchango mkubwa wa muafrika huyu ni suala la wazo lake uanzishaji wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ambayo imepewa jina la “Nelson Mandella African Institute of Science and Technology” inayoanzisha Vyuo Vikuu mbali mbali.

(a) Je, SMZ inaelewa kuwepo kwa Taasisi hiyo.

(b) Pamoja na mambo mengine Taasisi hiyo imeamua kujenga Vyuo Vikuu katika Kanda 3 muhimu za Bara la Afrika ambapo Afrika ya Kusini imepewa jukumu la kujenga chuo kwa ajili ya Teknolojia, Afrika ya Magharibi imepewa jukumu la Chuo cha Sayansi ya Maji na Afrika Mashariki imepewa jukumu la kuendesha Chuo cha Sayansi ya Uhai. Je, SMZ imejiandaa vipi kupeleka wanafunzi katika vyuo hivyo.

(c) Kwa kuwa Chuo cha Sayansi ya Uhai kinajengwa Arusha Tanzania. Ni vipi Zanzibar inashiriki katika ujenzi wa chuo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 lenye sehemu (a), (b) na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, *"Nelson Mandela African Institute of Science and Technology"* ni taasisi ya elimu ya juu ya Afrika ambayo imewekeza katika mafunzo na utafiti katika nyanja ya sayansi na teknolojia kwa mataifa ya Afrika. Taasisi hiyo imeanzisha Vyuo Vikuu na vituo vya utafiti vitatu vya kanda na kimoja wapo cha kanda ya Afrika ya Mashariki kimeanzishwa Arusha nchini Tanzania. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua kuwepo kwa taasisi hiyo.

b) Kwa vile chuo hicho ni kipya, wanafunzi wetu wengi hawajakifahamu lakini juhudi za kikitangaza zimeshaanza kuchukuliwa na naahidi kuwa siku za mbele tutapeleka wanafunzi kwenda kujifunza na kufanya tafiti mbali mbali ya sayansi ya uhai.

Serikali ya Zanzibar haishiriki katika ujenzi wa taasisi hiyo moja kwa moja kwa sababu taasisi hiyo ni ya kikanda na katika kutoa michango ya fedha tunawakilishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, vyuo hivi kama Mhe. Naibu Waziri alivyosema vinakusudia kuchukua wanafunzi kwa kuendelea na masomo ya *degree* ya pili na ili upate masomo ya *degree* ya pili maana yake umalize masomo ya *degree* ya kwanza. Hivi leo Zanzibar tumekosa kuwapa mikopo wanafunzi 1,300 kati ya 1,600 ambao wangeendelea na hii degree ya kwanza na kuendelea na *degree* ya pili. Hivyo, nini hatma yetu kielimu kama wanafunzi 1,300 wamekosa wakiendelea na masomo ya degree ya kwanza.

b) Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba vyuo hivi vinafadhiliwa na wahisani pamoja na Zanzibar

inawakilishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Spika, kwa kuwa elimu ya juu ni jambo la muungano, mimi naomba kujua mchango wetu kama Zanzibar ni shilingi ngapi na kama tunawakilishwa Zanzibar inajua kwamba tunawakilishwa kwa shilingi ngapi.

c) Kwa nini jambo hili la Muungano kwa mara ya kwanza lisijengwe Zanzibar badala ya Arusha-Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba kuna wanafunzi ambao mara hii hawakupata mikopo zaidi ya 1,300 kwenye wanafunzi 1,603. Mhe. Spika, nataka nikiri hilo, lakini kwanza ningependa Mhe. Mwakilishi ajue pamoja na Baraza lako tukufu kama hawa 1,603 ambao waliomba mikopo hii sio wote ambao walikuwa wana sifa ya kupatiwa hii mikopo. Ndani ya hawa Mhe. Spika, kuna wanafunzi ambao wamefanya fojari ya vyeti vya form IV au vya VI wamo, lakini ili upate mikopo hii jambo la kwanza ambalo unatakiwa ulete *admission letter* ya chuo husika. Mhe. Spika, mpaka hivi sasa wale wanafunzi ambao tumewapatia mikopo basi kuna nusu yake bado hawajaleta hizo *admission letter*. Mhe. Spika, ni kusema kuwa hawakuwa na sifa katika vyuo lakini walijaribu kuomba hii mikopo.

Mhe. Spika, jengine kama ambavyo nilijibu juzi hapa ni kwamba bajeti ambayo tunapewa na serikali ambayo inapitishwa hapa kwenye Baraza lako tukufu, ni kwamba haikidhi mahitaji ya wanafunzi ambao wanataka kwenda chuoni. Kwa hivyo, nikasema hapa kama tunajitayarisha na vyanzo mbali mbali vya mikopo kuzungumza na wenzetu wa mabenki, mifuko ambayo itakuwa haina riba kubwa.

Mhe. Spika, vile vile tumepitisha sheria hapa na hii sheria itatupa uwezo wa zile pesa ambazo tulikopesha kwa wanafunzi wetu kuweza kuzirudisha. Mhe. Spika, kwa taarifa ya Baraza ni kwamba tayari tumetoa bilioni 7 na bado pesa hizi hazijarudishwa kwenye bodi ya mkopo. Kwa hivyo, laiti ingekuwa bilioni 7 na bilioni 4 ambayo tumepewa kwenye bajeti, basi kwenye bilioni 15.3 ambayo tuliihitaji basi tungeweza kufika mbali. Kwa hivyo, niseme kwamba kama tuna vyanzo vyengine ambavyo tunavifuatilia na hivyo *inshaallah* mwakani mambo yanaweza yakabadilika. Lakini kama ambavyo nilieleza kwenye jibu mama kifungu cha © ni kweli kama Zanzibar moja kwa moja hatuchangii hii, lakini tunapeleka mchango wetu kwa sababu hii ni taasisi ya kikanda kwenye mfuko wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Spika, kwa taarifa ni kwamba chuo kile mpaka hivi sasa ni shilingi bilioni 67 ambazo zimetumika katika ujenzi wa chuo hicho.

Mimi naamini kama Wazanzibari ambao tuko katika *umbrella* hii ya *East Africa* basi na sisi pesa zetu zimo humu. Lakini ni kwa nini chuo hicho kisijengwe Zanzibar? Hayo yalikuwa ni maamuzi Mhe. Spika, wakati huo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa swali la awali lilikuwa zaidi limeelekezwa katika Chuo Kikuu hicho cha Kanda kinachoatokana na jitihada za mstaafu Nelson Mandela mimi nataka nirudie pale pale kwamba, kwa kuwa Zanzibar inahitaji watafiti, walimu wazuri zaidi katika vyuo vikuu vyake na inahitaji wataalamu mbali mbali katika taasisi zake zilizopo hapa.

Je, kuna utaratibu gani unaofanyika ili kuona kwamba Wazanzibari wanakwenda kujiunga na vyuo hivi hata kama wao wenyewe hawana taarifa kwamba vipo au havipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, utaratibu upo, kwa sababu ili uweze kuingia katika chuo hiki unahitaji kupasi vizuri masomo ya sayansi toka mwanzo. Kwa hivyo, moja ya mkazo wa Wizara ya Elimu ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanapenda masomo ya sayansi. Lakini vile vile kuhakikisha walimu wetu wana uwezo mkubwa sana wa kusomesha masomo hayo ya sayansi. Jitihada hizo tunazo na naahidi muda si mrefu tutafanikiwa.

Kuhusu lile suala alilosema kuwa japokuwa wanafunzi hawana habari kuwa chuo hicho kiko. Mhe. Spika, nilieleza kwenye swali mama kwamba wanafunzi watakwenda, tayari kwa taarifa ya Baraza lako wanafunzi wako tarehe 26 mwezi huu chuo hicho kinafunguliwa na kuna wanfaunzi 105 wataingia katika chuo hicho, lakini kati ya hao wanafunzi 26 wanatoka Zanzibar Mhe. Spika.

Nam. 80

Matumizi Ya Teknolojia ya "*Digital*"

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Kwa mujibu wa maendeleo ya Teknolojia ya Mawasiliano, ifikapo mwaka 2015 vyombo vyote vya Habari vinatakiwa kutumia Tekolojia ya *Digital* badala ya Analogi.

(a) Je, kwa upande wa vyombo vya Habari vya SMZ ikiwemo Radio na Televisheni ni hatua gani ambazo zimekwisha chukuliwa hadi sasa

ili vyombo vyetu hivyo visipitwe na wakati katika Teknolojia hiyo mpya.

(b) Ni madhara gani tutakabiliana nayo kama tukishindwa kubadilisha mfumo huo kwa wakati muafaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na maelezo kwamba, majibu wa *ITU – (International Telecommunication Union*) ifikapo mwaka 2015 Vyombo vyote vya Habari vinatakiwa kutumia teknolojia ya *digital* badala ya *analogy* na ndio lengo la *ZBC*.

(a) Kwa upande wa Vyombo vya Habari vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiweno redio na televisheni hatua ambazo zimechukuliwa kuelemisha watendaji wake, kupata vifaa vya kisasa, kuboresha maslahi ya wafanyakazi wote ili wawe na upendo na majukumu yao zaidi ili vyombo vyetu hivi visipitwe na wakati katika teknolojia hiyo mpya.

(b) Madhara tutakayokabiliana nayo kama tukishindwa kubadilisha mfumo huo kwa wakati muafaka kama ifuatavyo:-

1. Tutashindwa kuwashawishi walengwa (*audience*) kutizama na kuskiliza vyombo vyetu. Kwa maana hiyo, tutashindwa kuelimisha jamii.

2. Tutakosa ushindani wa habari.

3. Vyombo vitakosa uhamasishaji wa wananchi katika maendeleo yao ya kitaifa, kwa vile watazamaji wataangalia vyombo vyengine vya habari.

4. Kwenda kinyume na maamuzi ya Shirika la Mawasiliano Duniani (*ITU*) uliweka muda huo 2015 wa kufunga matangazo ya *analogy*.

5. Kukosa ulinzi idhaa yetu itakapounganishwa na matanganzo ya idhaa nyengine.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Katika vifaa vilivyoagizwa kwa ajili ya kutoka katika hali hii ya teknolojia na kuingia katika mfumo mzima wa *digital* ni kifaa kinachoitwa *DVB (T1)*. Kifaa hiki kilifika Zanzibar lakini baada ya kuonekana uwezo wake wa kazi na ushauri kutoka nchi za *SADC*, wizara ilishauriwa itafute kifaa chengine cha aina ya *DVB (T2)*. Wizara ilijitahidi kufanya hivyo na kuanza kuomba fedha ya ziada kutoka Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Je, kifaa hiki kwa ufupi *T2* kilifika? Na kama kilifika hiki cha *T1* kilikwenda wapi na wakati ni vifaa vyenye gharama kubwa sana.

Pili, kama hakikupatikana kwa sababu uwezo wa *DVB (T1)* ni mdogo kabisa na hautafika katika hali inayotakiwa. Wizara ina mpango gani kabla hatujaingia katika mfumo huu kikamilifu wa kidigitali, itafanya mpango wa kupata kifaa hiki ambacho ndicho kinachotakiwa hasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Mhe. Salim Abdalla kwa sababu yeye alikuwa ni Mjumbe wa Kamati tuliwaeleza maelezo yote na wanayo kwa umakini. Kwa kweli suala hili lipo katika wizara yangu na limeshafuatiliwa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa suala hili la mageuzi ya kiteknolojia mbali ya serikali na utekelezaji wake, lakini linawahusu zaidi wananchi kwa kuwa wao ndio watumiaji wakubwa wa televisheni pamoja na redio.Vile vile kwa kuwa mwaka 2015 ni keshokutwa Mwenyezi Mungu akituweka hai.

Je, serikali inawaandaa vipi wananchi au kuwahamasisha katika kupokea mfumo huu.

Lakini vile vile kwa kuwa suala hili la kiteknolojia linawahusu wananchi, serikali nayo kwa upande wake suala hili limefikia katika hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli wizara yangu inahamasisha vya kutosha ili kujua utumiaji huu mpya utakaoingia mwaka 2015.

Swali lako la pili Mheshimiwa sikulisikia vizuri.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, swali langu nilitaka kujua hatua ambayo serikali imeshafikia katika kujiandaa na mpango huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, serikali ina mpango maalum wa kuelimisha wananchi kuhusu utumiaji wa mfumo huu mpya na kuweka utaratibu maalum.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa katika Baraza lililopita 2005/2010 tulielezwa katika kikao kimoja na wizara hii, kwamba kuna vyombo maalum vitaagizwa na wizara kwa kuwapatia wale wenye televisheni za zamani ambazo sio digital katika kupata matangazo ya televisheni.

Je, utaratibu huo bado upo katika wizara au kila mmoja ataachiwe atafute chake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nashukuru Mhe. Spika, kwa ufupi ni kwamba kama alivyoeleza Mhe. Naibu kuwa mitambo tayari imeshafika na imeshafungwa Unguja na Pemba na wakati wowote itaanza kufunguliwa, ingawaje tulikuwa tunasubiri chombo kimoja tu, ni *battery* na si jambo kubwa. Tuliwahi kujaribu na ikaonesha Pemba tunashukuru, lakini hatutaki ku-*risk* tumesema mpaka tupate *battery* kwa sababu ndio inayohifadhi umeme, unapotokea mkato wa umeme basi matangazo yatakuwa yanaendelea kama kawaida. Kwa hivyo, mitambo yote imeshafungwa Unguja na Pemba iko tayari wakati wowote itaanza na hatutofika haya huo mwaka 2015 kama tulivyowekewa. Sisi tumejiwekea mwaka 2012 kwa nchi za *SADC* iwe tayari tumeshamaliza shughuli hiyo.

Vile vile tumeweka ratiba maalum ya kuja kuwaelimisha wananchi namna gani utaratibu wote unatakiwa uwe. Tuna imani kwamba hakutotokea matatizo makubwa kwa sababu tumejaribu kutafuta na ving'amuzi vile vile ambavyo vya kusaidia na kuhakikisha hakuna hasara kubwa kwa watu ambao wanatumia televisheni za analog yanaweza yakatokea mambo ya kitaalamu na zote zikawa zinafanya kazi bila ya matatizo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nilitaka kujua kwamba mpango huo wa wizara kuagiza hivyo vifaa ambavyoa wananchi wataunganisha na televisheni zao zile za zamani sio za *digital*, uko bado katika wizara au wataachiwa kila mwananchi anunue chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, wizara italishughulikia suala hili ili kuhakikisha kwamba watu wote wanapata vipindi bila ya kila mmoja kununua chake.

Nam. 28

Wananchi Waliovunjiwa Nyumba zao eneo la Mtoni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Katika mwaka 1997 kuna wananchi karibu 900 walivunjiwa nyumba zao katika maeneo ya Mtoni Kidatu, kwa sababu tofauti. Serikali iliunda Kamati kuchunguza maafa hayo na Kamati ilipendekeza kuwa waliovunjiwa walipwe angalau kifutia machozi. Pamoja na ushauri huo kukubalika Serikalini, lakini hadi leo kuna watu hawajalipwa na wengine tayari wameshatangulia mbele ya haki.

(a) Je, Serikali bado inao mpango wa kuwalipa watu waliovunjiwa.

(b) Kiasi gani cha fedha zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa wananchi waliovunjiwa.

(c) Je, Mhe. Waziri, Serikali ni lini itawalipa hicho kufutia machozi watu waliovunjwa nyumba zao hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye vifungu a, b, na c kama ifuatavyo:-

a) Wizara yangu inayo taarifa kuwa baadhi ya wananchi walilipwa fidia kabla ya kuanza kuvunjwa nyumba zao, kwa wale waliokuwepo kwenye vianzio vya maji Mtoni kwa ajili ya kunusuru vianzio hivyo. Baada ya hapo wananchi hao walirudia eneo hilo kinyemela, ndipo serikali ikavunja tena nyumba hizo. Serikali iliunda Kamati kwa ajili ya kuchunguza nani wanaostahiki kulipwa na kiwango gani cha malipo.

   Aidha, kamati hiyo ilimaliza kazi na kuiwasilisha taarifa yake serikalini ambayo ilikuwa na mapendekezo ya namna ya malipo na nani anastahiki kulipwa.

b) Mhe. Spika, kwa msingi wa majibu ya swali (a) wizara yangu haijatenga kiasi chochote cha fedha kwa mujibu wa malipo hayo.

c) Mhe. Spika, hadi hapo serikali itakapotoa maamuzi na muongozo wa namna gani wananchi hao walipwe ndipo wizara yangu itakuwa katika nafasi ya kujibu suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amesema wizara yake inayo taarifa kwa baadhi ya wananchi ambao ni 900 waliolipwa fidia kabla ya kuanza kuvunjiwa nyumba. Kati ya wananchi hao unaweza kunitajia 10 tu, wamelipwa nini na mwaka gani.

Pili, atakubali kwamba karibu miaka 14 – 15 kuna familia zimesambaratika kutokana na kuvunjwa nyumba hizo na hawana pahala pa kuishi na ukiangalia hii ni Serikali ya Kitaifa hivi sasa. Je, mna mpango gani kuwasaidia wananchi hao angalau viwanja wakaweza kujistiri wananchi hao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba muulizaji maswali ayarudie tena maswali yake, sikuyafahamu na sikuyasikia vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alisema wizara yake inayo taarifa kuwa baadhi ya wananchi walilipwa fidia kabla ya kuvunjiwa nyumba hizo, wananchi 900. Ninachotaka kujua mimi ni kutajiwa angalau wananchi 10 tu waliopewa fidia, kama ni nyumba za Michezani zilizojengwa vihi juzi au kiasi gani cha fedha na mwaka gani walilipwa.

Pili, Mhe. Waziri atakubaliana nami karibu mwaka wa 14 mpaka 15 sasa kuna familia zimesambaratika na hazina pa kuishi muda wote huu na tukiangalia hii ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Je, wananchi wale tumewafikiria nini? Kama hatuna uwezo mimi ningewaombea tuwasaidie japo kiwanja kimoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, suala la kwanza ni la kitakwimu nitamletea kwa maandishi na nitaliarifu Baraza hili wananchi wangapi wamelipwa na kiasi gani kimelipwa.

Lakini swali la pili ni wananchi ambao ni wangapi hawajalipwa mpaka leo na kama inawezekana tulipe kiwanja japo kimoja. Hili suala mbona lina utata, kwa sababu kama ni wananchi wengi na ukalipa kiwanja kimoja kitafidia wananchi hao waliosambaratika mahitaji yao?

Mhe. Spika, nadhani serikali iliunda tume kufanya makisio ya mahitaji ya fidia. Nasema tena nitaleta kwa maandishi lakini wapo wananchi waliolipwa fidia hizo. Lakini vile vile wapo wananchi hao hao waliolipwa fidia wakarudi tena kinyemela wakajenga nyumba katika maeneo hayo yaliyokatazwa. Kwa

hivyo, ndio maana malipo ya fidia yakazuiliwa ili tupate muda wa kuweza kuwajua wale waliorudia na wale ambao wanastahiki kulipwa fidia.

Mhe. Spika, zoezi hilo bado linaendelea na tukilimaliza tutaanza kulipa fidia kwa wale wanaostahiki kulipwa fidia, lakini kulipa kiwanja kimoja kwa wananchi 20 au 30 haitawezekana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuona uzito wa tatizo la ardhi Zanzibar na migogoro ambayo Wazanzibari imewakumba kwenye maeneo ya ardhi na viwanja pamoja na majumba, ameamua kwa makusudi kuunda tume ya serikali ikiongozwa na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwamba angalau tupunguze tatizo la ardhi.

Mhe. Waziri bajeti iliyopita mimi nilipomuhoji alithibitisha kwamba suala hili lipo serikalini na hadi leo hawajalipwa fedha kwa sababu hawana. Tofauti na majibu ya leo ambapo anasema wapo watu wamelipwa fedha. Hivyo Mhe. Waziri anakusudia kutwambia kwamba serikali haijui kile walichokifanya na kwamba takwimu zao zinagongana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, serikali inajua inachokifanya, serikali inakuwa na takwimu sahihi, lakini kwa sababu swali lililokuja leo la nyongeza sikujitayarisha kwa takwimu hizo ndio maana nikasema nitajibu kwa maandishi. Lakini serikali inajua idadi gani ya watu waliolipwa, kiasi gani wamelipwa na bado kama nilivyojibu swali la nyongeza la Mhe. Jaku kwamba serikali bado inaendelea kuwatafuta wale hasa wanaostahiki kulipwa, sio wale waliorudia kujenga katika maeneo yale yale.

Mhe. Spika, tukishawajua watu hao tutatenga fedha katika bajeti ijayo ya kuwalipa fidia wale wanaostahiki kulipwa. Serikali inajua hilo na serikali haibabaiki katika suala la takwimu wala suala la kilichoamuliwa kufanywa, tutafanya kwa mujibu wa maagizo ya serikali.

Nam. 64

Tatizo la Umeme

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Serikali ya awamu ya Sita ilifanya juhudi kubwa ya kuhakikisha kwamba tatizo la umeme lilokuwa likikikabili Kisiwa cha Pemba limetatuka na kubaki

historia. Baada ya juhudi hizo za kupongezwa limejitokeza tatizo kwenye Kisiwa cha Misali. Baada ya wataalamu kutoka Norway kuufikisha umeme Mkumbuu kuna waya uliobakia ulizamishwa baharini kwa ajili ya akiba endapo itatokezea dharura. Lakini wamejitokeza watu wasiopenda maendeleo wameanza kuuiba waya huo adimu na wenye thamani kubwa na watu hawa wanajulikana.

Je Mhe. Waziri, taarifa hiyo unaielewa. Kama unaielewa watu hawa wamechukuliwa hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kumejitokeza wizi wa waya wa akiba uliowekwa baharini katika kisiwa cha Misali. Wizara yangu umekuwa ikifuatilia kwa karibu tatizo hili. Wizara kupitia Shirika la Umeme baada ya kupata taarifa ya wizi huo kutoka kwa raia wema ilichukua hatua za kuwasiliana na vyombo vya ulinzi kwa hatua za kufanya upelelezi na hatimae jumla ya watuhumiwa wanne walikamatwa na kufikishwa katika Mahakama ya Mkoa wa Chake Chake Pemba. Baadhi ya watuhumiwa wengine hawajapatikana na wanaendelea kutafutwa.

Upelelezi wa kesi hiyo unaendelea na watuhumiwa wako nje kwa dhamana na huku wizara yangu ikisuburi uamuzi wa Mahakama.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyonegza. Je, Mhe. Naibu Waziri atawahakikishiaje Wazanzibari kuhusiana na ulinzi wa sehemu iliyowekwa waya huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nitachowahakikishia Wazanzibari kwamba baada ya kuibiwa waya huo basi waya uliobakia baharini tumeuwekea ulinzi mkali kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi kama nilivyozungumza.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala la umeme kisiwani Pemba limekabiliwa na limewezekana, lakini kisiwani Unguja bado tatizo hili la kukatika umeme mara kwa mara lipo. Je, Mhe. Naibu Waziri ni sababu zipi zinazofanya ukatikaji wa umeme ovyo kisiwani hapa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba tatizo la kukatika umeme mara kwa mara Zanzibar lipo, lakini tatizo hili litaondoka baada tu ya kumaliza mradi wetu ambao utaanza hivi karibuni wa kutoa laini mpya ya umeme kutokao Kiromoni hadi Fumba na kutoka Fumba hadi Mtoni.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa vile nchi yetu tunakabiliwa na watu waliokuwa hawapendi maendeleo na neno hili lipo zamani la kuibiwa umeme, leo umeme unaibiwa Unguja sasa hivi unaibiwa na Pemba umeme uliogharibu pesa nyingi sana. Atatuhakikishia vipi Mhe. Naibu Waziri kutoa adhabu kali kwa wabadhirifu hawa na ikawa ni funzo kwa wengine.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri wangu alipokuwa akijibu swali la msingi alisema suala la wizi wa umeme limesharipotiwa polisi, kesi iko Mahakamani, sasa tumesema tusubiri maamuzi ya Mahakama. Sisi hatuna uwezo wa kuamua ni adhabu gani mfanya kosa apewe.

Lakini alipokuwa anajibu swali la pili alisema ulinzi mkali utachukuliwa. Nasema hiyo ni ahadi lakini si rahisi kulinda nyaya za umeme kila zilipo. Jambo muhimu tunatumia askari shirikishi, askari wa kawaida na kadhalika lakini bado wizi unaendelea. Hasa pale unapokatika umeme kutoka Tanzania Bara kwa Unguja nzima au Zanzibar nzima ndio wakorofi wanapopata muda wa kuingia na kukata nyaya zetu za umeme. Kwa hivyo, tunatoa wito kwa wananchi wote wawe wakakamavu katika kutusaidia ulinzi wa miundombinu yetu iliyokuwa muhimu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 55

Kutofaidika na Rasilimali ya Kisiwa cha Mnemba

Mhe. Kazija Khamis Kona – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa wananchi wa Shehia nne za Wilaya ya Kaskazini "A" yaani Nungwi, Kijini, Pwani Mchangani na Matemwe, wanalalamikia kutofaidika na rasiliamali ya Kisiwa cha Mnemba ambayo imo kwenye wilaya yao, kupitia mradi wa MIMCA ulioanzishwa na Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini kisiwani humo.

(a) Je, Mhe. Waziri wizara yako inayo taarifa ya malalamiko hayo.
(b) Ni hatua zipi zilizochukuliwa na wizara yako katika kupata ufumbuzi wa malalamiko hayo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 55 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Wizara yangu inayo taarifa ya malalamiko hayo.

(b) Mhe. Spika, naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba MIMCA sio mradi bali ni hifadhi ya eneo la bahari inayozunguka Kisiwa cha Mnemba na maeneo jirani na kwamba nilitegemea kupata malalamiko zaidi kutoka kwa wavuvi wanaotumie eneo la bahari hiyo ambao pengine wanaathirika na hatua za hifadhi hiyo kuliko wananchi wa kawaida wa shehia nne za Nungwi, ambao ni Kijini, Pwani Mchangani na Matemwe.

Hata hivyo, malalamiko hayo mimi mwenyewe nimeyafuatilia kwa kwenda Matemwe na kuwaita walalamikaji mbele ya Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A", Afisa Tawala wa Wilaya, Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe na Jimbo la Nungwi, Mhe. Mwakilishi wa Viti Maalum kutoka Kaskazini "A", Sheha wa Shehia ya Matemwe na viongozi wengine.

Baada ya kuyasikiliza malalamiko yao, hatua ya kuyachunguza zinaendelea na sasa tumefikia hatua kubwa kabisa na mara tu tukimaliza kuyachunguza madai yao, Mizara ya Mifugo na Uvuvi itatoa uamuzi wake. Hadi hapo wizara itakapowapa uamuzi wa malalamiko yao ambapo ninaamini hatutochelewa yaani hatutochukua muda mkubwa kuanzia sasa. Kwa hivyo, nawaomba waendelee kuwa na subra.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wananchi ambao wamezungukwa na hifadhi hiyo ya Mnemba, moja kati ya malalamiko yao ni kwamba mwaka 2004 walikubaliana kwa mkataba kati yao na idara ya uvuvi kwamba mapato yatakayopatikana katika eneo hilo basi wapewe asilimia fulani, na walipewa mkataba. Baadae mkataba ule ukabainika kwamba hauna saini ya idara husika, kwa maana kwamba walifanyiwa udanganyifu kwa sababu ya kutokuelewa taratibu za mikataba. Kama hilo litabainika ni kweli nini kauli ya serikali.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Mhe. Spika, nakubali kwamba kulikuwa na mkataba baina ya hawa

wanakijini pamoja na *Mnemba Island Marine Conservation Area*. Sasa mkataba huo ndio uliosababisha matatizo haya yaliopo, kwa sababu zile fedha ambazo zilikubaliwa katika mkataba hawakulipwa wananchi. Ndio maana Waziri wa Mifugo na Uvuvi akenda huko na akakutana na watu hawa niliowataja, kwa niaba ya kusawazisha tatizo hilo. Kwa hivyo, tatizo hili ambalo linahusiana sana na fedha likikamilika. Sisi tulipokwenda kule tuliwaahidi kwamba mwezi huu wa Oktoba tutatoa jibu.

Kwa hivyo, naomba bado Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa wananchi wastahamili, Oktoba ndio hii inakaribia kumalizika na *Inshaallah* tutajitahidi kulimaliza suala hili katika kipindi kile kile tulichowapa ahadi.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora ndani yake

Mhe. Mwanasheria Mkuu:

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 49 kifungu cha 4(b) cha kanuni yako, naomba Baraza lako likubali kuahirisha Baraza au mijadala juu ya hoja iliyokuwepo mbele yetu ya Mwanasheria Mkuu, kujadili mapendekezo ya marekebisho ya baadhi ya sheria na kuweka masharti bora ndani yake kwa sababu zifuatazo.

Kwanza Mhe. Spika, mswada huu wa sheria ya madawa ya kulevya, tayari umeshafanyiwa marekebisho mara kadhaa katika Baraza lako tukufu na bado tunaendelea kufanya marekebisho.

Pia Mhe Spika, mswada huu wa sheria umefanyiwa marekebisho makubwa sana na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, marekebisho ambayo ni zaidi ya asilimia 50 ya mswada uliokuwa mbele yetu. Marekebisho ambayo tumeyapata sasa hivi asubuhi hii, ambapo Waheshimiwa Wajumbe wako hawatoweza hata kidogo kuweza kuyapitia marekebisho hayo kwa haraka haraka na kuweza kuyajadili na kutoa mawazo mazuri juu ya mswada uliokuwa mbele yetu.

Mhe. Spika, mswada huu wa madawa ya kulevya ni muhimu sana na hauhitaji kuripuliwa na unahitaji umakini wa hali ya juu katika kuupitisha. Mhe. Spika, kama ulivyoona katika semina ambayo tulihudhuria juzi, semina ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais juu ya athari ya madawa ya kulevya, vijana

wetu ambao wanaathirika. Lakini tumeona jinsi taarifa za wakubwa wanaoshiriki katika kufanya biashara hiyo haramu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, ikiwa hoja yangu itakubaliwa na Baraza lako tukufu, naomba mambo yafuatayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ayafanye wakati huo atakapowasilisha mswada huu kwa mara ya pili. Aambatanishe na mswada huo wa sheria jadweli itakayoonesha kifungu cha sheria ya zamani kitakachorekebishwa na kifungu kipya kinachotaka kuwekwa, ili kuweza kuwarahisishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kupima kati ya kifungu cha zamani na kifungu kipya.

Vile vile Mhe. Spika, hata katika haya marekebisho ambayo tumeyapitia sasa hivi, inaonekana hata Kamati ya Sheria na Utawala bado haijafanya vizuri marekebisho yake, kwa sababu ukiangalia katika marekebisho kwenye ukurasa wa 7, kuna kifungu kidogo cha 15, unasema; "kwa kuandikwa upya tafsiri ya neno chombo cha usimamizi wa fedha kwa kifupi CU" na kisomeke; "chombo cha uchunguzi wa fedha kwa kifupi CU maana yake ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 6(a) cha sheria hii". Ukiangalia sheria inayohusiana na suala la fedha haramu, kifungu cha 6(a) hakuna kabisa katika sheria hii.

Pia katika kifungu kidogo cha (3) nacho kimezungumzia, kwa kuandikwa upya tafsiri ya neno "kamati ya kitaifa" ambapo isomeke, "kamati ya kitaifa" maana yake ni kamati ya kitaifa ya pamoja kati ya kudhibiti usafirishaji fedha haramu iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 6(b) cha sheria hii. Sheria hiyo ya kifungu cha 6(b) kama ni sheria ambayo tuliipitisha katika Baraza lako tukufu, kama haikufanywa marekebisho, basi kifungu hiki pia hakipo.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, bado inaonekana hata haya marekebisho yaliyokuwa yamefanywa hayajakamilika. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu hicho nilichokitaja cha kanuni ya 49(4)(b) kwamba Baraza lako liahirishe hoja hii isijadiliwe, hadi hapo itakapofanywa marekebisho kamili. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza sina hakika labda wenzangu wazoefu zaidi wanisaidie. Lakini suala la kifungu cha 49(4)(b), kama kilivyoanza kusema kwamba hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila taarifa na moja ni hoja ya kuliahirisha Baraza na mjadala.

Sasa hoja iliyotolewa ya kuliahirisha Baraza inahusiana na hoja ya marekebisho ambayo yamefanywa kwenye mswada. Mhe. Spika, tukiangalia kwa mujibu wa utaratibu ambao unafuatwa katika kusimamia miswada, baada

ya kamati kuupitia na kupendekeza marekebisho yake, kamati ilifanya hivyo, iliupitia kwa makini na imetoa mapendekezo ya marekebisho.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Mjumbe aliyetoa hoja hii, kama atayapitia haya marekebisho yaliyofanywa na kamati. Kwa kweli ukiangalia na marekebisho zaidi ya uandishi. Kamati ilikuwa makini sana, sio marekebisho *substantive*. Ukiangalia ni kidogo, lakini zaidi ni marekebisho ya uandishi ili tupate mtiririko mzuri. Mimi nilidhani kwamba Baraza baada ya kuipa kamati hii makini kufanya kazi hii na kamati yenyewe kuyaona haya, nilidhani kwamba itaamini kwamba kamati ilifanya kazi yake kwa umakini.

La pili, kuhusu hoja ambayo Mhe. Mjumbe ameitoa na ambayo ni kuonesha kwamba labda kamati haikuwa makini nayo. Nadhani kwa heshima kubwa Mhe. Salmin Awadh labda yamemchanganya haya maneno yaliyotumika. Kwa sababu yaliyoingizwa kifungu cha 6(a) na kifungu cha 6(b) ni sehemu ya marekebisho ambayo yanapendekezwa na huu mswada. Kwa hivyo, ni kweli katika sheria sasa hivi hayamo, lakini yanaingizwa katika hii sheria sasa hivi, kwa hivyo yakishaingizwa kwenye huu mswada ina maana itakuwa ni sehemu ya sheria na kwa utaratibu wa mswada hivyo ndio unavyoandikwa.

Mhe. Spika, mimi nikiri kwamba kweli marekebisho yanaonekana ni mengi, lakini nadhani Waheshimiwa Wajumbe wakiyapitia wataona kwamba kamati ilifanya kazi nzuri. Pengine na kwenye hii taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati atakuja kueleza yale ambayo ameyaona. Sasa nilidhani kwamba kama ni mapema kutoa hoja hiyo kabla ya taarifa ya Mwenyekiti. Nilidhani labda kwanza tusome, tusikilize taarifa ya Mwenyekiti, halafu baada ya hapo ndio tuamuwe kuhusu suala hili.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mimi nafikiri kiti kingesaidiwa. Tukiahirisha tufanye nini, maana ingekuwa kuna jambo ambalo turejeshee kamati ikakae upya iangalie, halafu ituletee basi tungeweza kufanya hivyo. Lakini kama tunaahirisha mjadala ni kwa sababu tu ya kuwapa wajumbe muda wa kwenda kuowanisha marekebisho yale yaliyoletwa na kamati ambayo Mhe. Mjumbe pale anayasema ni mengi, ili iwe rahisi baadae kwa mjadala au kuna kitu *very substantive* ambayo kuahirisha kwetu kwa mjadala huu tunahitaji tuiambie kamati pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu wakakae upya ili kuweza kuyazingatia hayo, halafu baadae uweze kusomwa kwa mara ya kwanza mswada huu.

Labda hapa kiti kingesaidiwa. Hebu Mhe. Mjumbe mtoa hoja tupe taarifa zaidi, Mhe. Salmin Awadh.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, hoja yangu iko wazi, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba mswada huu wa sheria ulio mbele yetu umeshafanyiwa marekebisho mara kadhaa katika Baraza lako tukufu, na bado tunaendelea kuufanyia marekebisho. Hii inaonesha jinsi mswada huu ulivyokuwa *very sensitive* katika suala zima la sheria.

Mhe. Spika, tumepokea marekebisho haya ya sheria yenye kurasa 10 na mswada wenyewe una kurasa 9, zaidi ya asilimia 50 ni marekebisho. Kama unavyojua Mhe. Spika, mswada unapowasilishwa kwa Waheshimiwa Wajumbe unahitaji kupata siku 21, ili waweze kuupitia. Lakini marekebisho haya ya sheria tumeyapata leo. Kama Mhe. Mwanasheria Mkuu alivyosema kuwa kuna baadhi ya maeneo yamebadilishwa herufi na mambo mengine, lakini na mengine yamebadilishwa vifungu kabisa. Kwa hivyo, kunahitaji umakini wa hali ya juu katika kuujadili mswada huu ili kesho na keshokutwa tusijetukaletewa tena marekebisho ya sheria hii.

Kwa hivyo, kulingana na hiyo na kwa mujibu wa vifungu vilivyotajwa kwenye kanuni, haidhuru Mhe. Mwanasheria amekanusha, lakini ukiangalia kifungu cha 83(11)(1)(3) pia vinatupa nafasi ya kuahirisha mswada huu, ili Baraza lako lisifanye shughuli hii kwa kuripua ripua.

Mhe. Spika, nadhani kuahirisha Baraza hili tukapata muda wa kuujadili, ili tukija hapa tuje na kitu makini kilichokuwa bora, nadhani ni suala la busara zaidi kuliko hivi ambavyo tunavyotaka twende. Kwa hivyo, bado mimo hoja yangu ni kwamba marekebisho ni mengi, yameundanisha mambo mengi na kama nilivyosema kwamba kuna vifungu vingine vya sheria ambavyo vimenukuliwa humu na kamati, pia kwenye hiyo sheria ya mwanzo havimo, ni vifungu vyengine vipya. Sio suala la kwamba tuweze kuowanisha tu kama nilivyosema mwanzo, yale yalikuwa ni mapendekezo yangu ya pili, kwamba Mhe. Mwanasheria atakapokuja na mswada kwa mara ya pili atutayarishie jadweli.

Mhe. Spika, suala hili hata Bunge la Jamhuri ya Muungano wanafanya hivyo. Nimeshawahi kushiriki vikao vya kamati mara mbili, wanapowasilisha marekebisho ya sheria wanakuwa wanaweka jadweli ambayo wanaweka kifungu cha zamani kinachopendelezwa kufanyiwa marekebisho na kifungu kipya. Suala hili Mhe. Spika, niliwahi kulizungumza katika Baraza lililopita, ili tuone kwamba tunafanya marekebisho mapya, basi suala hili Mhe. Mwanasheria alifanye ili liweze kurahisisha kujua Waheshimiwa Wajumbe ni kifungu kipi cha sheria kinachotakiwa kurekebishwa na kifungu kipi kipya ambacho kinataka kuwekwa. Hiyo ndio hoja yangu Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nataka nithubutu kusema kwamba nimefahamu *concern* ya Mhe. Salmin Awadh. Lakini nataka nisaidie tu kidogo, chimbuko la mswada wa madawa ya kulevya kufanyiwa marekebisho kipindi hiki, umetokana na mswada wa fedha haramu kufanyiwa marekebisho. Kwa sababu fedha haramu kwa kiwango kikubwa zinatokana na madawa ya kulevya. Kwa hvyo, isingewezekana kuufanyia marekebisho mswada wa fedha haramu tukauwacha mswada wa madawa ya kulevya. Marekebisho yale yalikuwa yanaowana, ndio maana tunaufanyia marekebisho nao mswada wa madawa ya kulevya.

La pili, wajumbe wa kamati walipata bahati, wakakaa na Mwanasheria Mkuu na mawaziri wawili wanaohusika na marekebisho hayo. Nikiwemo mimi kwa upande wa sheria ya fedha haramu na Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej kwa upande wa madawa ya kulevya. Wakati ule anachokizungumza Mhe. Salmin Awadh, liliwasilishwa bango kitita hayo ndio mazingira anayoyataka Mhe. Salmin Awadh na wakaona kwamba kifungu hiki tunakirekebisha kutoka hapa kwenda hapa.

Lakini na mimi nataka nimuombe tu Mhe. Salmin Awadh kwamba kiutaratibu, kwa wajumbe ambao hawakuwepo katika kamati ni vyema tukampa nafasi Mhe. Mwanasheria Mkuu akawasilisha, tukampa nafasi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati akawasilisha, ili wale ambao hawakuwepo katika kamati wakapata *clause* na *highlight* nini kilichoongelewa kule. Kutoka hapo sasa Mhe. Spika, tunaweza tukaahirisha, ili kutoa nafasi kwa wajumbe wako kuweza kupitia yale yaliomo humu na kutafakari yale yaliyowasilishwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, pamoja na Mhe. Mwenyekiti wa kamati, labda mpaka jioni tukarudi kwa mjadala.

Mhe. Spika, hiyo ndio ambayo nilikuwa nataka nimuarifu Mhe. Salmin Awadh. Mimi napenda kumuita *Doctor* huyu, Mhe. Dr. Salmin Awadh kwamba bango kitita kwa kweli litawasaidia sana wajumbe wako, hiyo ambayo anaitaka yeye, sisi tunaita bango kitita itawasaidia sana wajumbe wako kuweza kufahamu hasa na haya yapo pia Mhe. Spika, sio kama hayapo, yapo na yametayarishwa na Afisi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kushirikiana na afisi zetu na yanaweza pia yakaletwa wakati wa mjadala. Mimi nadhani kwamba tuwaruhusu Mwanasheria Mkuu na Mwenyekiti wawasilishe baadae labda kama tutaahirisha kuanzia hapo ili twende tukatafakari kwa pamoja, pamoja na hilo bango kitita litakuja ili jioni tuweze kufanya mjadala.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mimi nafikiri haya masuala yana umuhimu kwa pande zote mbili, kupata wasaa Waheshimiwa Wajumbe

mkajadili vizuri ni jambo muhimu sana na tutasaidia serikali katika kufikia maamuzi juu ya marekebisho ya sheria mbali mbali ambazo ziko katika mswada huu. Kwa hivyo, hapo ni suala la namna gani Waheshimiwa Wajumbe kuweza kujadili vizuri na kuisaidia serikali, kumsaidia Mwanasheria Mkuu pamoja na zile wizara ambazo zinahusiana na marekebisho ya mswada huu.

Lakini wakati huo huo kuna umuhimu wa jambo hili kwa umuhimu wake kama tulivyoona pale kwenye semina. Juzi tuliona sote kwamba kwa kweli kuna umuhimu mkubwa sana. Pale tulitoa wito kwamba hiyo sheria iletwe, tena kulikuwa na wito hata wa kuombwa Mhe. Waziri hapa na yeye alete sheria ya *corruption,* kumbe kunakuwa na kitu fulani, yaani tuhuma za *corruption* nyingi kupitia katika masuala haya ya madawa ya kulevya. Hiyo pia akaombwa nayo ije haraka, tena ikaelekezwa hasa katika mkutano ujao wa Januari. Sasa hii inathibitisha umuhimu wa jambo hili kwamba lifanyike katika wakati muafaka huu.

Kama hivyo ndivyo, basi mimi naelekeza kwamba mswada huu uwasilishwe na Mhe. Mwanasheria Mkuu, tumuombe Mhe. Mwenyekiti na yeye atowe maoni kama walivyoona, kama kuna tatizo la kuowanisha hapo tunaweza tukasema. Kwa kweli, hoja yake sio kwamba tuahirishe mswada huu sivyo. Hoja yake tuahirishe mjadala. Sasa tuone baada ya hapo kama tunaweza tukatowa muda kidogo ili wajumbe wakapitia marekebisho yale kwa sababu ya muda mfupi uliopatikana, wakaweza kuowanisha na hatimaye jioni kuweza kuja na kuona vipi tunaweza tukaendelea na mjadala wetu.

Kwa hivyo, nitowe maelekezo kwamba tumruhusu Mhe. Mwanasheria Mkuu awasilishe na baadae Mhe. Mwenyekiti, tumruhusu na yeye awasilishe maoni ya kamati na kutokana na maelezo yatakayotoka katika pande zote mbili basi tunaweza tukajua ni kwa kiasi gani jambo hili tunaweza tukaahirisha mjadala wake hadi jioni ili kuweza kufanya kitu kizuri zaidi. Mhe. Mwanasheria Mkuu wasilisha.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili mswada wa sheria ya kubadilisha baadhi ya sheria na kuweka masharti bora ndani yake.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii pia kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mswada huu. Aidha, nakushukuru kwa miongozo yako mbali mbali uliotupa wakati wa matayarisho ya kuwasilisha mbele ya Baraza hili.

Mhe. Spika, napenda pia kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza hili tukufu, kutokana na michango, maoni na miongozo yao ambayo imechangia sana kuufanya mswada huu kuwa bora zaidi. Marekebisho muhimu na ya msingi yaliyopendekezwa na ambayo nimeyakubali, yameondoa utatanishi katika baadhi ya vifungu na kuweka mtiririko bora zaidi wa kiuandishi.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya mswada huu ni kufanya marekebisho katika sheria tatu tofauti ambazo ni:

1. Sheria ya Kuzuwia Dawa za Kulevya Nambari 9 ya mwaka 2009,
2. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nambari 7 ya mwaka 2004, na
3. Sheria ya Kudhibiti Usafishaji Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu Nambari 10 ya mwaka 2009.

Mhe. Spika, mswada huu umegawika katika sehemu 4.

Sehemu ya Kwanza, inahusu utangulizi ambayo imeeleza jina fupi la sheria inayopendekezwa na tarehe ya kuanza kutumika.

Sehemu ya Pili, inahusu marekebisho ya sheria ya kuzuwia dawa za kulevya nambari 9 ya mwaka 2009.

Madhumuni makubwa ya marekebisho ya sheria hii ni kuweka muundo mpya wa Tume ya Taifa ya kudhibiti na kuratibu dawa za kulevya Zanzibar. Katika muundo mpya tume itakuwa ikiongozwa na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, akiwa ni Mwenyekiti. Hii inatokana na muundo mpya wa serikali uliotokana na mabadiliko ya 10 ya katiba ya Zanzibar yaliyofanywa na Baraza hili tukufu mwaka 2010.

Kabla ya marekebisho hayo tunayopendekeza, tume hii ilikuwa ikiongozwa na Waziri Kiongozi, nafasi ambayo imeshafutwa na katibambali muundo wa tume, marekebisho mengine yanaelezea akidi ya vikao vya tume na uwezo wa tume kupanga utaratibu wa mwenendo wa vikao vyake. Aidha katika sehemu hii inayopendekezwa kuanzishwa kwa Kamati Tendaji pamoja na majukumu yake.

Vile vile inapendekezwa kufanya marekebisho kwa baadhi ya adhabu zinazotokana na makosa mbali mbali yanayohusu utumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, marekebisho mengine katika sheria hii ni kuongezwa kwa dajuweli linaloelezea makosa, adhabu pamoja na mahakama itakayosikiliza makosa hayo. Hii itarahisisha usikilizaji wa kesi zinazohusiana na uingizaji wa dawa za kulevya nchini kwetu na pia kwa watumiaji wa madawa hayo hapa Zanzibar.

Katika kuimarisha zaidi utekelezaji wa marekebisho hayo, tumeongeza sehemu mpya ya tatu inayohusu marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2004. Marekebisho hayo yamo katika Mswada tuliochapisha bali ni sehemu ya marekebisho yaliyofanywa wakati wa majadiliano na kamati na kukubaliwa. Hivyo, marekebisho hayo yameoneshwa kama sehemu ya mapendekezo ya kamati.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu iliopo katika mswada kutokana na marekebisho hayo niliyoyaeleza awali tunapendekeza isomeke kuwa ni sehemu ya nne kufuatia marekebisho tuliyofanya na vifungu vitabadilika kutokana na marekebisho mapya. Sehemu hii inahusu marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Usafishaji Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu Nam. 10 ya mwaka 2009.

Mhe. Spika, kama unavyofahamu kwamba masuala ya kupambana na fedha haramu yanasimamiwa na Mikataba ya Kimataifa, ambayo Jamhuri ya Muungano imeridhia. Chini ya mikataba nchi wanachama zinatakiwa ziwe na mfumo unaokubalika kisheria. Aidha zinatakiwa ziwe na taasisi zenye ufanisi katika kusimamia sheria hiyo.

Tutakumbuka kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilipitisha Sheria ya Kupambana na Fedha Haramu ya mwaka 2006, ambayo ilionesha pia kwamba itatumika Zanzibar. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikataa sheria hiyo kutumika Zanzibar, kwa vile sehemu kubwa sheria hiyo inahusu mambo ya muungano.

Vile vile kama tunavyofahamu kuwa baada ya mtafaruku huo wa sheria hiyo iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, Baraza hili tukufu lilipitisha Sheria ya Zanzibar kuhusu Kupambana na Fedha Haramu, ambayo kupitia mswada huu ndio tunayoirekebisha.

Mhe. Spika, chini ya taratibu za kimataifa nchi zote zimekubaliana kufanyiwa tathmini, kama sheria na taratibu zao za kupambana na fedha haramu zinatimiza vigezo vya kimataifa vinavyotolewa na Tume Maalum ya Fedha ya Umoja wa Kimataifa, yaani *Financial Action Task Force*.

Tathmini hizo hufanywa kupitia taasisi mbali mbali zilizokubalika. Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Jumuia

Nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika ya Kupambana na Fedha Haramu, ambayo Makao yake Makuu ni Dar-es-Salaam Tanzania. Jumuia hiyo ndio iliyokubaliwa kuwafanyia tathmini wanachama wake kwa niaba ya Jumuia ya Kimataifa.

Madhumuni makubwa ya marekebisho tunayopendekeza yanatokana na mapendekezo ya Kikundi cha Kushughulikia Kupambana na Usafishaji wa Fedha Haramu cha Jumuia ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Mashariki. Kikundi hicho kilifanya uchunguzi wake mwaka 2009 hapa nchini Tanzania ikiwemo Tanzania Bara na Zanzibar.

Tathmini hiyo ilibainisha kuwa Tanzania ni nchi ambayo haifuati ipasavyo vigezo vya kimataifa vya kupambana na fedha haramu, kwa vile sheria zake pamoja na taasisi zake zina mapungufu kadhaa. Sehemu kubwa ya kasoro hizo zilihusu Tanzania Bara, hata hivyo zipo zilizohusu Zanzibar.

Baada ya tathmini hiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ililazimika kuandaa mpango kazi, yaani *Action Plan* wa kushughulikia kasoro hizo zilizogunduliwa ndani ya miaka mitatu. Mpango huo uliidhinishwa na Mkutano wa Mawaziri nchini Malawi Novemba, 2010, ambapo Zanzibar pia iliwakilishwa.

Aidha utekelezaji wa mpango huo kama unakwenda vizuri ulifanyiwa tathmini nchini Ufaransa na Jumuia ya Kimataifa mwezi wa Mei mwaka huu, ambapo Zanzibar iliwasilisha maendeleo ya utekelezaji. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya nchi hizo inawajibika kufuata mapendekezo hayo kwa kurekebisha sheria hii, ili kutekeleza viwango vya kimataifa katika kupambana na usafishaji wa fedha haramu.

Mhe. Spika, miongoni mwa marekebisho hayo ni kama yafuatayo:-

1. Kukitambua Kitengo cha Usimamizi wa Fedha pamoja na Kamati ya Kitaifa ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu kama ilivyoanzishwa na Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 ya Sheria ya Tanzania, kufanyakazi hapa Zanzibar bila ya kuwa na kitengo hicho sheria yote nzima haiwezi kusimamiwa ipasavyo.

2. Kuongezwa baadhi ya vifungu vipya kama ifuatavyo:-

    (a) Kifungu cha 6(A) na (B), ambavyo vinaeleza kufanyakazi kwa *FIU* pamoja na Kamati ya Kitaifa ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu hapa Zanzibar.

(b) Kuongeza kifungu cha 9(a) kinachoeleza hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya taasisi zinazojitegemea endapo zitakiuka masharti ya sheria hii.

(c) Kifungu cha 14(a) kinachoeleza hatua za kiutawala, yaani *administrative functions* zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya mtu au taasisi yoyote itakayokiuka masharti ya sheria hii.

(d) Kifungu cha 17(a) kinachoeleza ulinzi dhidi ya mashahidi na watoa taarifa.

(e) Kifungu cha 18(a) kinachoeleza wajibu wa msimamizi wa taasisi za fedha.

(f) Kifungu cha 81(a) kinachoeleza wajibu wa Taasisi za Fedha kupeana taarifa miongoni mwao zinazohusiana na kazi zao.

(g) Kifungu chengine kipya cha 81(b) ambacho kinaweka adhabu za jumla dhidi ya mtu au taasisi itakayokiuka masharti ya sheria hii.

Marekebisho mengine madogo madogo ni kama yanavyoonekana katika mswada.

Mhe. Spika, kama marekebisho haya yatakubaliwa, basi yataijengea heshima Zanzibar na kuondoa ule wasi wasi uliokuwepo, kuwa Zanzibar haina na nia ya dhati ya kupambana na fedha haramu baada ya kuikataa ile sheria ya Muungano na kutunga sheria yake.

Mwisho Mhe. Spika, kwa muhtasari hayo ndio mapendekezo ya marekebisho ya Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Baadhi ya Sheria na kuweka Msharti bora ndani yake. Naomba Waheshimiwa Wajumbe waupokee na kuujadili na hatimaye kuupitisha mswada huu kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja imetolewa ijadiliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, hoja imeungwa mkono kumaanisha kwamba inaweza kujadiliwa. Kwa hivyo, naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Ifuatayo ni Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti bora ndani yake.

Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukuwa fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu.

Mhe. Spika, pili napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada huu muhimu wa Kurekebisha Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake.

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inatoa mkono wa pole kwako wewe binafsi na kwa familia ya Marehemu Mhe. Mussa Khamis Silima aliyekuwa Mjumbe wa Baraza hili kupitia Jimbo la Uzini, ambaye pia alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi na aliyekuwa Mbunge wa Bunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia nafasi tano za Baraza la Wawakilishi kufuatia kifo cha mpendwa wetu huyo.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu amlaze mahali pepa peponi, amuondoshee adhabu za kaburi na sisi tulobaki atujaalie khatma njema. Aidha, awajaalie wafiwa wote kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu, Amin.

Mhe. Spika, kwa moyo wa dhati napenda kuipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa kuundaa na hatimaye kuuwasilisha mswada huu kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ili kuipa fursa kamati yetu kutoa mapendekezo yake kabla ya kuwasilishwa mbele ya Baraza letu tukufu kama Kanuni ya 111(f) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi inavyoelekeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mswada ulipo mbele yetu umejumuisha Wizara mbili naomba uniruhusu pia kuwashukuru, Mawaziri wa Wizara hizo kama ifuatavyo:-

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais ambaye pia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Omar Yussuf Mzee Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais, ambaye pia ni Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Vile vile nimshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa jinsi alivyotoa ufafanuzi katika mswada wetu huu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo naomba niwapongeze na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuupitia kwa makini mswada huu na kutoa mapendekezo yao, ili kuimarisha zaidi. Mhe. Spika ili kuzipa nguvu shukurani zangu hizo napenda kuwatambua Wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
8.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
9.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu.

Mhe. Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naomba kidogo nitoe maelezo kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, hivi sasa vijana wetu wengi waliokuwa wakitumia dawa za kulevya wameamua kwa hiari zao kujikusanya pamoja kwa lengo la kuachana na dawa hizo haramu pamoja na kuwashajihisha na watumiaji wengine kuachana na shughuli hiyo ovu, ambayo hulipelekea taifa kupoteza nguvu kazi ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kwa kuwa vijana hawa waliokuwa wakitumia dawa za kulevya kwa hiari zao wameamua kuachana na shughuli hii, na kuwa vijana hawa hukaa kwenye nyumba walizozianzisha kwa muda maalum na wakitoka katika nyumba hizo hawana shughuli madhubuti wanayoifanya kutoka na ukosefu wa mitaji, na kwamba wanataaluma au fani mbali mbali na kwa kuwa baadhi ya vijana hawa hutengwa na familia zao.

Tunaiomba Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na jamii kwa ujumla kuwaamini vijana wetu hao na kuwapatia mitaji, ili waweze kuendesha shughuli zao binafsi kwa lengo la kujikimu maisha yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sambamba na hayo tunamuomba Makamu wa Kwanza wa Rais kuzitekeleza kwa vitendo ahadi mbali mbali alizozitoa wakati alipokuwa anazitembelea *Sober Houses* mnamo mwezi wa Mei mwaka huu huko Pemba. Aidha, tunaiomba serikali kujenga nyumba za kuwahudumia watu wanaoachana na dawa za kulevya kama inavyowahudumia Watoto Yatima na Wazee Wasiojiweza.

Kwa kuanzia tunaishauri serikali kuzisaidia *Sober Houses* ingawa ni Taasisi Zisizo za Serikali, lakini zina malengo mazuri kwa mustakbali mzima wa maendeleo ya nchi yetu. Kwani katika nyumba zao hizo wanakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo ukosefu wa chakula, usafiri, dawa na hata kodi za kulipia majengo hayo.

Mhe. Spika, tunaomba haya kwani endapo vijana hawa watakaa bila ya shughuli yoyote, badi kuna uwezekano mkubwa wakushawishika kurudia tena katika shughuli hiyo haramu kitu ambacho ni kinyume na matarajio yao na ni jambo ambalo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala hailipendelei lijitokeze.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nije moja moja kwenye Mswada. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake umekuja kufuatia, pamoja na mambo mengine kurekebisha baadhi ya Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya, Nam. 9 ya 2009 na Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu, Nam. 10 ya 2009, ili kukidhi hali halisi tuliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, kamati yetu imefanya kazi ya kuupitia mswada huu kwa kina kifungu kwa kifungu na kutoa maoni na mapendekezo yake kwa baadhi ya vifungu kwa kadri ambavyo kamati imeona inastahiki.

Mhe. Spika, tuliongeza baadhi ya maneno kwa baadhi ya vifungu vya mswada vilivyokuwa maelezo yake hayakidhi haja, ili kuvifanya vifungu hivyo visomeke kama ilivyokusudia.

Baadhi ya vifungu hivyo kwa Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya ni kama ifuatavyo:- Kifungu cha 6 cha Mswada kinachorekebisha kifungu cha 4 cha Sheria Mama kwa kuingiza vifungu vipya vya 4A, 4B na 4C, kamati ilipendekeza kufanywa marekebisho katika kifungu cha 4A kijifungu cha (1)(c) kwa kuongezwa maneno ‘Mwanasheria wa Serikali’ na kufutwa maneno ‘Mtu mmoja’.

Aidha, kifungu cha 4C kijifungu cha (2)(b) tumependekeza kuongezwa neno ‘isiyopungua’ baina ya neno ‘ya’ na ‘Shahada’, ili kutoa nafasi zaidi hata kwa yule mtu wenye zaidi ya Shahada ya Kwanza kuwa Mkurugenzi Mtendaji. Mhe. Spika, marekebisho mengine ni kama yanavyoonekana katika waraka wetu wa Mapendekezo ya Marekebisho.

Marekebisho kama hayo tuliyafanya kwa baadhi ya vifungu katika Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu. Baadhi ya vifungu hivyo ni; Kifungu cha 21 cha Mswada kinachorekebisha kifungu cha 2 cha Sheria mama, kimependekezwa kurekebishwa katika kijifungu cha (ii)

cha kifungu hicho cha Mswada kwenye tafsiri ya neno ‘Msimamizi’ katika mstari wa tatu kuongezwe maneno ‘Uwekezaji na’ baina ya neno ‘ya’ na ‘Kukuza’ ili jina la taasisi hiyo lisomeke kwa ukamilifu wake. Aidha, katika mstari wa pili kutoka chini liongezwe neno ‘yeyote’ baina ya neno ‘mwengine’ na ‘ambaye’.

Mhe. Spika, kamati yetu pia imefanya marekebisho kwa kuweka uwiano wa maelezo ya vifungu baina ya Mswada wa Kiingereza na Kiswahili kwa Sheria zote mbili. Kwa upande wa Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya baadhi ya marekebisho hayo ni; Kifungu cha 4 cha Mswada kinachorekebisha kifungu cha 2 cha Sheria Mama katika kijifungu cha (a) tafsiri ya neno ‘Mkemia wa Serikali’ imependekezwa isomeke; “Mkemia wa Serikali” maana yake ni Mkemia wa Serikali aliyeteuliwa chini ya masharti ya Sheria ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali’.

Aidha, kijifungu cha (c) tafsiri ye neno ‘dawa zinazokatazwa’ imependekezwa isomeke; ‘dawa zilizokatazwa’ maana yake ni dawa yoyote ambayo serikali inaweza kutokana na taarifa ilizonazo kwamba upo uwezekano wa kutumika, kuzalisha au kutengeneza dawa za aina ya nakotiki au saikotropiki au ni kinyume na masharti ya Mikataba ya Kimataifa, kwa kutoa tangazo katika Gazeti Rasmi la Serikali kutangaza kuwa ni dawa zilizokatazwa’.

Ama kwa upande wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu. Baadhi ya vifungu tulivyopendekeza kufanyiwa marekebisho kama hayo ni; Kifungu cha 21 cha Mswada kinachorekebisha kifungu cha 2 cha Sheria Mama katika kijifungu cha (vii)(u) neno la kwanza ‘uharamia’ limependekezwa lisomeke ‘upatu haramu (*pyramid scheme*)’.

Aidha, Kifungu cha 31 cha Mswada kinachorekebisha kifungu cha 17 cha Sheria mama kinachoongeza kifungu kipya cha 17A, Kifungu cha 17A(1)(a) cha Sheria Mama kimependekezwa katika mstari wa pili kutoka juu kuongezwa maneno ‘mkutano kwa njia ya’ baina ya neno ‘vile’ na ‘video’ ili maneno haya yaendane na maneno ya Mswada wa Kiingereza yasemayo ‘*video conferencing’*.

Mhe. Spika, katika kuimarisha utendaji wa sheria hizi tumeongeza pia baadhi ya vifungu. Kwa mfano; kwa Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya tumehisi ni busara kuongeza kijifungu kipya cha (j) mara baada ya kijifungu cha (h) cha Kifungu 4(2) cha Sheria mama ambacho imependekezwa kisomeke, ‘Waziri mwenye dhamana ya Sheria’.

Tumependekeza hili ili kuimarisha utendaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Sambamba na hayo tumependekeza kuongezwa kijifungu kipya cha (4) mara tu baada ya kijifungu cha (3) cha kifungu cha 5 cha Sheria mama ambacho kisomeke; 'Tume itapanga taratibu za vikao vyake yenyewe'. Aidha, mapendekezo kama hayo tuliyapendekeza yaingizwe katika kijifungu kipya cha (3) mara tu baada ya kijifungu cha (2) cha kifungu cha 5A.

Pamoja na hayo, tumeongeza 'Sehemu ya Tatu' mara baada ya 'Sehemu ya Pili'. Mhe. Spika, ili kuunusuru muda wako nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waupitie kwa kina waraka wetu, ili wavione vifungu vyengine tulivyovipendekeza kuingizwa, kwa kuwa haitokuwa busara kuvieleza vifungu yote hapa.

Mhe. Spika, kwa kuhitimisha, haya ndio maelezo ya uchambuzi wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa muhtasari. Napenda kuchukuwa nafasi hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuuchangia Mswada huu muhimu na hatimaye kuupitisha, ili tujenge Zanzibar yetu mpya na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwezesha kufika pale tulipokusudia.

Mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

TAARIFA

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 82(2) kamati iliyopelekewa mswada haitokuwa na uwezo wa kufanya mabadiliko ya mswada huo kwa mujibu wa kanuni hii. Lakini inaweza kumshauri waziri anayehusika na mswada huo kufanya mabadiliko katika mswada wakati umeshafika kwenye Baraza, isipokuwa masharti ya kanuni hii yatatumika pia kwa Mswada wa Mjumbe.

Kutokana na maelezo hayo, naomba Mhe. Spika, utuamulie wakati wanaoleta miswada zaidi ni upande wa serikali na miswada haiji kamili, kwa sababu kwa mujibu wa kanuni hii mara baada ya kamati kumaliza wao wanatarajiwa wauandike tena ule mswada ndio waulete hapa kwa mujibu wa kanuni hii. Kwa hivyo, tutaendelea kufanya makosa haya kila siku kwa kuletewa vipande vipande. Kwa hiyo, tunaomba hekima yako.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, alichosema Mhe. Mjumbe sehemu moja ni sahihi kabisa kwamba kamati inaweza kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika mswada.

Nadhani nilipokuwa nikiwasilisha au kutoa hoja nilisema hilo kwamba kamati ilitushauri kufanya marekebisho, nimeyakubali marekebisho hayo ambayo kamati imeyapendekeza na hilo nililisema kwa wazi kabisa.

Sasa nasema tuna-*establish practice* hapa kwamba baada ya kamati kufanya marekebisho, basi wanaleta mapendekezo ya marekebisho yao kama waziri naye yapo, ambayo hayakubali anayo marekebisho ya ziada basi na yeye analeta *shadow of amendment* ya kwake. Hivyo, haya yaliyopendekezwa na kamati nimeyakubali kwa asilimia mia moja na ndio maana sikuleta *shadow of amendement*.

Mhe. Spika, nadhani miswada yote iliyopita utaratibu umekuwa ndio huo, lakini ikiwa sasa tutakuwa na utaratibu wa kuleta jaduweli kama ambavyo Mhe. Salmin Awadh Salmin alileta nafikiri si jambo baya.

Kwa hivyo, tutakapokuwa na huu utaratibu wa kusomwa mara mbili, basi nadhani litatupa muda kwa sababu tatizo hili limetokana na muda, ambao tunakuwa nao tokea kusomwa mara ya kwanza tukae kwenye kamati mara ya kwanza na pengine mpaka mara ya pili.

Kutokana na hali hiyo, nadhani utaratibu mpya utatupa ufumbuzi wa tatizo hili. Lakini Mhe. Spika, nafikiri kwa hili marekebisho yalishatolewa kwa kina, pia ombi limetolewa kwamba tupate muda labda Waheshimiwa Wajumbe kuoanisha. Hivyo, nadhani baada ya kuyasoma wameyaona mengi ni marekebisho ya kiuandishi.

Kwa hiyo, nafikiri tutakapopata muda wa kuyapitia haya marekebisho, basi tutaona kile ambacho kimerekebisho na kamati imependekeza, yale tuliyoyakubali na wataona hasa kwamba mswada hivi sasa utakuwa unasomeka vizuri zaidi.

Kwa maana hiyo, pengine litakalokosekana kwa hivi sasa ni muda, kwa sababu ya muda tulionao hatutoweza kuandaa ile *shadow of amendement* na kuweza ku-*print* kwa idadi inayotosha kwa Waheshimiwa Wajumbe wote na kuweza pengine jioni kuweza kuigawa kabla ya kikao.

Mhe. Spika, kwa sababu tumo ndani ya utaratibu ambao ni *practice* ya Baraza kwa kipindi chote hiki, basi mimi nadhani mswada huu tunaweza kuujadili na kuupitisha bila ya kuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nia na madhumuni ya maelezo yote haya ni kwamba tufanye kitu kwa uhakika na hiyo ndio nia kubwa, yaani tufanye jambo zuri ambalo litakuwa tumeisaidia serikali pamoja na jamii yetu kutokana na umuhimu wa Mswada huu wa Marekebisho wa Sheria mbali mbali.

Sasa labda pengine Mhe. Mwanasheria Mkuu ambaye ndiye aliyetoa hoja hii alichoacha kusema ni kwamba anawaomba Waheshimiwa Wajumbe pale alipokuwa akiwasilisha kuwa waelewe mswada huu unasomwa pamoja na marekebisho, ambayo hatimaye Mhe. Mwenyekiti ameyatoa. Jambo ambalo hivi sasa ametuhakikishia kuwa wao kwa upande wao Mhe. Mwanasheria Mkuu na bila ya shaka alishirikiana na Mawaziri wanaohusika na sheria hizo mbili, basi marekebisho yale yaliyofanywa na kamati yamekubalika na serikali.

Kwa hivyo, inapotokezea kwa mfano, tunazo *practice* hizo marekebisho yale bado hayanauhakika wa kukubalika na serikali, basi huwa tunaagiza serikali ikakae, ili hatimaye ieleze kile ambacho wanakubaliana kama wanakwenda sambamba na yale marekebisho ya kamati au laa. Lakini kwa hapa marekebisho yale yamekubalika kwa asilimia mia moja kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Waheshimiwa Wajumbe, mimi nimesimama tokea pale awali kwa madhumuni ya lile ombi ambalo alitangulia kulitoa Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa kweli marekebisho ni mengi na wala sina sababu ya kukataa hivyo. Kwa kweli ingehusu marekebisho haya yaje mapema, ili Waheshimiwa Wajumbe wapate nafasi ya kuyaangalia na kuyaoanisha pamoja na ule mswada ulivyokuja na yale marekebisho yaliyopendekezwa.

Sasa muda wetu kama tunavyoelewa si mkubwa wa kutosha mpaka kufikia kuahirisha shughuli zetu hizi. Kwa hivyo, naomba tukubalianae na tukatumie muda huu mchache kidogo, ili tukajisomee na jioni tuendelee na mjadala wa mswada huu ambao tayari umeshawasilishwa. Kwa kweli jambo hilo tumeliona mapema pale ambapo Mhe. Salmin Awadh Salmin alipotoa hoja, basi ni vyema tukubaliane kwamba tusitishe shughuli zetu hadi hapo jioni.

(Saa 5:00 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti jioni hii kunipa fursa ya kuchangia machache katika mswada wetu ulioko mezani hapa, kwanza nataka nipitie ujumla jumla baadae nitaingia ndani kidogo kuangalia kifungu baada ya kifungu.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyama hivi sasa katika nchi yetu tukawa tuna sheria ambazo zitatuepusha na mengi sana na zitatuepusha na majanga ya kupotelewa na vijana wetu pamoja na kuingiliwa na mambo ya nnje ambayo sisi kwa ujumla hatujayazoea, lakini katika hayo mara nyingi sheria zetu tunapozipitisha zinakuwa zina walakini fulani na ufuatiliaji wake unakuwa mdogo sana.

Katika jaduweli hii ya utendaji una orodha kubwa ya watu, hapa kuna kamati, baadae kuna tume na tume hizi zote zina watu wengi sana mimi kwa mazazo yangu shughuli kama hii ilihitaji watu wachache sana kwa sababu mambo mengine ni ya siri kabisa hakutakiwa kila mtu kuyajua, lakini kuyapanua kwa kila kona inabidi habari zinaenea na yale ambayo tunakusudia kuyafanya yanakuwa hayatendeki. Kwa hivyo mimi ningeona haya mambo ya kuwa na matume halafu kukawa nakamati ni mzigo tu lakini utendaji utakuwa haupo.

Mhe. Mwenyekiti nasogea mbele kidogo naangalia kifungu kidogo mimi kidogo nilikuwa na wasi wasi na kifungu kinachosema kwamba, iwapo mtu atakuwa ametenda kosa basi mtu yule mali yake itafilisiwa, kufungwa moja kwa moja au kwa muda wa miaka mitano jengo analolitumia kuendesha biashara zake, hapa kidogo nina wasi wasi kwa sababu nchi yetu hivi sasa tuna utamaduni wa kukodishana majumbe, sasa wasi wasi wangu ni kwamba atakuja kuingizwa mtu katika hatia ambae hakutenda kosa.
Inawezekana tu kwamba mwenye kutenda kosa nyumba ile sio yake yeye amekodi, lakini sheria hii inaelekeza kwamba kama mtu anaitumia nyumba ile akagundulika kwamba atakuwa ametenda kosa basi nyumba ile itakuwa kwa miaka mitano au kuendelea haipati kutumika tena, na yule aliyetenda kosa nyumba sio yake yeye amekodi na yule aliyekodi atakuwa anatafuta chochote kwa kumsaidia yeye katika maisha yake, sasa yeye atakuwa ametiwa hatiyani kwa kosa ambalo hakulifanya. Kwa hivyo naomba hii iangaliwe ili tusije tukafanya makosa makubwa zaidi ya hayo ambayo tunataka yasitendeke tuyalinde.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba sheria hii katika kifungu cha 15 (c) imeelezwa kwamba mtu ambae atatumia au atakutwa anatumia aina yoyote ile

ya dawa hizi basi adhabu yake ni miaka mitano au faini kama ilivyoelezwa, lakini vile vile kifungu 16 (c) sijui ni tofauti ya maneno au vipi, kukutwa akiwa anatumia vile vile limetumika nene anatumia. Lakini adhabu yake ni miezi sita sasa nahisi hapa pana *contradiction* kidogo, ningeomba wanaohusika na mswada huu wakakiangalia kipengele hiki kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti mimi naona kwa hayo machache niseme kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti na mimi nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi kidogo ya kuweza kuchangia katika marekebisho ya sheria ya kuzuia madawa ya kulevya Nam. 9 ya 2009.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mmoja kati ya wajumbe ambao tulifanya kazi kubwa sana katika mswada huu wa sheria ambao takriban ni mswada mzima, kama ulipoona mabadiliko au mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Katiba na Sheria ilivyotolewa leo asubuhi na marekebisho yake ni makubwa sana, tena ni mengi mimi sitotaka kuchangia sana kwa sababu tumepitia takriban mswada mzima na uwezo wetu wa kuona tumeona kama hayo tuliyoyaona na kama tulivyoyapendekeza. Lakini niseme tu kwamba pamoja na kwamba marekebisho ni mengi lakini bado kuna baadhi ya vifungu vyengine vitahitaji kufafanuliwa zaidi au kuelezwa zaidi na wenzetu ambao watapata nafasi sasa hivi ya kuweza kuchangia.

Kwa hivyo marekebisho haya ya mara hii ni muhimu sana kwetu sisi wenyewe na kwa wananchi wetu tulionao, angalau waweze kufahamu au kupata taarifa ya uelewa na kuweza kujua fadia kubwa ambayo itaweza kupatikana kutokana na mswada huu, ambao unahusiana na suala zima la madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la madawa ya kulevya nathubutu kusema kwamba hili ni janga la kitaifa na janga hili ni kubwa sana, sisi kama ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunahitaji kuisaidia serikali ili angalau kuweza kupunguza maafa ambayo vijana wetu yanawapata, kwa kuwa naamini kwamba katika kila jimbo hawawezi kukosekana vijana ambao wanaendeleza shughuli hizi za madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya yapo katika nchi yetu yanaingizwa kwa wingi na mengine yanatoka, madawa haya yanaathiri nguvu kazi yaani vijana wetu ndio wanaoshiriki kikamilifu katika masuala haya, kwa hivyo sisi kama ni viongozi tuliopo hapa ambao ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutakuwa na mchango mkubwa sana wa kuweza kuisaidia serikali katika suala zima la madawa ya kulevya ambao vijana hawa ni watoto wetu wenyewe.

Kama sio mtoto wangu basi atakuwa ni mtoto wa jirani yangu, kwa hivyo sisi kwa upande wetu sio lazima kuiachia serikali peke yake lakini na sisi tuna wajibu katika majimbo yetu kuweza kuangalia na sisi kupunguza kwa asilimia fulani.

Mhe. Mwenyekiti, taifa letu linahitaji vijana na vijana wenyewe ni hawa wengi wao wanashiriki kikamilifu katika masuala haya ya madawa ya kulevya, vijana kama hawa wakishiriki siku hadi siku na idadi kwa mujibu wa takwimu hivi sasa idadi inaendelea kuwa kubwa. Kwa hivyo vijana kama hawa wakishiriki kikamilifu ina maana tunakosa nguvu kazi na maendeleo katika nchi yetu hii kwa hivyo tuna wajibu wa kuisadia serikali, vijana hawa wanaoathirika ni wengi sana na wanaathirika kimwili vile vile kiakili, miongoni mwa hao vijana ambao wameshiriki kikamilifu katika madawa ya kulevya wangine wanawake na wana watoto pamoja. Sasa uangalie hii hali yenyewe hali ambayo mtu tayari ameshajishirikisha katika masuala ya madawa haya ni namna gani anaweza kufanikisha familia yake nyumbani akiwe na mke na watoto hili ni suala gumu na mzigo mkubwa sana wa kitaifa.

Kwa hivyo hawa vijana ambao wameshiriki kikamilifu katika masuala haya wanawajibika vile vile kwa wake zao kuweza kusaidia familia zao, lakini kutokana na hali hiyo wanashindwa kusaidia wake zao na watoto na wanashindwa kusaidia wazazi wao, sasa tuione ile hali kwa sababu wananchi lazima wajue kile tunachozungumza katika suala zima la madawa ya kulevya. Kwa hivyo katika dawa za kulevya hiyo ndio hali halisi.

Tukiangalia upande wa pili katika suala zima la uwezo wa kufanya hivyo kuleta mfanikio ya kifamilia pamoja wazee wao waliowazaa imekuwa ni ngumu sana, wanabaki kuishi katika jumuiya tunazoziita swaba house. Swaba house ni pahala ambapo vijana hao wanajikusanya kwa kuona sasa wamekwisha au wamekwama kimaisha na wanahisi wanahitaji watu wawasaidie angalau kuwaliwaza dili la kufanya na kutaka kutoka katika suala zima la dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti watu hawa wanakusanywa au wanajikusanya mahali pamoja wanaishi hapo kwa taratibu maalum na kwa muda maalum, baadae wanalazimika kuondoka hawawezi kukaa pale kwa muda mredu kwa sababu wana dhamana wameziacha nyuma, kwa hivyo inaonyesha katika kila swaba house kuna *Intec* za vijana kama hawa kila baada ya wiki nne kuna *intec* ambayo inatokezea. Kwa hivyo hawa vijana ni wengi na kila siku idadi inazidi kuendelea, kwa hivyo hawa vijana wanapata mafunzo ili kuweza kubadilisha tabia zao ambazo wanatakiwa waziache za kushiriki katika ulevi huo, baadae kujiingiza katika masuala mazima ya UKIMWI.

Matumizi ya sindano Mhe. Mwenyekiti, baina ya mteja na mteja yanaendelea kama kawaida na matokeo ya ulevi huu kujiendeleza katika masuala ya mashindano kupeyana mmoja baada ya mmoja matokezeo yake ni kuambukizana ugonjwa wa UKIMWI. Kwa hivyo kama hali ni hiyo vijana wanashiriki kikamilifu kuanzia miaka 15 mpaka miaka 35 hii inaonyesha kwamba idadi inazidi kuongezeka na taifa linakuwa na mzigo mkubwa sana.

Kwa hivyo katika hili ningelimuomba Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais ningelimuomba kwamba pamoja na tume ya ukimwi waweze kuwapitia hawa vijana, kwa ajili ya kuwapa maelezo, nasaha, ushauri lakini pamoja na nasaha na ushauri ambao wataweza kuutoa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na wengine, lakini hayo hayatoshi wanahitaji vijana hawa kuweza kupewa msaada wa kifedha jambo ambalo ni muhimu kwa sababu ya maisha yao, pale anapokaa wanaishi kwa matumizi na matumizi ni fedha na pale fedha haiwezi kupatikana kwa sababu hawana kazi.

Kwa hivyo pamoja na taaluma wanayoipata na ushauri watakaoupata na nasaha watakazozipata lakini bado tatizo la kimaisha litabakia pale pale, kwa hivyo ningelishauri Mhe. Makamo wa Kwanza Rais akasaidia hizi *Sober house* zilizopo Unguja na Pemba, kwa sababu muda wao ukimalizika hawa wanahitaji kuondoka wakatafute maisha. Kwa hivyo ningelipendekeza kwamba baada ya kupitiwa kuna watu wana uwezo na elimu nzuri na wana fani mbali mbali watu wa aina hii, wakaweza kupatiwa ajira. Nafikiri suala la ajira litaweza kuwakomboa katika mambo yote, hili ni jambo muhimu sana linahitaji kuzingatiwa.

Sasa kuna WAMATA Chake Chake kule Pemba ambayo hii WAMATA inashughulikia zaidi watoto wenye mazingira magumu, lakini vile vile wanajaribu kutoa huduma kwa hizi *Sober house*, lakini jumuiya hizi pamoja na kusaidia misaada ya kiukimwi, lakini na serikali nayo ingezisaidia hizi jumuiya ili kuweza kusaidia pande zote mbili. Kwanza watoto wenye mazingira magumu na vile vile kuwasidia hawa watu ambao wana mahusiano makubwa baina ya *Sober house* na jumuiya hii ya WAMATA, kwa kweli hayo ndio mawazo yangu yaliyobakia.

Lakini pamoja na hayo yote kuna baadhi ya vifungu vyengine ambavyo viliwahi kupitiwa leo asubuhi na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Katiba na Sheria, lakini tunahitaji baadhi ya hivi vifungu vyengine vilivyokuwa vimeandikwa ambavyo kidoto vinahitaji kuwekwa vizuri.

Kwa mfano kifungu cha 18 kama kilivyoandikwa pale kifungu cha 18(a) lakini kifungu hicho kimeondoshwa kabisa kifungu hicho cha 18 na

kinazungumza kifungu hicho kwamba kusimamia utelelezaji wa sheria ya taasisi zinazosimamia na sheria.

Halafu vile vile kuna sehemu nyengine ya kifungu cha 36 namna ya kuwatambua vizuri wateja, ambapo kulikuwa na maelezo kuingiza aya mpya kama ivufatavyo namna na taratibu za kuhudumia wateja, kwa hivyo pale tumeifuta ile na tunaandika tu namna ya kuwatambua vizuri wateja.

Katika kifungu cha 29 kuna neno pale limefutwa kifungu cha 2 mstari wa pili kuficha bila ya kujali masharti ya sheria inavyohusika na kuficha siri na uaminifu hapa tunaliondosha neno kuficha na badala yake tunaweka kutunza siri na uaminifu.

Katika kifungu cha 6b(3) masharti ya kijifungu cha pili cha kijifungu hiki, kifungu hicho kilikuwa na matatizo mengi na tukaona tukiandike vyengine kwa hivyo tukaweka masharti ya kijifungu cha 6a pale pana 6a na 6b. Kijifungu cha 6a kifungu cha kwanza na cha pili vya kijifungu hiki kwa namna yanavyohusiana na kutumika Zanzibar, hayatotumika moja kwa moja pale yatakaporekebishwa na Bunge mpaka masharti kama yatakavyofanywa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, hayo ni mambo ambayo yameweza kubadilishwa vile vile.

Katika kifungu cha 21 kijifungu cha 3 Kamati ya kitaifa maana yake ni kamati ya Kitaifa ya Pamoja katika kudhibiti usafishaji wa fedha haramu iliyoanzishwa.

Katika kifungu cha 4(2) ambacho kina a, b, c, d, e, f, g, h, I, kuanzia f mpaka I pana maneno pale yameunganishwa pahala pamoja mwenye dhamana, yale yanahitaji kuwekwa mbali mbali mwenye mbali na dhamana mbali. Lakini vile vile kuna maelezo Waziri mwenye dhamana na mambo ya afya ile na mambo yanahitaji kuondoka yanafutwa kabisa, na isomeke moja kwa moja waziri mwenye dhamana ya afya na ustawi wa jamii, isomeke moja kwa moja waziri mwenye dhamana ya ustawi wa jamii na vijana.

Mhe. Waziri mwenye dhamana wa Miundombinu isomeke Waziri mwenye dhamana ya bandari na viwanja vya ndege.

Mhe. Mwenye dhamana ya Habari, Utamaduni Utalii na Michezo, iwe waziri mwenye dhamana ya utalii na michezo, hayo ndio baadhi ya mambo ambayo madogo madogo yaliyokuwa yalihitaji kubadilishwa badilishwa.

Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema nawapa nafasi wenzetu ambao wataupitia kwa mara ya pili ili kuweza kutoa michango yao katika suala zima hili la madawa ya kulevya, ambayo yanaathiri vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru kwa mchango wako naunga mkono hoja. *(Makofi).*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze jinsi ulivyopendeza na joho lako jipya, pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia au kutujaalia sote neema yake ya uhai na afya tukaweza kujadili mambo yanayogusa maslahi ya nchi yetu na watu wake, leo hii au laasiri hii tukiwa tunazungumzia Mswada huu wa kurekebisha sheria mbali mbali ambapo hasa kumeguswa sheria tatu.

Sheria ya kupambana na madawa ya kulevya, Sheria ya kupambana na fedha haramu pamoja na sheria ya mwenendo wa kesi za jinai. Mhe. Mwenyekiti na mimi kama wenzangu nitangulie kusema kwamba nilipata nafasi ya kutosha nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala kutoa maoni yetu wakati mswada huu ulipoletwa mbele ya kamati. Kwanza nomba nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mawaziri wahusika wawili, Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia masuala ya Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa jinsi walivyotoa mashirikiano na kukubaliana na mapendekezo takriban yote ambayo yametolewa na kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti baada ya pongezi za shukurani hizo niseme kwa jumla sitokuwa na mapendekezo ya ziada kuhusiana na mswada huu, kwa sababu kama nilivyosema takriban yote tumeshayatoa katika kamati, lakini nishukuru kwa semina ambayo tumeipata juzi nashukuru na naipongeza sana Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa semina ile ambayo wametupatia. Kwamba ilitusaidia kuongeza uelewa wetu kuhusu mambo mengi na kama nilivyosema katika semina ile nadhani hata kamati yetu ingefaidika zaidi kama semina ile ingelikuja kabla mswada haujaletwa katika kamati, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo ambayo tungeweza kuyachangia kwa vizuri zaidi. Lakini nashukuru tulitoa maoni yetu pale na kwa kiasi kikubwa naamini kwamba yatakuwa yamesaidia.

Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema mimi katika mswada kwa jumla sina kubwa nina mambo mawili tu, ambayo moja nataka kupongeza na moja nataka kidogo kurejea indhari ambayo niliitoa katika kamati lakini nafikiri imepata nguvu zaidi baada ya semina ambayo Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais wenyewe kutupa ile semina ya juzi. Nataka kupongeza Mhe. Mwenyekiti kwanza nipo katika sehemu ya tatu ya mswada huu ambayo

inazungumzia marekebisho ya Sheria ya usafishaji wa fedha haramu na mapato halisi Nam. 10 ya mwaka 2009.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 22 cha Mswada huu, ambacho kinapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 6(a) na (b), katika kile kifungu cha 6(b) kifungu kidogo cha (3) hapa nataka nimpongeze sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuona umuhimu wa kudhibiti na kutunza mamlaka ya Zanzibar. Kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, tulikirekebisha kidogo uwandishi katika Kamati na katika ukurasa wa 8 wa taarifa ya kamati au marekebisho ya kamati kitaonekana tulivyokiandika upya na naomba nikisome. Kinasema hivi:-

> "Masharti ya kifungu cha 6(a) na vijifungu vya (1) na (2) vya kifungu hiki kwa namna vinavyohusiana na kutumika Zanzibar, hayatomika moja kwa moja pale itakaporekebishwa na Bunge mpaka marekebisho kama haya yatakavyofanywa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar"

Mhe. Mwenyekiti, nataka kumpongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba ya kuliona ili na kulianzisha kupitia Mswada huu. Kuweka utaratibu wa kulinda mamlaka ya Zanzibar. Kumekuwa na utaratibu nafikiri rafiki yangu Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ni shahidi sana wa haya. Mara nyingi Bunge limekuwa likitumia vibaya mamlaka yake, kwa kutumia Katiba ya Jamuhuri ya Muungano kwa kutunga sheria hata zisizohusu masuala ya muungano. Baadaye kuandika pale mwaka kwamba sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Haya mambo mara nyingi yanaleta malalamiko mengi sana kwa Wazanzibari.

Sehemu kubwa ya mambo tunayoyaita kero za Muungano huwa mara nyengine yanatokana na vianzo kama hivi. Nitoe mfano mdogo Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana katika muda mfupi nilipotumikia Bungeni ilikuja sheria ambayo ilizua mjadala mkubwa sana, sheria mpya ya madini ya Tanzania. Kama mnavyojua madini sio suala la muungano. Na wao wenyewe upande wa pili ndugu zetu wa damu, siku zote wamehakikisha kwamba ni mafuta na gesi asilia tu ambayo imetajwa katika Katiba kwamba ni mambo ya muungano, lakini madini mengine wameyazuia. Lakini ile sheria ya uchimbaji walishaileta kinyemela pale katika Bunge kwamba imeandika kwamba sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Baadhi ya wajumbe waliotoka Zanzibar waliokuwepo wakati ule na naomba niwatambue hasa nao ni:

1. Mhe. Yahya Kassim Issa — Chwaka
2. Mhe. Mohammed Habibu Mnyaa — Mkanyageni

Wakishirikiana na baadhi yetu ambao hatukuwa wajumbe wa kamati ile latini tulishiriki katika vikao vyake, tulisimama kidete ili kuona kifungu kile kinafutwa. Sasa kume kuwa na huu utaratibu wa kuandika vifungu kama hivi na baadaye kuonekana kwamba kwa sababu hiyo inaipa mamlaka Bunge ya kuingilia hata mambo yasiyokuwa ya muungano kwa upande wa Zanzibar kuyapenyeza. Kwa hivyo nasema nafurahi na nakupongeza sana kwamba katika Mswada huu serikali inaliona hilo na inaanza kuchukua hatua za marekebisho. Ni imani yangu kwamba hatutaishia hapo, tutachukua hatua kila inapobidi kulinda kilichochetu.

Moja katika matatizo makubwa Mhe. Mwenyekiti katika muungano huu tunaile tabia ya kuona ndugu zetu wa damu wanataka chao kiwa chao lakini chetu sisi kiwe chao pamoja na wao. Haya ni mambo ambayo Wazanzibari hatuwezi kuyakubali hata siku moja. Naamini wakati ukifika wakati wa kujadili katiba mpya na unakuja haupo mbali, Wazanzibari tutasimama kidete kurejesha kila kilichohaki yetu katika mamlaka ya Zanzibar. Kwa hivyo nalipongeza hilo Mhe. Mwenyekiti.

Jengine nikiondoka hapo, hili kidogo nimekuja na mawazo tofauti. Kama nilivyosema nilitoa maoni katika kamati na wenzangu, lakini serikali ikatujibu wakati ule na tukaridhika shingo upande. Mhe. Mwanasheria Mkuu atakumbuka, tulikuwa tukijadili kifungu cha 11cha Mswada huu kwenye hii Sehemu ya Pili, ambayo kuwa ilikuwa ikizungumzia Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya. Katika kifungu cha 11 cha mswada huu kinasomeka.

> "Kifungu cha 16 cha sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta kijifungu cha 1 (c) na badala yake kuandikwa upya kama ifuatavyo:
>
> (C) Ikiwa itapatikana akiwa anatumia dawa za kulevya atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miezi sita."

Mhe. Mwenyekiti, kwa wale wajumbe wenzetu ambao asubuhi walitoa hisia zao kwamba ina wapa shida mara nyengine kuchangia miswada kama hii kwa. sababu hakuna *metric* inayoonesha maeneo gani ambayo yamerekebishwa na yale ambayo yalikuwepo awali. Kifungu hichi kinahusu kifungu kilichokuwepo awali ambacho kilikuwa kinalazimisha au kinaweka shauku kwa yule mtumiaji wa madawa ya kulevya. Ikiwa atapatikana na hatia basi atapewa adhabu ya kifungu kwa kipindi cha miezi sita na a/kitoka alikuwa atapelekwa katika kituo cha kurekebisha tabia *(Rehabilitation Center)*. Tulihoji kwa nini kinarekebishwa hivyo. Bila shaka serikali ilikuwa ina majibu ya kutwambia kwamba kwa hali ilivyo hivi sasa hakuna vituo vya kurekebisha tabia Zanzibar. Kwa hivyo kuweka kifungu kama hiki cha sheria

kunatoa uzito na kuinaifanya serikali kama vile haitekelezi kisawa sawa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sirudi hapa nikasema kwamba tukirejeshe kwa sababu naikubali hoja hii ya serikali lakini nataka kutoa maoni tu kujumla. Pamoja na kwamba tumekirejebisha, lakini serikali isitumie nafasi hii kujivua jukuu la kuanzisha hivi vituo vya kurekebisha tabia *(Rehabilitation Center)*. Hilo sio jambo ambalo tunaweza tukalikwepa, kama tumeamua kujikubalisha kuingia katika mfumo wa kilimwengu, mfumo wa kidunia wa kupambana na utumiaji wa dawa za kulevya, basi katika kurekebisha wale wanaotumia, suala hili la kuwapeleka katika vituo ni moja katika mambo ambayo yamewekwa kama ni mambo ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, Mkutano maalum wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliokutana tarehe 8-10 Juni, 1998 wanasema:

> *"Special session of the general assemble devoted to countering the world drug problem to together".*

Katika maazimio yake para ya 14 inasomeka,

> *"In order to promote the social integration of drug abusing offenders where appropriate and consistent with the national laws and policies of member states. Government should consider providing either alternative to conviction punishment or in addition to punishment that abuses of drugs, should undergo treatment, education, aftercare, rehabilitation and social reintegration.*" Nina *underline* maneno yaliyosemwa hapa kwamba. *We are appropriate and consistent with the national laws and policies of member states.*

Bila shaka imetoa nafasi kwa serikali za nchi wanachama kupima uwezo wake. Lakini ninachosema na serikali pengine iliingiza kifungu hichi kwa nia njema. lakini sasa imekiondoa kwa sababu haina uwezo. Lakini nasema isiwe tena baada ya kukiondoa ndio tumejivua jukumu kwa hivyo sasa ndio tunataka kuachia kabisa kutolishughulikia suala hili. Katika hili tuliuliza pale moja nilikuwa nadhani tuliambia ile Ofisi ya Umoja wa Mataifa inashughulikia madawa ya kulevya na uhalifu. Wao nashughulikia zaidi kujenga uwezo. Kwa hivyo hawawezi kutusaidia katika hili.

Nilisema niliwahi kumuona dada angu Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais katika gazeti la Zanzibar Leo ukurasa wa mbele, akizungumza na Balozi wa Marekani hapa nchini. Ambaye alionesha nia ya kusaidia Serikali ya Zanzibar kupambana na utumiaji haramu wa dawa za

kulevya. Nilikuwa nasema hebu tuwaombe hawa wenzetu tuone tunaweza kusaidia kiasi gani suala hili.

Hili nalisema Mhe. Mwenyekiti kwa sababu tutakuja kuona na pemezungumzwa sana hapa *sober houses.* Sisi katika Kamati tulipendekeza, lakini serikali walipendekeza kwamba wanaogopa kujitwisha mzigo ambao kuwa watakuja kuwa hawauwezi. Wakati serikali haina hivi sasa *rehabilitation center* basi angalau ingelijikubalisha kuwapeleka wanaokamatwa wakahukumiwa, wakitoka wakapelekwa katika *sober houses*. Lakini wakasema pale pana malipo. Na mimi nakubali pana malipo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi na wewe ni shahidi kwa sababu tumeshapeleka baadhi ya wananchi wa majimbo yetu na inabidi umlipie kwa kile kipindi anachotakiwa kukaa pale miezi mine kila mwezi shilingi laki moja. Kwa hivyo kwa mtu mmoja unatakiwa upeleke laki nne, sasa wamesema hilo ni jukumu zito. Sasa nasema ni sawa lakini tujitahidi kuona kwamba tunatengeneza hizi *rehabilitation center*.

Mhe. Mwenyekiti, haya yalikuwa yanahusu katika upande wa Mswada. Lakini ya jumla yanayohusu malengo na madhumuni ya Miswada hii na mambo mengine ambayo nadhani tuyaseme ili serikali iyazingatie pengine yatakuja kufanyiwa marekebisho huko siku za mbele au mambo mengine yanayohusiana na hayo katika kuzidi kuimarisha hii hali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisisitize suala moja, moja katika maeneo ambayo yanaonekana yanatumika sana uingiaji wa madawa ya kulevya ni maeneo ya hivi visiwa vidogo vidogo ambavyo havina ulinzi wa kutosha. Nchi yetu ni visiwa vidogo vidogo na vina maeneo mengi lakini zina hizi zinazoitwa Bandari bubu. Nasema tuna haja ya kuona. Wananchi wanazungumza mengi huko nje kwa hivyo kuna maeneo kama kisiwa cha Mnemba, Mantarif Pemba, Fundo, Tumbatu. Hizi bandari bubu nyingi zilizokuwepo Pemba na Unguja tuone kiasi gani zinalindwa kwa kuwa na vituo vya polisi na Uhamiaji, ili kuona kama kuna upenyo ambao unatumika na waingizaji wa dawa hizi ili upenyo huo uweze kuzibwa.

Mhe. Mwenyekiti, la pili katika la jumla naomba serikali itupie sana jicho katika vituo vikuu vya uingiaji watu, Bandarini na Uwanja wa Ndege lakini hasa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali itumie macho matumizi. Nimepiga kelele mara nyingi sana juu ya chumba cha wageni mashuhuri (VIP). Mara nyingi tumesema Zanzibar pamekuwa hapana utaratibu, unakuta watu unajiuliza hawa wanatumia VIP kwa msingi upi. Unamkuta sio yeye tu, yeye anatumia VIP, ana rafiki zake,

ana jamaa zake, jamaa wa rafiki zake na jamaa na wao pia wanatumia VIP. Utaratibu huu Mhe. Mwenyekiti, huuoni popote isipokuwa Zanzibar.

Mara moja niliuliza suala hapa, nikajibiwa na Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu kwamba suala hili linakuwa gumu kwa sababu kuna Idara tofauti zinazohusika na suala hilo. Nasema kwamba hizi idara zote ni za serikali, kwa hivyo serikali iyone vipi inaweza kufanya uratibu ili kudhibiti matumizi mabaya ya VIP. Kwa sababu hatujui Mhe. Mwenyekiti, inawezekana kabisa katika hawa hawa ikawa kuna watu wanatumia vibaya VIP kwa sababu tumezoea, kwamba katika VIP hata utaratibu wa kusachiwa ambao ni wa lazima kwa kila mtu, hata sisi tunaojiita waheshimiwa haufuatwi upasavyo. Sasa kama haufuatwi upasavyo inawezekana kabisa watu wakaitumia vibaya nafasi ile wakapitisha madawa ya kulevya katika VIP. Matumizi yake yanapaswa kuchungwa sana sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo nizungumzie suala la *sober houses*. *Sober houses* ni taasisi zinazojitegemea. Wameziunda vijana wenyewe. Tuna shukuru baadhi yetu tumeshiriki kikamilifu kuwapa moyo. Ilianza moja leo zimeshafika 12 katika nchi na zinasaidia sana. Lakini uwezo wao ni mdogo. Katika hili niiyombe Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, tulipopitisha bajeti nakumbuka Mhe. Waziri wa Nchi, alitwambia tulipokuwa tukitaka maelezo kwamba kumetengwa milioni 47 kwa ajili ya kusaidia sober houses katika mwaka huu wa fedha. Lakini baadaye *sober houses* wanatwambia wameambiwa watapewa milioni 10. Sasa tunataka kujua sisi Baraza tuliopitisha matumizi, zilikuwaje 47 zikashuka zikawa 10.

Lakini pia tumekikuta kitu ambacho hakiridhiki. Hivi karibuni kamati yetu ilizitembelea *sober houses* zilizokuwepo Pemba. Vijana wa *sober houses* ya Wete walikuwa wanalalamika kwamba wamepewa ahadi nyingi na Makamo wa Kwanza Rais katika mkutano wake wa pamoja lakini hawajatimiziwa hata moja. Ili ya Chakechake wametimiziwa baadhi na wametwambia wametuonesha mpaka picha za kuthibitisha. Lakini ile ya Wete wanasema hawajatimiziwa hata moja katika waliyoahidiwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika jambo kama hili tunampaka matope Makamo wa Kwanza wa Rais bila ya sababu. Nadhani hata kama alikuwa ameahidi basi jukumu la watendaji sasa kusimamia na kuona ahadi alizotoa zinatekelezwa kwa vijana wale.

Lakini tusiishie hapo tu, sasa hivi *sober houses* wamekuwa wabunifu. Tunapiga kelele mara nyingi kwamba hawa wanaomaliza kupata nafuu pale wanahitaji shughuli za kujishughulisha kimaisha ili wasije wakarudia katika tabia zile. Sasa wenyewe wameomba mara nyingi kusaidiwa kupata nafasi za kazi lakini hawazipati. Hivi sasa wao wenyewe wameamua kuanzisha

utaratibu wa kuwapa mafunzo ya kufanya kazi za mikono, ili na wao baadaye waweze kujiajiri.

Sasa nataka kuona Ofisi ya Makamo wa Kwanza ije itwambie imejipanga vipi kuwasaidia hawa vijana kwa vifaa, ili waweze kuimarisha huduma zao kama hizi, ili kuweza kuongeza ufanisi wa yale mafunzo ambayo wanayatoa pale ambayo yanawasaidia sana wananchi. Mafunzo yale yanafanya kazi ambayo serikali ilipaswa ifanye baada ya wenyewe kuwa haina uwezo wa kujenga *rehabilitation center*.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala dogo lakini kubwa ambalo tumelipa juzi katika Semina, katika hili namuomba sana Waziri wa Katiba na Sheria anisaidie. Katika takwimu ambayo tulipewa na Jeshi la Polisi pale, zilikuwa zinatisha katika kuona wingi wa kesi ambazo zinapelekwa Mahakamani. Lakini ni idadi ndogo sana ya kesi ambazo kuwa zimepata hatia. Unakuta katika kesi zaidi ya 100 kesi iliyopata hatia ni moja. Ni hali unaikuta katika mwaka 2009, 2010 mpaka 2011 tunavyozungumza, takwimu hazipishani sana.

Tulipouliza pale na Mhe. Mwenyekiti ulikuwa shahidi polisi walijivua wakasema wao kazi yao ni kukamata na kufikisha Mahakamani. Kazi iliyobakia baada ya pale ni ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama. Wakatwambia hili si lao wao, sisi tuwaulize Mahakama. Hapa tunae Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria tulikuwa tunamuomba atusaidie hapa, tatizo liko wapi? Je, polisi wanapopeleka kesi hizi upelelezi wake huwa ni dhaifu kiasi ambacho panashindwa kupatikana kutiwa mtu hatiani au kunapita nini hapa kati kati mpaka kukawa hakuna hukumu mpaka polisi wenyewe wakafikutwambia kwamba wanavunjia moyo kwa sababu ya kuendelea mambo kama haya kwa sababu ya kiwango kidogo cha kutiwa hatiani na ucheleweshwaji wa kesi hizi kwa ujumla wake.

Wametupa mfano kwamba kesi za wale watumiaji ambao wamefanyiwa uchunguzi kwa kwenda kupimwa haja ndogo zao, hapo ushahidi ni baina ya Mkemia Mkuu, Mahakama na Polisi. Sasa kwa nini tena bado unakuta kesi kama ile hata za watu kama wale inashindwa kupatikana hatia. Kuna kitu gani hapo? Mhe. Mwenyekiti, katika hili huko nje kuna maneno mengi yanasemwa na nadhani ni wajibu wa serikali kupitia chombo hichi kuwatoa hofu wananchi, kwamba usikilizaji wa kesi hizi juu ya kuhukumu kweli zinakwenda kwa mujibu wa sheria na hapana mchezo mchafu unaopelekea watu hawa kuweza kufanya wanavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, karibuni kabisa katika jimbo la Mjimkongwe katika maeneo ya Shangani Minaramiwili na moja Vuga karibu na Msikiti maarufu

unaitwa Msikiti wa Bwana Udi, palikuwa kuna watu walikamatwa, lakini siku ya pili wanaonekana wapo mitaani. Sasa ukiwauliza polisi wanakwambia sisi kazi yetu tumemaliza, kama wameachiwa, kama wamepewa zamana kama kuna lolote hilo waulizeni Mahakama. Kwa hivyo tunataka atwambie Mhe. Waziri kwa bahati nzuri na yeye alishiriki katika ile semina anayo karatasi kama tuliyopewa sisi yenye takwimu zile. Atueleze katika Mahakama kunapita nini au katika Afisi ya DPP kuna pita nini hata kesi hizi zinashindwa kupata hukumu zinazostahiki na kupelekea kuingia katika biashara hii na ikaonekana kama biashara hii ni jambo la kawaida ambalo haliwezi kudhibitiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika maoni ya jumla nimalizie. Nimesema moja katika tulichojifunza katika semina iliyoandaliwa na Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na naendelea kuwashukuru tena na tena kwa mafunzo yale. Tuliambiwa moja katika suala la msingi ni kuangalia *profiling* kwa maana ya wanaojihusisha na vitendo vile na *factor* nyengine katika nchi. Moja kubwa ambalo tumeambiwa ni suala zima la umasikini, niseme kuchanganyikiwa, mnong'onyoko wa maadili.

Sasa katika hili niseme imefika pahali serikali si katika hili la madawa ya kulevya tu lakini kwa ujumla wake. Kuna masuala mengi sasa hivi katika nchi yetu kuna vitendo viovu vinakuwa kutokana na mnong'onyoko wa maadili. Pengine kwa sababu ya changamoto ambazo tunazo katika dunia hivi sasa, kwa sababu ya tunaouita utandawazi, sijui utandawizi. Imepelekea kushindwa kudhibiti maadili yetu. Mara nyengine inakuwa ni vigumu sana. Sasa katika hali kama hiyo lazima kuwe na nguvu ambayo inapambana na huu unaoitwa utandawazi. Huwezi kuzuia katika dunia ya leo vijana. wasitizame ma – TV na *satellite* yanayokuja haua ma- *internet* ambayo yanapotosha sana, lakini angalau nguvu ile ya maovu ingekuwa inadhibitiwa kwa nguvu nyengine ambayo ni ya kuwafundisha mema, basi angalau kidogo ile kasi ingekuwa inapungua.

Nilikuwa nataka kupendekeza kwamba serikali iyone haja katika mitaala ya masomo maskulini kuanzisha somo maalum la maadili ambayo itajumuisha sio masuala haya tu lakini kwa ujumla wake masuala mengi ambayo yanapelekea mmong'onyoko wa tabia na maadili katika nchi yetu ambayo yanapelekea vijana wetu kujiingiza katika mambo mengi kama haya tunayoyazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, upande wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu nina moja tu. Nalo ni kwamba ukitizama sheria hizi mbili zina mahusiano makubwa sana ndio maana zimeletwa kurekebishwa kwa pamoja. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ametwambia alipokuwa akiwasilisha

Mswada. Na hata ukiusoma Mswada wenyewe kwenye madhumuni na sababu yanajieleza hivyo, kwamba mabo haya yanahusiana. Kwa sababu mara nyingi hizi fedha haramu huwa zinatokana na mapato yanayotokana na dawa za kulevya.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba katika nchi yetu kumekuwa kuna vitendo vinaonekana hapa ambavyo ni vya usafirishaji wa fedha za kigeni kwa wingi kwa njia sio za kibenki. Hili lilizungumzwa hata katika mkutano uliokuwa umefanyika juzi wa Baraza la Biashara Zanzibar ambapo kuna mfanyabiashara mmoja limwambia Mhe. Rais na hapa Mhe. Rais alionekana kushtushwa na suala hili lakini akasema atafatilizia. Suala hili linazungumzwa lakini lipo. Unajiuliza kama fedha hizi ni biashara halali, maana yake tuna sababu ya kuzitilia mashaka, pengine ni ya biashara halali lakini unajiuliza kwa nini kama biashara halali zisipite katika mfumo wa kawaida wa kibenki. Kwa nini ziwe zinasafirishwa kwa malundo kila wiki watu kusafiri nje, Zanzibar kuziondoa. Tulipoliuliza juzi kwa vyombo vya dola walitwambia wao hawawezi kuchukua hatua yoyote kwa sababu hakuna sheria Zanzibar inayokataza kusafirisha fedha kwa mfumo ule.

Mimi nilikuwa nadhani kuwa sasa tunapitisha marekebisho haya, nilisema pengine Kamati na Baraza kwa jumla tungepata ile Semina kabla tungepata kuchangia vizuri zaidi. Lakini nasema hatujachelewa bado kuna uwezekano wa kuleta marekebisho mengine ili kuona mambo kama ambayo yanaongeza wasi wasi kwamba fedha kama zile zinatokana na biashara kama ile, sina hakika lakini inawezekana kutokana na mazingira yake basi tukaweza kuzidhibiti ili kuona kwamba nchi yetu haiteuzwi kuwa kituo cha usafirishaji na upitishaji wa madawa ya kulevya lakini pia ikawa ni usafirishaji wa fedha haramu zinazotokana na biashara hii au mambo mengine ambayo hayakubaliki katika ulimwengu huu wa leo.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar imeingia katika enzi mpya. Serikali ya Umoja wa Kitaifa na maridhiyano yaliyofikiwa mwaka juzi, yametupa nafasi nzuri sana ya nchi sasa kujiendeleza kiuchumi na katika maendeleo ya jamii. Kwa taarifa yako Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza hili sasa hivi Zanzibar inatizamwa vizuri sana. Kuna kitabu kimoja kimetoka mwaka huu Marekani kimeandikwa na muandishi mmoja anaitwa Robert Kaplan kinaitwa *"Monsoon: The Future of American Power and Indian Ocean".* Kitabu hiki kinazungumzia huu muelekeo unaonekana hivi sasa wa Mataifa ya Magharibi nguvu yake kupungua na kupanda kwa mataifa ya Mashariki hasa ya Asia. Lakini katika kitabu hichi nchi pekee ambayo imetajwa katika Bahari ya Hindi kwamba nayo ina muelekeo wa kunyanyuka na kurejea nafasi yake iliyokuwa ya zamani ya kuwa kituo kikuu cha biashara na uchumi na harakati katika Bahari ya Hindi basi ni Zanzibar.

Kitabu kimechapwa Marekani Mhe. Mwenyekiti, kimeitaja Zanzibar kama inauwezekano wa kurejea kule walikosema Waingereza wa miaka ya nyuma kwamba *(When one pipes in Zanzibar they dance in the lakes)* kwamba tarumbeta likipulizwa Zanzibar wanadimkwa na kuhemkwa waliokuwepo katika maziwa makuu. Pengine ndio nafasi ya kufanya safari hii wakademkwa na kuhemkwa mpaka waliokuwepo Bara Hindi na Arabuni huko. Lakini nasema nafasi hii iliyotabiriwa Zanzibar itakuwa ngumu kufikiwa na pengine itakuwa tunaitia dosari ikiwa tutashindwa kudhibiti vitendo hivi, ili kufanya Zanzibar na kuonekana kwamba kituo kikubwa cha biashara. Matokeo yake sehemu tunayoitegemea ikajakuwa kituo kikubwa cha biashara cha madawa ya kulevya na kituo kikubwa cha kusafirishia fedha haramu.

Kwa hivyo hii tuiyone kama ni changamoto kwetu, bubadilike utendaji wetu, tuifikie hapo inapotegemewa na Waziri kwamba itaweza kufika. Lakini pia tuimarishe upambanaji wa dawa za kulevya na pia upambanaji wa fedha haramu. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naipongeza serikali na kuitakia kila la kheria katika utekelezaji wa sheria hii. Ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na taufiqi ya kuzungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kwenda kwenye Mswada wenyewe mimi napenda nasisitize umuhimu way ale marekebisho ambayo yanafanywa na Kamati kuingizwa ndani ya Mswada kabla ya kuletwa katika siku ya Mjadala. Hapa naziomba Kamati zote za Baraza hili tusaidiane.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi katika Baraza lililopita na Mswada huu wa kusafisha fedha haramu ulikuwa ni moja katika Miswada mikubwa sana iliyowahi kufika katika hili Baraza. Kwa kuona hivyo sisi tulitoa shindikizo kwa Wizara ya Fedha kwa wakati ule kuchapisha marekebisho kama alivyotaja Mhe. Salmin leo asubuhi katika mchango wake wa taarifa. Kuweka jaduweli inayoonesha kile kilichofutwa na kile kilichoingizwa. Lakini hii inafanyika baada ya kukubaliana na majadiliano na Kamati yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa tunawaomba wenye viti wa Kamati zetu za Baraza tuwasaidie wajumbe wengine. Ikiwa Mswada una marekebisho makubwa basi tuiyombe ile wizara ifanye hivyo na sisi hapa tukifika tutasaidiana kuona kwamba imefanya hivyo. Ikiwa haikufanya hivyo bora waurejeshe. Haya mambo ya kuombana ombana kila siku bora tuujadili, bora tuujadili, tumeshachoka tena. Kwa sababu tutakuja kudanganyana katika

Baraza la kutunga sheria. Kwa hivyo ni afadhali twende kwenye utaratibu mzuri. Nashukuru kwamba tunaelekea kwenye hiyo kusomwa kwa mara ya kwanza na mara ya pili, lakini haimaanishi kwamba kweli tutafikia hapo. Bila ya kuanza hatutoweza kufikia.

Hilo naomba sana niliseme, tunapata tabu sana Mhe. Mwenyekiti, kutizama neno moja moja ambalo ndani ya lile neno limeandikwa maneno 10 kwamba, toa hapa, tia hapa, ingiza hapa, halafu ndio linakuja hilo neno. Tunaomba sana awamu hii iwe ni ya mara ya mwisho tena kwa kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naiyamini Kamati ya Katiba na Sheria. Kuna michango ambayo nitatoa baada tu ya kuamini yote waliyoyafanya na hususan tunamshukuru sana Mwanasheria kutueleza wazi kwamba wamekubaliana na michango yote waliyoitoa Kamati kikamilifu. Wasi wasi wangu mmoja mkubwa Mhe. Mwenyekiti ni utekelezaji. Na utekelezaji hivi ilivyopangwa katika huu Mswada inaonesha kuwa hapatakiwi kutekelezwa. Mhe. Mwenyekiti, angalia kifungu cha 4 cha mswada huu wa mwanzo kwamba tume itakuwa na wajumbe wafuatao.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, tume ikishakutaja waziri basi asiingizwe mtu mwengine hivyo itakuwa haifanyi kazi. Mhe. Mwenyekiti, mimi napendekeza kwamba kuwe na tume ya mawaziri mbali, wenzetu wanaita *Ministerial Committee* wao ndio wanaotunga sera, halafu kuwe na *technical committee* ambayo itashughulikia mambo yale. Mhe. Mwenyekiti, ukiwachanganya hawa watu wa *technical* na watu wa *ministerial* hapafanywi kazi hapa kila siku watakwambia sisi tuna kikao cha Baraza la Mapinduzi, sisi tuna nini hii wale wanataka kukutana hawapati kukutana. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema tuwabague kabisa wale wajumbe wa *technical* tuwabague na wale wajumbe wa *ministerial* pia tuwabague.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna kikao cha pamoja basi kiitwe vyengine, lakini haiwezekani kuchanganya mawaziri tena wapo saba hapa akiwemo mwenyewe Makamo wa Kwanza wa Rais na mawaziri wengine saba. Mhe. Mwenyekiti, hii si Baraza la Mapinduzi karibu ya robo tatu hii, hapa amekosekana Rais na Makamo wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, mimi sikubali kwamba watakutana hawa na mambo yatakwenda vile vile. Ni kwamba tukubali ku-*reduce* namba ya mawaziri wasiozidi watano ndio kweli watakutana kwa madawa ya kulevya. Pia hii kamati iliyobaki chini huku itafute na wengine wafanywe *technical committee*, hao kila siku wanaweza wakakutana kwa sababu hawana vikwazo vyengine hawa. Mhe. Mwenyekiti, mimi suala langu lipo hapo kwanza la kufanyika hivyo vikao na kuweza kuendesha mambo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 4(a) baada ya ile tume sasa kuna na kamati tendaji. Mimi nasema katika mambo haya hakuna haja ya kuunda makamati mengi, kuna mambo ile *profession* yake mtu ndio atekeleze sio lazima awemo katika ile kamati. Kama *profession* yake mtu yuko bandarini ina maana yeye anatakiwa afanye ile kazi ya bandari na anaweza kuitwa wakati wowote na viongozi ili kupewa taarifa zinazohusiana. Lakini wale watu ambao wanatarajiwa waunde kazi wataundiwa kamati na matokeo yake itakuwa ufanisi haupatikani.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka kuzungumza mimi, unaona kifungu cha 5 kinasema tume itafanya vikao vyake mara mbili kwa mwaka ikizingatiwa kuwa ikitokezea dharura tume inaweza kukutana katika kikao cha dharura. Mhe. Mwenyekiti, haya ndio niliyosema kwamba kutokana na dharura iliyopo mara mbili kwa mwaka pia ni vikao vidogo sana, huko siku za mbele tutakapoweza kurekebisha mambo yatakuwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine katika kupambana na madawa ya kulevya ni kwamba hatuwezi kupambana na madawa ya kulevya ikiwa hatujajenga *confidence* ya serikali mbele ya wananchi wake. Mhe. Mwenyekiti, tukishajenga *confidence* ya serikali mbele ya wananchi wake ni moja katika mapambano wenyewe ya madawa ya kulevya. Kwa hivyo, hebu fanyeni ikiwa kuna kifungu kinakosekana au hakipo basi fanyeni akamatwe mmoja tu, mbona Brazil wale wanaoleta madawa hasa wanakamatwa hata kama ni kwa bunduki lakini wanakamatwa. Lakini hapa vinakamatwa vidagaa tu hakuna papa hata mmoja aliyekamatwa, kweli hatuna uwezo huo. Mhe. Mwenyekiti, unajua baadhi ya mambo wananchi wako tayari kusaidia, na mimi nazungumza haya juzi nilizungumza kidogo kwenye semina watu wakawa hawakunifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mwaka jana tulipitisha sheria hii ya madawa ya kulevya, mimi wakati ule nilikuwa Waziri Kivuli wa Afya na ile ililetwa na Wizara ya Afya. Pia ilitakiwa tutoe mchango wetu sisi sehemu ya upinzani kuhusiana na sheria ile. Mimi nilifanya utafiti kama nilivyotarajiwa na nikakutana na watu wakubwa kidogo ambao walikuwemo katika vikosi vya kupambana na madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba askari wanatishwa, hilo ni jambo la ukweli kwamba askari wanaokamata madawa ya kulevya wanatishwa. Mhe. Mwenyekiti, akikamata wale wateja inakuwa hakuna tatizo, lakini akitaka kuingilia wenyewe hasa tatizo lipo, na mimi hilo nimepewa kwamba lipo. Kwa hivyo, tusidanganyane tumkamate mtu mmoja hapa utizame lakini kwa kukamata vidagaa tu hivi, kwa kweli tutahangaishana. Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya inatakiwa zitolewe fedha zifanywe *under cover agency*

wapewe hata kama itachukua miaka miwili, sisi tusijali muda. Lakini siku watakaokamatwa basi tutampeleka kwenye MV. Mapinduzi akaizamuwe, maana itakuwa ni mtu wa kweli huyo na lazima tufunge kazi kwanza na tufanye sherehe. Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio mawazo yangu kwanza lazima pafanywe kazi akamatwe huyu anayeleta.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kwamba sisi tunafanya kazi na tunaunda sheria, lakini ni kwamba hatuweki nyenzo. Mimi huwa najiuliza ni nchi gani ambayo hata hivi leo haina hata *helicopter* moja duniani ni nchi gani? Mhe. Mwenyekiti, hoteli ya kitalii ina *helicopter* inashindwa nchi, hebu Mhe. Waziri wa Fedha atusaidie zile *MBRI* mara hii tununueni *helicopter*. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaomba wajumbe tuchangie laki moja moja ya mafuta kila mwezi, tukitaka *helicopter* mpaka tupige simu Dar es Salaam au hoteli ya kitalii, si aibu hiyo. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo pamoja na sheria zetu kama nilivyosema mimi kuwa nawaamini kamati walivyofanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, tukija katika suala la fedha haramu sisi tuna mabenki ambayo tumeyapa leseni hapa, je, katika sheria hii ni kifungu gani ambacho kinatupa uwezo wa kufuatilia katika hizi benki ambazo ni matawi tu hapa yamefunguliwa. Mhe. Mwenyekiti, tunaweza tukasema kwamba watu wanakuja kusafisha fedha zao hapa Zanzibar, lakini kwa kuzifuatilia. Je, ni kifungu gani ambacho kitatupa uwezo wa mtu kumfuatilia fedha zake ambazo ziko katika benki, hususan benki ambayo ni tawi tu hapa lakini imeenea katika ulimwengu mzima.

Mhe. Mwenyekiti, ilipokuja shindikizo hili la kusafisha fedha haramu kulikuwa na tatizo moja lilijitokeza, ni kipindi hicho hicho ndio kulikokuwa na ongezeko la neno “magaidi” na hata humu nimeliona. Kwa bahati mbaya sana liliathiri shughuli za kidini kwa sababu kuna taasisi zilikuwa zinapokea fedha kutoka nje kwa kuendeshea shughuli zao za kidini. Na wakati ule ilionekana kwamba kwa sababu michango mengine inakuwa haiko wazi, ni watu wenyewe wanajikusanya wanasaidia zile jumuia. Je, katika sheria hii ni wapi ambapo italindwa fedha ya aina hiyo na isichanganywe na ile usafishaji wa fedha haramu, fedha ambazo zinakuja kutokana na wafadhili mbali mbali husaidia kuendesha taasisi za kidini. Kama vile skuli za kidini au kusaidia misikiti, au kusaidia madrasa au kusaidia shughuli zozote zile za kidini. Je, kuna kifungu gani ambacho kimelinda hili isichanganywe zile fedha haramu za madawa ya kulevya na mengineyo zikachanganywa na utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa iwapo marekebisho haya yanapelekea kwenye uzima wa sheria wenyewe, napenda niunge mkono hoja, lakini kwa kusisitiza tena kwamba tunamuomba sana Mwanasheria Mkuu alisaidie

Baraza hususan wale wanaopenda kujishughulisha ili tusije na kurudi kama vile sokoni. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii leo kuweza kuchangia mswada huu wa madawa ya kulevya. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutupa pumzi sasa hivi tungali hai sote waheshimiwa wa Baraza lako hili tukufu. Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpe hongera sana Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu kuwa una lengo la kuwaokoa vijana wetu katika hali hii ambayo sasa hivi wanapotea.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sana mimi nikichangia huwa naweka msisitizo, maana ya kuweka msisitizo ni kuwa mara nyingi sana huwa tunapenda kutunga sheria, lakini utekelezaji wake unakuwa uko taratibu sana. Kwa hivyo, hapa mimi mara nyingi huwa mnyonge kabisa kwa kuwa tunatunga sheria nzuri za kuwasaidia wananchi wetu, lakini utekelezaji wake unakuwa ni mdogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sana mnatwambia msipende kuyarejea rejea yale mazungumzo ambayo mjumbe ameshayasema. Lakini kila mtu ana staili yake katika kuyaeleza, hata hizi sheria *formality* yake ni refu sana utakuta huyu ana kipengele hiki cha sheria cha kumtoa mtu, utakuta na huyu na yeye anasheria ya kumtoa mtu. Kwa hivyo, mheshimiwa sheria utaikuta ndio ile ile lakini kila mtu ana ufasaha wake jinsi ya kuweza kuizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nataka nianze na huu ukurasa wa 262 kuhusu kuanzishwa kwa hiyo tume. Mhe. Mwenyekiti, watu wengi sana wameilalamikia hii tume, na kwa kuwa hii tume imebeba shehena kubwa sana ya mawaziri na ndipo hapo wajumbe wakawa wana woga hapo na ndio maana wakawa wanapenda sana kuisema. Mimi nasema tungewaondoa hawa mawaziri basi kusingekuwa na tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna mheshimiwa alisema kuwa mara nyingi sana waheshimiwa wetu wanakuweko katika vikao vyao vya juu. Kwa hivyo, sio rahisi Mhe. Mwenyekiti, kama tunakusudia kutaka kuondoa suala hili basi hawa waondoke ili tuweke mustakbali mzuri wa kuliondoa tatizo la madawa ya kulevya hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, vyengine vyovyote haitowezekana.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Mhe. Waziri sio mtendaji katika hali halisi ilivyo, waziri ni mtu wa kupewa na akipewa mara nyingi sana waziri ndio inapolichukua lile suala akalilaza kwenye meza yake. Mhe. Mwenyekiti, hatimae bado tungali na matatizo yale yale.

Mhe. Mwenyekiti, nimesoma hawa watendaji walioundwa kwenye tume hii, lakini sijaona hata mwakilishi mmoja ambaye na yeye ameoneshwa humu kuingizwa kwenye hii tume. Naamini kabisa Mhe. Mwenyekiti, kama tunataka kufanya basi tusiogope, hivyo naomba waingizeni wawakilishi kwani ndio wenye hasira kabisa na jambo hili na ndio watakaoleta kitu cha maana kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sana wajumbe wanaogopwa katika tume nyingi sana, sijui kwa sababu gani wanakuwa hawahusishwi kwenye tume nyingi sana. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba sisi ndio tunaokaa na wananchi, sisi ndio tunaopata ripoti kwa wananchi, tunajua moja hadi mbili. Lakini leo utakuta hujahusishwa kwenye kamati niambie utalipeleka wapi, hatimae unalitia kwenye mfuko, na unajua kama ile ni hasara kubwa lakini sasa utafanya nini. Mhe. Mwenyekiti, hebu na wamuingize mwakilishi waone atakavyofanya ni kwamba atajitahidi kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kuwa wengi wamesema hapa kuhusu Mahakama na wengine wamesema kuhusu masuala ya polisi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikwambie ukweli ulivyo ikiwa tuko makini na jambo hili la kama tupo hapa tumekaa tunapiga makofi kwenye meza na kula pesa za watu, basi tusifanye hivyo. Lakini kama tuna nia hasa ya suala hili mheshimiwa mbona ni kitu rahisi tu wala hakina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na polisi wangu kwanza hawana nyenzo, hili naomba tukubaliane nalo. Mhe. Mwenyekiti, unapotaka kumtuma polisi na unapotaka kumpa kazi polisi basi ujue kwamba hana nyenzo. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu polisi wanapigana kweli kweli na wanapata shida kwenye mitaa yanapigwa mawe na hao wanaokula madawa ya kulevya. Lakini akiumia hata kitengo cha kumsaidia kwenda kufanya matibabu yeye anakuwa yupo tu, hata huyo askari mwenyewe atakuwa hana nia ya kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ni kwamba hakuna siri kwa sababu leo wananchi wanataka kujitokeza kulisema neno hili, lakini hatimae anapokwenda kupeleka ripoti anakuta siku ya pili anapewa hongera yule mtu ambaye aliyetumwa ile kazi akaifanye anakwenda kupewa yule aliyepewa ripoti anakwenda kupewa hongera. Mhe. Mwenyekiti, hii kazi sio masihara, kazi hii inataka ujasiri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema kuna mapapa makubwa ambayo hayatajwi, sio kitu cha mchezo papa kubwa uende ukalisema basi litakuondoa na hulivui hilo papa kubwa asilani. Kwa sababu

kutokana na hali halisi ilivyo tusidanganyane mimi nasema ukweli tuuseme hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada zake Mwanasheria Mkuu kurekebisha sheria, lakini bado sheria ingali ngumu mimi namuamini sana mwanasheria wangu. Lakini bado kwa tatizo hili la madawa ya kulevya ni kwamba bado sheria ingali ngumu ukweli tuuseme hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba polisi anafanya kazi yake anapoukamata ule unga anaufikisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambaye zamani tukimwita basi hapo ndipo kunakochezwa mchezo. Mhe. Mwenyekiti, polisi kazi yake imeisha, polisi ametengeneza jadala lake, anang'ojea ripoti kutoka kwa huyo ambaye tulomsema hapa ambaye ni Mkemia Mkuu wa Serikali, hatimae hapo ndio unapoambiwa ule sio unga lile ni jivu.

Mhe. Mwenyekiti, nina historia napenda kusema kitu ambacho tayari nimekiona kabisa wala hakibabaishi. Mhe. Mwenyekiti, kuna wakati fulani nilipigiwa simu katika ukanda wangu wa Kiwengwa, nikaambiwa mheshimiwa njoo huku tumekamata kete hizi za unga. Mimi nikenda maishani mwangu sijapata kuona unga hata siku moja na nilipofunguliwa tu nilianza kwenda chafya. Nikasema ndio hali yenyewe umefunguliwa tu wala sijaula nimekwenda chafya, nikasema kweli huu ndio unga.

Mhe. Mwenyekiti, polisi baada ya kukamata ule unga na kuhakikisha kwa *experience* yake, anajua kama huu ni unga, lakini hana sheria yeye ya kusema moja kwa moja kama huu ni unga mpaka ampelekee Mkemia ambaye anahusika aliyewekwa na chombo cha serikali kwa mujibu wa sheria. Mhe. Mwenyekiti, hapo tena ndio yanakuja majibu unaambiwa ule sio unga, ule ni unga wa saruji. Kwa hivyo, yule inakuwa hana uwezo tena hapo, ule ni unga wa ng'ano wewe umekosea tu, atafanya nini Jaji, polisi atafanya nini na ameshaambiwa kitu kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiria kama kweli tunataka tumuweke mtu ambaye tayari ana imani hiyo, hapo ndio tutakwenda vizuri, asiwe mbabaishaji, asiwe mchakachuaji. Mhe. Mwenyekiti, na mazingira gani ya kumjenga huyu Mkemia Mkuu ni kwamba mumuongezee mshahara, mkimuongezea mshahara hachakachuwi lakini unampa mshahara mdogo asichakachue vipi yeye ni masikini milioni kumi hajapata kuiona. Mhe. Mwenyekiti, sisi tatizo letu ni mshahara, hili suala la mshahara siku zote nitalisema na nitaendelea kulisema kwamba mshahara kidogo ndio unaombadilisha mtu kuwa na mazingira mabaya. Mhe. Mwenyekiti, kama utakuwa na mshahara mzuri basi maendeleo yatakuwepo tu na wataalamu tutakuwa nao hawakimbii tena nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona tatizo ni hilo na lazima hili tuliseme kwani hii hatari, mshahara wetu ni mdogo. Mhe. Mwenyekiti, hivyo kweli leo Mkemia Mkuu kama atapewa shilingi 300,000 na ana kazi ngumu basi ni lazima atafanya manyago pale. Mimi nasema ni lazima atafanya manyago yake, nayo hayo tumjengee mazingira mazuri kama vile Mkemia apewe gari, apewe nyumba. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Mkemia ahifadhiwe kama wanavyohifadhiwa mawaziri, wasikaribiane na waziri tu lakini ajengewe mazingira mazuri ndipo hapo habari hii ya madawa ya kulevya tutaondoa.

Mhe. Mwenyekiti, tukija na hao polisi nao vile vile tuwaandalie mazingira mazuri, na majaji wetu nao mwenyewe Mhe. Waziri yupo hapa wa Utawala Bora, nina amini sana Mhe. Waziri Mhe. Jussa hapa alisema tupo katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni kuleta nema katika nchi kama vile kuboresha mambo mengi ili yaelekee na jina la Serikali ya Kitaifa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atawaona sana Majaji hawa mishahara yao yaangaliwe kuanzia Mahakama ya mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mkoa mpaka kufika juu huko. Hapo kidogo ndio tutaweza lakini tutasema siku zote.

Mhe. Mwenyekiti, kama serikali yetu haijarekebisha mishahara basi tusidanganyane mambo haya ya rushwa lazima yatakuwepo. Jambo la pili ni kwamba hawa vijana wetu tunakusudia kuwaondoa katika hali ambayo wako nayo sasa hivi na tuwaeke katika hali ambayo iliyokuwa ya kibinadamu. Mimi nafikiri serikali iwe na kazi za kuwapa hawa vijana, tusiwe wabahili. Mhe. Mwenyekiti, leo mtu tunamtoa mle katika hali yake ile tunamwambia wewe acha madawa ya kulevya, baada ya muda yule yule anaendelea kwenda kula tena madawa ya kulevya ni kwa sababu hukumshughulisha na kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni hali ya hatari ambayo ndio inasababisha kuwa vijana wanarejea mambo yao hata waende chuo gani, wahifadhiwe na nani, wapelekwe mental hiyo yote ni bure tu. Lakini akitoka kule hebu mpe kibarua cha kufanya uone kama ataendelea kula madawa ya kulevya, maana yake ile dawa mtu huwa anakula kwa raha zake. Kuna wengine wanakwambia tunakula madawa ya kulevya ili tufike Marekani, kwa sababu zile hisia zinakuja tu anaona mimi nikila madawa ya kulevya basi Marekani nimeshaingia. Ni kuwa kila mtu ana hisia zake basi hisia zile sisi hebu tuwafanye kuwa mu ajisikie tajiri apewe fedha za kujikimu, hapo ndio tutawaweza lakini tukisema tu kwenye *paper* tunatunga sheria tutawafunga bure hawa. Sasa mimi ningeomba tuwanusuru kwa kuwatafutia kibarua cha kazi au miradi ya kujiendesha vijana hawa wasirejee tena.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nisifu kitu kimoja katika Jeshi la Polisi sasa hivi wameweka polisi jamii. Kwa kweli polisi jamii ni nzuri sana, lakini mimi najiuliza hawa polisi jamii watapoumia watalipwa nani? Hebu tuangalie suala hili mazingira yake, wanafanya kazi ya kulinda kwa mikono na kirungu, wanapambana na mtu ambaye ana silaha Mwenyezi Mungu asitujaalie hayo, lakini anapambana na mtu mwenye silaha akiumia tuulize huyu kifungu gani kitamlipa? Hili tulione Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sasa hivi wazee na vijana wameshaikubali polisi jamii lakini tunawajengea mazingira gani au tunahamasisha tu, tutawamaliza.

Mimi ninachoomba kuwa tunaweka polisi jamii na tuwatendee au tuwape *facilities* zote ambazo zinahusika na wao isikaribie kama yule polisi mwenyewe, lakini tuwatengezee mafungu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea lazima sasa hivi tuhamasike katika majimbo yetu, tuhamasishe na tuhamasike viongozi hasa sisi wawakilishi ili kuwatafuta wale ndugu zetu wanaokula madawa ya kulevya na tuwaulize tatizo ni nini hata ufanye hivi? Sasa tuanzie kwa wawakilishi halafu tuje kwenye daraja ya juu. Lakini pia turuhusiwe sisi kwenye majimbo yetu tujenge na vituo.

Mhe. Mwenyekiti kuna jambo moja linasikitisha kabisa, kuwa leo Mwakilishi anataka kujenga kituo cha polisi katika jimbo lake kwa kunusurisha hatari na mambo ya ugaidi leo ananyimwa ardhi kwa nini? Hii inasikitisha ndani ya moyo, tunafanya nini sasa, kama wapo wahusika wa ardhi mpeni ruhusa mama ajenge sasa mwakilishi yule tuondoe tatizo hilo, tunang'ang'ania nini, yeye hataki kujenga holi la densi yule anachoataka kujenga ni kituo ambacho kitalinda wananchi wake, nani asiyejua eneo lapela kama watu wanabakwa?

Watu wanabakwa pale, watu wanawekwa magari yao mawe, ameona fikira hizo ni bora niwajengee wananchi wangu kwa kuwalinda leo tunakwenda kumkatalia halafu tunaleta miswada kama hii tuondoe matatizo hayo kumbe sisi wenyewe ndio tunaendeleza kuweka matatizo hayo, ukweli tuuseme ni huo, sisi wenyewe na si hasha tukaambiwa sisi wenyewe mawaziri na wawakilishi ndio tunaosafirisha unga tusikatae. Kuna viashirio, hili tuliseme kuna viashirio vinawezekana, inawezekana kiongozi wa juu akashiriki kupitisha unga imo hiyo tusikatae na hili tulikubali. Ndio maana Makamo wangu wa kamati akasema inawezekana kuna mapapa si ndio hayo? Ndio mapapa yenyewe hayo viongozi wa juu inawezekana na ndio ilivyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu kasema hapa hata *VIP* iheshimiwe, ndio unaweza kumleta mtu kumbe anavyo mule amevihifadhi utajuaje Makame Mshimba

kaja na mgeni wake tu kumbwe ana mali ndani ya mfuko. Mhe. Mwenyekiti anapita pale keshakwenda kuuwa watu.

Sasa mambo haya Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tuyaseme, tujirekebishe sisi wenyewe viongozi. Mheshimiwa anataka kujenga eneo la usalama pale wananchi wake wasidhalilishwe na ukienda sasa hivi hebu piteni usiku vijinga tu vya moto unaviona viko kule unafikiria kunapikwa maji kule? Anazuiliwa. Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Mwenyekiti hilo suala tuliangalie bwana mtupe ruhusa ya kujenga vituo na ndio maana tukataka polisi shirikishi ndio hiyo sasa.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa huu wa 263 ndio yale yale ya kamati tendaji, huku tumesema kamati hiyo, tume itakuwa na wajumbe wafuatao na huku kamati ndio wale wale Mhe. Mwenyekiti hayumo hata mwakilishi. Mhe. Mwenyekiti tutafika wapi, mimi naiomba wizara husika hebu tuangalieni na sisi Waheshimiwa Wawakilishi mtutie katika hizi kamati msione tabu, sisi ndio tunao-*deal* na jamii, sisi ndio maskani zetu kwa vijana, sisi tunajua ripoti zote sasa leo kama hukunitia humu utazipata wapi ripoti, hata siku moja Mhe. Waziri *Wallahi* nakuonea huruma sana, una nia nzuri lakini *finishing* yake itakuwa *poor* na mimi ninavyokujua wewe uzoefu wako ukiungwa mkono na Mwanasheria Mkuu Mwenyezi Mungu atujaalie salama sasa kweli tuna nia ya kuondoa madawa ya kulevya.

Kuna mmoja ananambia unapiga debe, sipigi debe Mwanasheria lazima nimsifu, ukweli niseme.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kuwa naunga mkono kutokana na sheria hii au mswada huu, kwa kweli nimefarajika sana kuwa sasa hivi tuna nia ya kutaka kuondoa matatizo haya ya waletaji na wavutaji unga. Mimi niombe dua kwa Mwenyezi Mungu atujalie tuikamate hii sheria na niipitishwe haraka na Mhe. Rais aitie saini ili tuweze kuifanyia kazi kwa haraka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia nafasi hii na nitagusia husia tu, kwa sababu mswada huu umechangiwa na watu wengi ambao wametoa miongozo na baadhi ya vipengele visahihishwe.

Lakini kwanza niseme *Bismillahi Rahmani Rahym*, ewe Mwenyezi Mungu nakuomba na magharibi haya hayo waleta madawa ya kulevya wote

uwaangamize. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kwa semina tulioipata juzi watoto wetu na wajukuu wetu wanaangamia. Nichukue nafasi hii niipongeze sana Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na watendaji wake na waziri wao, lakini pia nimpongeze na Mwanasheria Mkuu. Kwa sababu katika maisha yangu yote ile ndio semina iliyonifungua kichwa ikanionesha kwamba baadhi ya semina zinatakiwa ziwe namna ile, maana yake wanatuonesha hali halisi ya vijana wetu wanavyoangamia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niseme suala hili la madawa ya kulevya linakwenda sambamba na UKIMWI kwa sababu chanzo cha UKIMWI ni madawa ya kulevya Mhe. Mwenyekiti, sasa sijui tumeiweka wekaje. Kama kuna uwezekano basi tuseme madawa ya kulevya *plus* UKIMWI.

Mimi nataka niunge mkono baadhi ya wenzangu waliochangia, mimi najiuliza hivyo mtu kweli atoke Marekani au Pakistani ameze vidonge vya unga wa ngano au sembe? Kwa sababu tunaoneshwa kwenye televisheni vimepatikana sijui kete ngapi lakini matokeo yake kete zile zinapotea. Sasa tunajiuliza zinapotea zinakwenda wapi? Hivyo mtu ameze ndani ya tumbo lake pipi zinazofika mia moja au na ishirini kweli uwe ni unga wa ngano au wa sembe ule? Hapa kuna kizungumkuti.

Sasa naomba na niiombe sana serikali itafute kizungumkuti hiki kinatokea wapi. Kwanza naomba yule anayekamatwa akanyeshwa pipi zile zikageuka mavi basi atiwe yeye ndani kwanza achukuliwe hatua. Halafu baadae ndio ifuate *process* nyengine, lakini la kushangaza inasemekana kwamba Zanzibar ni kitovu kimoja wapo cha kupitisha madawa ya kulevya. Amesema mwenzangu Mhe. Ismail Jussa hapa, kwa sababu sisi wenyewe ni kisiwa halafu tuna visiwa vidogo vidogo ni dhahiri kwamba kweli Zanzibar ni kitovu cha madawa ya kulevya. Kwa hivyo, naiomba serikali na sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwe miongoni mwa kuisaidia serikali kwa sababu tunalalanao, tunaamka nao, nyumba ya jirani yako, lakini tunapishana hivi hivi kila mmoja anaogopa. Tunaoneana muhali kusema fulani ndiye mwenye kuuza unga huu.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ikishakupita sheria hii serikali ijikaze sana, lakini kwa upande mwengine vifaa vyetu ni kidogo. Tulikuwa na mbwa hapa nasikia alikuwa mkali kweli kweli, lakini hata sijui alifanywa nini mbwa yule alipoonekana anafichua fichua mambo wee hakuonekana. Sasa huu muhali na kuoneana haya watu wanatajirika wala hufikirii utajiri ule wanaupata wapi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nilisema na mimi nitilie mkazo lakini narudia tena kwamba wanaoleta madawa ya kulevya Mwenyezi Mungu awaangamize, kama wanavyotaka kutuangamizia watoto wetu basi na wao Mwenyezi

Mungu awaangamize. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii kuwa hapa kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu tukiwa wazima wa afya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuungana na wachangiaji ambao wamechangia mswada huu wa Sheria ya Kurekebisha baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora nadni yake, ambapo ndani yake pia kunarekebishwa Sheria za Kuzuia Dawa za Kulevya Nam. 9 ya mwaka 2009.

Mhe. Mwenyekiti, sote tuliomo humu ndani tunakubaliana kwamba tatizo la matumizi na uingiaji wa madawa ya kulevya katika visiwa vyetu ni zito na semina ya juzi ambayo tulibahatika kuipata tushukuru sana ambao walikuja kutufanyia semina ile kutoka vyombo mbali mbali walielezea ukubwa wa tatizo lenyewe. Mimi nashukuru kwamba hapa tulipo sasa tunajijua hasa kama kisiwa hali yetu na suala zima kwanza la uingizaji wa dawa za kulevya lilivyo lakini vile vile jinsi gani vijana wetu wametumbukia katika matatizo ya kutumia madawa haya ya kulevya na athari mbali mbali za kifamilia, kisaikolojia na athari za kiuchumi ambazo nchi yetu inapata kutokana na vijana wetu kujiingiza katika matumizi haramu ya madawa haya ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu nitapenda sana kuzungumza katika mswada huu wa sheria hii ya kurekebisha sheria hizi tatu (3) katika sheria hii ya kurekebisha sheria ya Tume ya Kuzuia Dawa za Kulevya. Napenda nizungumzie machache kuhusiana na wajumbe ambao wamezungumza.

Kwanza nikubaliane na wajumbe wote kwamba kweli tatizo hili ni zito wameliona kwa uzito wake na kwamba imefika wakati sasa Zanzibar tuungane nguvu katika kupambana na vitendo hivi haramu vya kuingiza dawa za kulevya lakini vile vile kuweza kuzuia vijana wetu kuingia katika matumizi hayo. Hayo yatawezekana ikiwa tu, tutaweza kudhibiti uwepo wa dawa hizi ndani ya visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wengi waliozungumzia katika sheria hii wamezungumza suala zima la kuwa na ukubwa wa tume yenyewe na kwamba labda ukimuacha Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais ambaye ndiye Mwenyekiti wa tume hii kuna mawaziri pale kama wanane na kuna viongozi wengine wazito.

Tumetanguliza sote kusema kwamba suala hili ni zito na jinsi ya uzito wake na ukubwa lilivyo litahitaji maamuzi mazito yafanywe na kwa haraka mno. Kwa hivyo, hiyo ndio maana tume hii ukaona kwamba kwanza ina mawaziri. Mhe. Mwenyekiti, mawaziri kama alivyotangulia kusema mjumbe wetu mmoja wao si watendaji lakini ndio wanaotoa maamuzi katika sehemu ambazo wapo.

Kwa hivyo, suala zima la dawa za kulevya ni suala ambalo linagusa pande zote. Kwa mfano, ukija kwenye Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa nini Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili yupo pale, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ndio wasimamizi wa shughuli zote za serikali, kwa hivyo wao lazima wawepo pale.

Lakini ukitizama waziri mwenye dhamana ya afya waziri huyu lazima awepo hapa kwa sababu ya kuweza kuwahudumia vijana wetu. Tunasema kwamba vijana wetu wanapojiingiza katika matatizo haya wanahitaji utibabu kwa sababu wanaathirika na maradhi mbali mbali yakiwemo maradhi ya UKIMWI, maradhi ya homa ya ini na mengineyo. Kwa hivyo, ni muhimu sana tuwe na mtu ambaye anatoka Wizara ya Afya anayeweza kufanya maamuzi katika ngazi ya juu kabisa na ndio maana tuna Waziri wa Afya.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, sitaki nieleze umuhimu wa mmooja mmoja najua wajumbe watanifahamu kwa nini wajumbe wote wako hapa. Kila mmoja ambaye yuko hapa yupo kwa sababu tume ikitaka kufanya maamuzi baada ya kupata kazi ambazo zimefanywa na kamati tendaji basi iweze kupata watu ambao ndio wenye maamuzi. Sasa ukimleta Mkurugenzi hapa Mhe., Mwenyekiti, yeye hawezi kutoa maamuzi yoyote juu ya wizara yake itabidi arudi ofisini kwake akaonane na Katibu Mkuu, atoke tena akaonane na waziri ili kauli ya wizara hile ipatikane.

Kwa hivyo, hapa hakuna suala la mchezo ni suala la maamuzi mazito na ya haraka, ndio maana tume hii ikataka kuwa na viongozi hawa wakubwa ambao ndio wanaofanya maamuzi katika sehemu zao.

Lakini vile vile kuna baadhi ya wajumbe wameelezea pia hii kamati tendaji ya nini, labda ni jina tu ambalo linatumika. Lakini hii naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wajumbe kuwa hii ndio *technical committee*. Hawa ndio hasa watendaji wa shughuli zenyewe, na kwa mujibu wa masuala yenyewe yalivyo wametoka katika sehemu ambazo ndio hasa wataweza kushughulikia masuala yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, niliona kwanza niliweke sawa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo limezungumza sana kwa hamasa karibu na wajumbe wote ni suala zima la kuwashughulikia ndugu zetu na watoto wetu

ambao tayari wameamua kuacha dawa za kulevya na wanahitaji huduma za kuweza kuwasaidia kuacha, lakini pia nini kitatokea baadaye.

Naomba kwanza nianze na Mhe. Ismail Jussa ambaye yeye alilizungumza kwa mapana yake kwamba katika marekebisho ya sheria hii tumeondosha kipengele kizima cha kusema kwamba, wale vijana watakaokamatwa wakithibitika kwa kupimwa mkojo kwamba wametumia dawa za kulevya watawekwa ndani kwa kifungu cha miezi sita lakini baadae watapelekwa katika kituo cha kurekebisha tabia ili watoke wakiwa vijana bora katika jamii yetu. Niseme tu kwamba amefahamu kwa nini tumekiondoa kipengele kile, lakini pia nimhakikishie kwamba nia ya serikali bado ipo pale pale, kiwanja chetu tunacho na tayari kimepimwa na kimehifadhiwa kwa kuepusha kwamba kisije kikavamiwa kiko Tunguu na jitihada za kutafuta ufadhili wa kutengeneza kituo hicho zinaendelea hatukusita.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi tunagonga mwamba na wenzetu wanakuwa na sababu zifuatazo ambazo kwa upande mmoja ukizitizama nazo zina maana yake.

Wenzetu wengi washirika wa maendeleo ambalo tunajadiliana nalo kuhusiana na kutaka msaada katika hili wanatushauri zaidi tutumie *drop out center*, yaani tusiwe na kituo kama hospitali cha kuweza kurekebisha tabia na ku-*rehabilitation* wale ambao wanaacha dawa za kulevya. Na kwa nini wanasema tusiwe na kituo hicho? Ni kwa sababu gharama zake zitakuwa ni kubwa. Kwa sababu ni sawa sawa uwe na kama hospitali, uwe na huduma zote kama nyumba kabisa, uwe na wahudumu, watu wa hospitali na huduma zote. Tumeona ni ugumu kiasi gani ndugu zetu ambao wamejitolea kuanzisha *Sober House* wanaoupata katika kutekeleza kazi yao hii.

Kwa hivyo, wametushauri kwamba ni vizuri sana tuwe na *drop out center* kuliko kujenga *rehabilitation center* ambayo itakuwa na maana ya ku-*accommodate* moja kwa moja kama inavyofanya *Sober House*. Hata hivyo, sisi tunaona kwamba yote mawili ni ya busara, wako ambao wataweza kwenda kwenye *drop out center* lakini wako ambao watahitaji kuwekwa kwa kipindi fulani. Kwa hivyo, bado serikali ina nia ya kujenga *rehabilitation center* hii na juhudi za serikali yenyewe pamoja na wahisani zinafanywa ili kuona kwamba kituo hiki kitajengwa siku moja. Hivyo nimtoe wasi wasi kwamba tunaelewa umuhimu wa kuwepo na mahitaji ya dunia yalivyo vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo limezungumzwa kuhusiana na *Sober House* ni suala zima serikali kuzisaidia *Sober House* hizo. Niseme kwamba kwa kiasi fulani mwaka huu ikiwa ni wa kwanza katika awamu hii *Sober*

House ilipangiwa bajeti ya aina mbili, hapa naomba Mhe. Jussa anisikilize vizuri sana. Kuna bajeti ya shilingi milioni kumi hii ni ya moja kwa moja kutoka Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwenda kwenye *Sober House*, wakati tunapanga bajeti hii kulikuwa na *Sober House* Unguja na Pemba jumla yake ni tisa (9), tunajua ni pesa kidogo tungependa ziwe zaidi lakini bajeti yetu ni ndogo sana, lakini tulisema lazima tuanze. Baada ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na mimi mwenyewe kutembelea *Sober House* hizi tukaona kazi kubwa wanayoifanya tukasema ni lazima tuwasaidie.

Hata hivyo, Waziri, Katibu Mkuu, Makamo wa Kwanza wa Rais mwenyewe na wafanyakazi wa ofisi wenyewe binafsi wamechangia fedha za kutosha ndani ya *Sober House*. Lakini ni lengo la serikali kuona kwamba tunaendelea kuzisaidia.

Vile vile tunafanya usaidizi kwa kiasi fulani kuwasaidia akinamama ambao hawana uwezo na watoto wako tayari kuacha sisi wenyewe binafsi tu, tulioko pale ofisini kuwasaidia kuwalipia kuwapeleka katika *Sober House*. Kwa hivyo, hatuwaachii tu wawakilishi peke yao lakini na sisi wenyewe mmoja mmoja tunaingia katika jitihada hizo kwa jinsi ya kuona kwamba vijana wetu wanarekebishika kitabia na kurudi katika jamii.

Pia kuna suala la fedha shilingi milioni arobaini na saba ambazo wakati najibu hoja za wajumbe katika kikao cha bajeti nilizungumza. Ni kweli na hilo nililizungumza kwamba kwa kupitia *ZAC* yenyewe itatenga shilingi milioni arobaini na saba kwenda kwenye *Sober House*. Hilo ni kweli nimesema na bado liko pale pale, lakini ni kwamba fedha hizi ni za wahisani na kama mtakumbuka vizuri wajumbe walihoji sana hapa kwa nini Tume ya UKIMWI ina fedha nyingi?

Tukasema kwamba, tuna fedha hapa zinakwenda kwa wadau wengine na shilingi kama milioni arobaini na saba zinatakiwa kwenda kwa *Sober House* katika shughuli zao mbali mbali.

Lakini upelekwaji wa fedha hizi unategema pia zinavyopatikana kutoka kwa wahisani. Hii kauli tuliisema na ipo hapa, lakini hizi haziko moja kwa moja kwenye bajeti ya kutoka Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais zipo kutokea Tume ya UKIMWI shilingi milioni arobaini na saba. Na nimeambiwa mpaka hivi juzi karibu shilingi milioni saba zimeshapelekwa katika *Sober House* mbili za Pemba. Sasa inawezekana zimepelekwa kwa huduma ambazo zimepelekwa pale ikawa sio *cash*, lakini ni huduma ambazo zinapelekwa pale kutoka *ZAC*.

Mhe. Mwenyekiti, tunalifahamu pia tatizo tulilonalo kwamba vijana wanaotoka pale wanahitaji kupatiwa kazi za amali ili waweze kutulia nafsi zao na kuweza kufanya vitu vya kujiendeleza kimaisha ili kuwazuia wasirudi tena katika tabia mbaya ya kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inashirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuona uwezekano wa kuwapatia vijana hawa nafasi kwanza kwa kupitia Wizara ya Elimu nafasi katika vyuo vya amali ambavyo tayari tunavyo kama ni *special case* wao wenyewe ili waingie katika vyuo hivyo na kuweza kujifunza kazi za amali.

Lakini pili kuweza kuwakusanya katika vikundi, tukihakikisha kwamba hawa tayari sasa wako vizuri yaani wameacha matumizi na wako tayari kuweza kujiendeleza kupitia Wizara ya Uendeshaji Kiuchumi kuweza kupatiwa mikopo na misaada mbali mbali pamoja na taaluma ili waweze wenyewe kuweza kujiendesha. Niwakumbushe wajumbe tu kwamba suala la kutokuwa na kazi ni suala ambalo linaikumba jamii kwa ujumla wake na sio tu ndugu zetu hao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hii ni *effort* maalum ambayo tunaichukua ili kuona kwamba vijana hawa hawakati tama katika maisha yao na wanarudi katika familia zao wakiwa ni watu wa maana. Tukumbuke kwamba katika hawa wengine ni watu ambao wana wake na watoto yaani wana familia kabisa, hata kama hawana wake na watoto na wengine hawana waume kwa sababu wako wanawake pia waliojiingiza katika madawa ya kulevya, lakini ni watu ambao ni wenzetu katika familia na tungependa siku moja wawe na maisha katika familia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi sitakuwa na mengi sana ya kusema niwashukuru sana wale wajumbe ambao wamechangia katika mswada huu kwenye eneo hili la dawa za kulevya. Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe ambao kama wana taarifa tulikuwa kwenye semina juzi tafadhali sana wazipeleke hizo taarifa kunakohusika, kama kuna taarifa za mapapa na wanajulikana tafadhali sana hizo taarifa zipelekwe na ndivyo tulivyoambiwa juzi na wahusika ndani ya semina.

Mhe. Mwenyekiti, tusiwe waoga na ule muhali ndio tuliambiwa tuuondoshe. Kwa hivyo, kama kuna taarifa zozote unaweza kuzipeleka katika vyombo vinavyohusika kwa ajili ya kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala moja ambalo sitaki pia nilisahau kulisema ni matumizi ya *VIP*. Waheshimiwa Wajumbe wengi Mhe. Mwenyekiti, huwa wanazungumzia suala zima la ulegevu uliopo katika matumizi ya *VIP*

kwamba kuna watu ambao pengine sio wahusika na hata kama ni wahusika lakini hawasachiwi, wanapita na wala hakuna chombo cha usalama.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sifahamu kwa sababu mimi ninaposafiri huwa begi langu nalipitisha kwenye boksi la uchunguzi pale na mimi pia napita kwenye boksi ile la uchunguzi, najua hiyo *VIP* ipo. Lakini kama kuna malalamiko hayo basi serikali imeyaona na tayari kwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, taratibu zimeandaliwa na wategemee kwamba hivi karibuni hapatakuwa rahisi tena *VIP* kupita watu ambao, kwanza hawahusiki na pia kama ndio tunakisia kwamba ndio kunapitishwa vitu vibaya, basi mambo hayo serikali imeyajua na imeyafanyia kazi kwa hivyo, hivi karibu watu watakaa vizuri *VIP*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niungane na Waheshimiwa Wajumbe kuunga mkono hoja hii na niwaombe wote waunge mkono mswada huu, ili tuupitishe tuweze kufanya kazi, nakushukuru. *(Makofi).*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ndogo na mimi kuzungumza machache, kwa kuwa na mimi ni mdau katika sheria hii nikiwa kama Mwenyekiti ninayesimamia hii Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, ambapo moja katika marekebisho ya sheria hii na mimi kwa njia moja au nyengine pamoja na kamati yangu tunahusika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani pamoja na mapungufu ya sheria zetu, lakini kuna vitu tunavikosa. Ukiangalia Zanzibar tuna sheria nyingi nzuri sana na laiti kama ingelikuwa sheria hizi zinatekelezwa, basi nchi yetu Mhe. Mwenyekiti, ingepiga hatua kubwa sana ya maendeleo tena ya haraka sana. Lakini tatizo linalojitokeza kwamba hata akitokezea mtendaji ana moyo mkubwa wa kufanya kazi, basi anafika pahala anavunjika moyo. Hili nalizungumza kwa sababu leo tuna mswada wa marekebisho wa baadhi ya sheria, lakini je, hizo sheria ambazo tumezipitisha kweli tunazitekeleza kama vile tulivyozipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, kila siku hapa tutarekebisha sheria, lakini matunda ya marekebisho ya sheria zile hayaonekani. Mhe. Mwenyekiti, Sheria hizi ziliwahi kurekebishwa baadhi yake na tulikuwa tuna tatizo zaidi kwenye suala zima la sheria yetu ya madawa ya kulevya, kulikuwa kuna kipengele ambacho kinasema kwamba ‘mtu akikamatwa na kuanzia gramu moja ya *cocaine* au *heroine* basi kesi ile inabidi iende mahakama kuu. Mhe. Mwenyekiti, tukaona kuna tatizo na tatizo lile tukasema tufanye nini, hebu sasa turekebishe kwamba hata kama mtu anakamatwa hata kama ni kiasi kidogo tu.

Mfano, kuanzia gramu 1 mpaka gramu 10 au 20 basi kesi hizi ziweze kusikilizwa hata kwenye mahakama nyengine za mikoa. Mhe. Mwenyekiti, hilo limefanyika lakini bado ukiangalia ni jana tu tulikuwa tuna semina sisi, ukiangalia takwimu Mhe. Mwenyekiti, ya wale waliokamatwa na kutuhumiwa na madawa ya kulevya na wengine wamekamatwa nayo *red handed*, wengine wamekamatwa nayo majumbani, wengine katika vyombo vyao vya usafiri. Lakini kuna wengine Mhe. Mwenyekiti, wamekamatwa kutoka nje ya nchi wamekuja uwanja wa ndege pale wakenda kutoleshwa madawa yale kwa njia ya haja kubwa. Lakini bado Mhe. Mwenyekiti, urasimu umekuwa mkubwa wa kutoa hukumu katika kesi zinazohusiana na madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, hawa watu wanaodili na masuala haya ya madawa ya kulevya ni watu wajanja sana duniani, huu mtandao ni mkubwa sana. Wenzetu kule Colombia na nchi nyengine hawa wanamiliki mpaka silaha, wanapigana na serikali yaani wanapambana, wana ndege za kivita, wana mizinga na kila kitu wanapambana na serikali. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tatizo letu sisi sio kama tuna matatizo ya sheria, tunarekebisha kila tunapoona kuna tatizo. Lakini tatizo zaidi ni katika usimamizi na uwajibikaji katika kutekeleza hizi sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tungejaribu kuangalia uwezekano, zaidi kwa hawa watu ambao wanakamatwa na madawa ya kulevya, hasa hawa anaosafirisha kupitia njia ya matumbo. Wanaotoka nje wakaingia ndani ya nchi yetu, halafu baada ya kukamatwa na polisi na kuchunguzwa na kugundulikana ana madawa baadae wakenda kutolewa kwa njia za haja kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo linakuja kwamba mtu anakamatwa uwanja wa ndege, anatolewa madawa yale kwa njia ya haja kubwa, halafu madawa yale yanaondoka kwa mkono mmoja yanakwenda mkono wa pili na mkono watatu. Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio penye tatizo. Ndio maana kule kwenye semina jana na hata leo hapa nashauri vile vile, kungekuwa kuna kipengele katika sheria, pamoja na marekebisho tunayoyafanya. Kungekuwa na kipengele ambacho kinachoruhusu kuanzishwa *one stop center*, kama yanavyokuja mambo ya uwekezaji. Mambo ya uwekezaji kumewekwa *one stop center* ili kupunguza ule urasimu.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la madawa ya kulevya limekuwa kubwa na sasa tatizo ni kuupata ushahidi. Leo ushahidi mtu katoa tumboni, lakini kwenye kesi unaambiwa ushahidi haukupatikana. Lakini kama tutakuwa na *one stop center* watakuwa uwanja wa ndege, kuna polisi watakuwa wanashughulikia madawa ya kulevya, kuna daktari na kuna mkemia. Yaani kila kitu pale pale

kinaangaliwa, ina maana ikitoka pale kesi moja kwa moja inakwenda mahakamani. Lakini leo ikitoka uwanja wa ndege, sijui mtu apelekwe hospitali, akaharishwe ili itoke iende kwa mkemia mkuu, sijui iende kwa mkurugenzi wa mashtaka. Yaani huo urasimu ndio unaosababisha hizi kesi zikawa hazipati hukumu iliyokuwa nzuri.

Kwa hivyo, ndio maana inapotokezea kwamba askari ameshakamata madawa ya kulevya, tayari mtu yule ametoka nje ya nchi. Pengine Pakistani au Brazil au nchi yoyote ile ambako alikobeba huo mzigo, askari baada ya kuona kuwa huyu mimi nimemkamata na ametolewa yale madawa, halafu hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa, basi siku ya pili anapita tena na kibegi chake anapanda pipa anakwenda zake tena ulaya. Je, huyu askari atamkamata tena yule mtu, hawezi kumkamata, kwa sababu ataona aah! Hata nikimkamata kazi ni ile ile.

Kwa hivyo, mimi nadhani katika marekebisho yetu ya sheria haya basi tungeweka kipengele kinachoweka *one stop center* kikaruhusu chombo hicho kikawepo pale pale uwanja wa ndege na wale wanaokamatwa sehemu nyengine utaratibu utaendelea hivyo hivyo. Lakini wale ambao wanakamatwa pale uwanja wa ndege, ni lazima kuwa kuna utaratibu kama huo ili hizi kesi ziweze kwenda haraka haraka.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kesi hizi kuziendesha katika mahakama zetu za kawaida, basi itakuwa tatizo hili haliishi. Kwanza tutakuwa tunatengeneza mianya ya rushwa, kwa sababu kwanza kesi zinashindwa kuwa na ufuatiliaji, kwa sababu askari wa jeshi la polisi wao wameweka kitengo maalum, hiki ni kitengo cha madawa ya kulevya. Kwa hivyo, na afisi ya mkurugenzi wa mashtaka kungewekwa kitengo maalum, watu wa DPP wawe wanashughulikia na madawa ya kulevya.

Vile vile tungekuwa na mahakimu, tungekuwa na mahakama maalum ambayo inashughulikia madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, kesi zingepata hukumu za haraka haraka, lakini kwa utaratibu wa kutumia hizi mahakama za kawaida, basi tatizo hili litaendelea kuwa kubwa, halitibiki hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, ziko nchi za wenzetu ingawa walikuwa wanapata tabu majaji. Majaji nafikiri sijui kama nchi za South America, kuna mahakimu maalum. Sijui kama ni nchi ya Peru au nchi ya Haiti, kuna mahakimu maalum ambao wanashughulikia madawa ya kulevya na kutokana na tatizo hili kwa wenzetu limekuwa ni kubwa zaidi. Kama nilivyosema kule wenzetu wanatumia silaha, wanapambana mpaka na serikali. Matokeo yake hakimu akiteuliwa leo kwamba ni hakimu wa mahakama ya kushughulikia madawa ya kulevya, siku ya pili anamuandikia barua kiongozi wa nchi anamwambia mimi kazi basi. Kwa sababu gani, kwa sababu anajua yeye kazi yake pale ni

kushughulikia madawa ya kulevya tu na kule kwa vile wenzetu wanatumia silaha, basi anajua hapa mimi siponi. Sasa kwa hapa kwetu hawajakuwa na ujasiri huo, hawajakuwa na silaha za kuweza kupambana na serikali.

Mimi nadhani ni lazima tuweke utaratibu, kama kweli tuko *serious* katika kuondoa masuala ya madawa ya kulevya, basi Mhe. Mwenyekiti, tuweke mahakama maalum ambazo zitakuwa majaji maalum wao wawe wanashughulikia madawa ya kulevya tu sio kitu chengine chochote. Kwa nini hatukushindwa kuweka mahakama za manispaa pale, manispaa wana mahakama yao, kuna mahakama ya kadhi. Kama kweli tuko *serious* basi mimi nafikiri tukiweka mahakama hii tutaweza kuondoa tatizo hili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, masuala ya madawa ya kulevya, sio tu kuharibu akili na viwili wili vya watu wetu. Waliokuwepo kwenye semina jana tuliona kwamba kweli kumbe mtu akitumia madawa ya kulevya anakuwa hana akili, mtu anajipiga sindano mpaka puani, ili apate *steam*, hii ni hatari. Kuna watu wanatumia madawa ya kulevya na wanafamilia zao, wameowa na wengine wameolewa. Matokezeo yake hawa wanaotumia madawa ya kulevya baadae huwa wanapata maambukizo ya ukimwi, kwa sababu mtu akishaona hana pesa basi anamtoa damu mwenzake ambaye ameshatumia madawa ya kulevya kisha anajidunga yeye ili apate ile dozi na yeye. Basi matokeo yake Mhe. Mwenyekiti, kama ana ukimwi yule aliyetolewa ile damu basi na yeye yule aliyejitia ile damu anaupata ukimwi anaupeleka nyumbani au anaupeleka kwa mpenzi wake, hivyo anaueneza ukimwi.
Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hata ukiangalia katika takwimu Zanzibar maambukizo ya ukimwi yapo 0.6, lakini ukija katika kundi la watu wenye kutumia madawa ya kulevya wako asilimia 20 hao wanaotumia madawa ya kulevya. Kwa hivyo, ina maana hawa ni hatari sana wanaweza wakaeneza hili gonjwa.

Lakini baya zaidi Mhe. Mwenyekiti, na hili nilikuwa naomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alisikilize vizuri. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa wale wahisani wetu wengi wanaotusaidia katika mapambano dhidi ya ukimwi wameanza kupunguza kasi, zile bajeti zao kwa nchi za Kiafrika wameanza kuzipunguza. Fedha zile kwa kweli zilikuwa zinatusaidia sana. Mhe. Mwenyekiti, tumeshafanyiwa semina mbali mbali, watu wengine wanasema hizi semina ni kupoteza pesa. Mhe. Mwenyekiti, semina sio kupoteza pesa nikutoa taaluma. Kwa sababu katika masuala ya ukimwi dawa kubwa zaidi ni kutoa taaluma.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu tulitembelea Pemba, tumeangalia wale ambao wanashughulikia *sober house* na wale wengine ambao wanajitolea wanaoshughulikia kuratibu watu wenye virusi vya ukimwi. Mhe. Mwenyekiti,

fedha hizi zilikuwa zinasaidia sana. Kuna vijana wamejitolea kupitia *fund* zile wanapata angalau kutia mafuta vyombo vyao, kwa sababu vyombo wanatumia vyao wenyewe, wanatumia kwa ajili ya kufanya ile *out reach program*. Yaani wanawafuata wagonjwa majumbani mwao na hawa ndugu zetu wanawafuata wagonjwa wa ukimwi au wale waliopata maradhi ya ukimwi au maambukizo ya maradhi ya ukimwi wanawafuata mpaka vijijini.

Leo kitu cha kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, ile misaada waliyokuwa wanaipata sasa hivi haipatikani, wanaanza kutulalamikia. Matokeo yake wale waliokuwa wanapata *counseling* kule vijijini, sasa hivi *counseling* wataikosa. Kwa hivyo, ina maana hata ile elimu ya unyanyapaa Mhe. Mwenyekiti, inaanza kukosekana. Kama itakosekana elimu ya unyanyapaa Mhe. Mwenyekiti, maambukizo ya ukimwi Zanzibar yataongezeka, hii asilimia 0.6 na kama hao wafadhili wameshaanza kuondoa mkono wao katika kusaidia mapambano dhidi ya ukimwi, basi maambukizi yatakuja kuwa makubwa sana na tukiangalia Zanzibar ni ndogo.

Leo Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru watu wanajitolea kwa hiyari kupima, kwa nini wakajitolea kwa hiyari kupima. Kwa sababu baada ya kupata taaluma wakaona aah! Kumbe maradhi yenyewe sio aibu ni maradhi ya kawaida mtu yeyote anaweza kuyapata, vijana wadogo wanakwenda sasa hivi kupima na sisi watu wazima tunakwenda kupima, mpaka wazee watu wana miaka 70, 60 au 80 wanakwenda kupima. Hao hawakwenda kupima kwa hiyari yao ni baada ya kupata semina mbali mbali na maelekezo ndio wakaona kwamba kama mtu akipata maambukizo kama hajajua afya yake anaweza akaathirika na akapotea mapema. Mhe. Mwenyekiti, misaada hii imetusaidia sana. Leo fedha hizi zimeshaanza kupungua. Sisi tunajiuliza kuwa je, wakisema kuwa kila siku wanaendelea kupunguza je, wakikatisha kabisa hizi kazi serikali wenyewe itaziweza. Mhe. Mwenyekiti, kwa jawabu ya haraka haraka hatuiwezi.

Kwa hivyo, kuanzia hivi sasa katika bajeti na makusanyo yetu ni lazima tuweke fungu maalum, ukiwacha lile fungu la kila wizara ya kushughulikia kutoa elimu kwa masuala ya maambukizo ya ukimwi, lakini kuwe kuna fungu ambalo ni la kusaidia mpaka zile *NGOs* ambazo zimejitolea kwa ajili ya kwenda kutoa taaluma vijijini. Mheshimiwa hawa wanafanya kazi kubwa sana. Ukiangalia kuna watoto mayatima, basi *NGOs* hizi wanawashughulikia. Kuna watoto waliopata maambukizi ya ukimwi *NGOs* hizi wanawashughulikia. Lakini ukiangalia je, nguvu hii ya kupata kuwashughulikia wanaipata wapi, wanaipata kwa kupitia zile *donor fund* ambazo wanachangia. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tokea walianza kutoa *early warning* wakasema tunategemea huwenda tukapunguza, wameanza

kupunguza na sasa hivi tayari kuna mashirika mengine yameshaanza kukatisha.

Sasa hofu yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa wale ndugu zetu *NGOs* walioamua kwa makusudi kwenda kuwafuata wagonjwa majumbani mwao, wakishakuwa hawana nyenzo za kwenda kule, sijui tutafanya nini. Kwa sababu nikitoa mfano mdogo, leo kuna baadhi ya familia kwa kuwahawajapata hii taaluma, basi kama anatokezea mtu mgonjwa wa ukimwi ndani ya nyumba yake, hata kama ni mtoto wake basi wanamnyanyapaa na wanamnyanyapaa kwa sababu hawajapata taaluma. Lakini hawa ndugu zetu wanakwenda na wanawasiliana na ile familia wanayomshughulikia yule mgonjwa kisha wanawapa taaluma, na matokeo yake sasa hivi wale wananchi ambao familia zao miongoni mwao ametokezea mmoja amepata maambukizo na kama ameshaanza kupata maradhi basi wanamshughulikia wao wenyewe. Lakini kama hawakupata wale wenye taaluma kwenda kuwaelekeza namna ya kushughulikia hao wagonjwa basi kuna hatari hata na wao kupata hayo maambukizo.

Ndio maana tukasema hii asilimia 0.6 ya maambukizi kwa Zanzibar, kama taaluma itasitishwa kutokana na ukosefu wa fedha, basi Mhe. Mwenyekiti, itaanza kuongezeka na kuja asilimia 1, asilimia 2 na mwisho tutakuja kuwa kama South Africa au Botswana. Botswana ilifika pahala wakafikia kama sikosei mpaka karibu asilimia 30 ya maambukizi. Sasa kwa Zanzibar asilimia 30 ni kubwa, kwa sababu wale wenzetu wanatoka wanakwenda mbali. Sasa hapa Zanzibar unatoka unakwenda wapi, Darajani, Jang'ombe, Kiwengwa na sijui Michamvi umerudi, kwa hivyo mtu anapita anaeneza tu.

Kwa hivyo, mimi nadhani ni lazima tuchukuwe hatua za haraka. Moja katika maeneo ambayo maambukizo yanaenea kwa haraka ni kwa hawa wanaotumia madawa ya kulevya, ndio maana tukasema kwamba suala la maambukizi ya ukimwi na madawa ya kulevya ni mtu na shemegi yake, kwa sababu ukianza kutumia madawa ya kulevya basi ndio inapelekea sasa kwenda kwenye matayarisho ya maambukizi ya ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kitu nilichokuwa nataka kusema ni kwamba lazima tuharakishe hizi sheria zetu na sio tuharakishe tu, kwanza kuzisimamia hizi sheria zetu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ambaye ndio kiongozi wetu wa serikali, kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, iandaliwe semina ya mahakimu, polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa tunajitahidi kutunga sheria, polisi wanajitahidi kukamata, DPP wanajitahidi kupeleka mahakamani, lakini hukumu katika kesi, sijui kesi 98 unakuta kesi zilizopata hukumu hazizidi 10. Kwa hivyo

hapa kuna tatizo na tatizo lenyewe, sisi tunakuwa wakali kwa sababu sisi Mhe. Mwenyekiti, ajira yetu ni kusema na kama ajira yetu ni kusema basi sisi tunalipwa kwa sababu ya kusema. Sasa kama maneno yote tunayoyasema halafu baadae hakuna utekelezaji, faida yetu nini, ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika marekebisho yao kuna sheria ya *money laundry*, hata na sisi kama tunatunga sheria hazitekelezwi basi *money laundry* ndio hivyo hivyo. Maana yake tunatunga sheria lakini hatuzitekelezi, kwa sababu unapata fedha ambazo haziko katika utaratibu. Sasa ndio maana nikapendekeza iweko semina ya hivi vyombo ambavyo vinashughulikia mambo haya. Narudia tena Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Kamishna wa Polisi na kitengo chake cha madawa ya kulevya, Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na watendaji wake pamoja na mahakimu.

Mhe. Mwenyekiti, kama itatayarishwa semina hii basi naamini ndani ya miezi mitatu tutaanza kuona matunda yake. Kwa sababu pale itakuwa kazi yetu ni kulaumiana tu, mahakimu ilifika pahala tulipokuwa tunalaumu wakasema jamani hizi sheria zenu mlizoziweka mbovu. Ndio maana wakasema leo unaposema gramu moja lazima kesi isikilizwe na mahakama kuu na kesi ikija mahakama kuu kunatakiwa ma-*assessor* wanne na hao ma –*assessor* wanne wanalipwa, bajeti ya mahakama ndogo na kesi za madawa ya kulevya ni nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna safari moja tulifanya uchunguzi katika zile siku 4 za skukuu, basi walikamatwa watu 47, katika 47 hao wengi wao wamekamatwa na hivyo vitu, lakini matokeo yake kesi haina ushahidi, kesi haijakamilika, polisi pale kwa mujibu wa sheria hawezi kumuweka mtu zaidi ya masaa 24, inabidi polisi wawaachie kwa sababu ushahidi haujakamilika. Kwa hivyo, utakuta kuna urasimu mwingi. Mimi nadhani huu urasimu mwingi wakati mwengine unatokana na uadilifu, sasa tukiwa pamoja tukiambizana kweli mimi naamini pale tutatoka na maazimio. Kama mahakimu wanasema sheria bado zina mapungufu basi tutawauliza pale pale tutawaambia ni kifungu gani, basi watatuambia ni kifungu fulani tutaandika na mwengine atatuambia kifungu fulani tutaandika na polisi vile vile na yeye atasema. Kwa sababu polisi mara nyengine wanalalamika kwamba wao wanakamata, lakini mahakamani wanakwenda watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, zamani kulikuwa kuna sheria polisi anakamata na anakwenda kusimamia kesi mahakamani. Lakini baada ya utawala bora maana yake huwezi ukakamata halafu wewe ukasimamia kesi utakuwa na upendeleo. Tumerekebisha ile tumeweka *DPP*, sasa yeye polisi analalamika kwa sababu kakamata halafu kule anaachiwa, kwa hivyo kila mmoja

anamlaumu mwenzake. Kwa hvyo, polisi wanaongozwa na sheria yao ya Jeshi la Polisi, mahakimu sheria ndio tunazitunga sisi, *DPP* sheria tunazitunga sisi. Sasa tukikaa pamoja sote hao niliowataja, basi mimi naamini Mhe. Mwenyekiti, tutakuja na sheria hapa ambayo kila mmoja kama hakuitekeleza basi tutajua nani ni mkosa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo katika suala zima la madawa ya kulevya, nataka nije kugusia eneo la *money laundry*. Mhe Mwenyekiti, kwa bahati sisi tulikwishapitisha hapa sheria ya *money laundry*, kuna mapungufu ambayo yamejitokeza, imeletwa tena marekebisho. Lakini bado katika eneo hili mimi narudia tena. Mhe. Mwenyekiti, sheria tuliyoipitisha ya *money laundry* ilikuwa sio mbaya, ni sheria nzuri kabisa. Mimi nitatoa mfano mmoja katika sheria ya *money laundry* mtu anaposafirisha, mfano ya madawa ya kulevya, akagundulikana biashara yake anayoifanya ni ya madawa ya kulevya, yaani ile faida anayoipata kutokana na madawa ya kulevya, basi katika ile sheria inasema kuwa mtu anatakiwa awe muflisi, yaani ile mali yake anayoikusanya kwa ajili ya biashara ile inakuwa muflisi. Lakini bado tatizo liko kwenye utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, kuna chombo vile vile kiliundwa kwa ajili ya kuchunguza sijui ACPU kitu kama hivi. Lakini ukiangalia je, kweli hapa kwetu tokea kutungwa sheria ile kweli hakuna watu hapa wanaosafirisha fedha zao baadae wakaja kufanya miradi mingine. Kwa sababu usimuone mtu yuko tajiri tu, hujui utajiri wake kaupata vipi. Ndio kama hivyo watu wanasafirisha madawa ya kulevya, watu wanafanya mambo mbali mbali ya dhulma, utawaona tu. Mtu tajiri mara leo kasaidia hiki na kile, lakini ukiangalia biashara yake haitambulikani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sijui hizi sheria zetu zina udhaifu kiasi gani. Kwa hivyo, bado mimi narudia tena katika eneo hilo hilo la *money laundry* kwenye semina hiyo, basi tunaweza tukalizungumza kwa pamoja, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wanafanya biashara, lakini ukiangalia biashara wanazozifanya ukiangalia na uwezo wao au mali wanazozimiliki hazilingani na wakati kuna sheria vile vile kwamba mali zile ambazo unazimiliki, kwanza unatakiwa uzilipie kodi. Lakini je, zile mali unazozimiliki kweli zinalipiwa kodi kihalali.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tuliwahi kupitisha sheria ya kodi ya majengo, sheria ile mpaka leo hatujaja kuifanyia marekebisho. Kuna siku niliwahi kuzungumza na swahibu wangu Mufti, Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, nikamwambia Mheshimiwa bado kuna pesa hapa Zanzibar hatujazikusanya, zipo kila ukizichungulia fedha unaziona. Mufti akaniuliza fedha zipi hizo, nikamwambia kuna nyengine nitakuja kukuambia

lakini kuna pesa za kodi za majengo hatujazikusanya. Nitaomba Mhe. Mwenyekiti, japo kidogo uje umpe nafasi, najua hakujiandaa kuchangia leo, lakini japo kidogo tu, je kodi za majengo anazikusanya, lakini tumeshazipitisha kwenye sheria.

Kuna watu Mhe. Mwenyekiti, wana majumba kuliko Baraza la Wawakilishi, unatakiwa ulipie kodi, kwa sababu unajua wakati mwengine watu hawa kama hatuwafuatilii, basi tutakuwa tunawanyanyasa wananchi na tunawakosesha haki zao wananchi. Baraza la Wawakilishi likishatunga sheria hasa ya kodi, kama kodi ile haikusanywi basi mwananchi tunamdhulumu. Ndio maana tunasema kwamba wakati mwengine tunalalamika kuwa serikali haina fedha, lakini kuna sheria ambazo tumeshapitisha lakini tunashindwa kukusanya.

Labda Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aje aniambie anaogopa nini na tulisema sio kodi mpaka kibanda cha mgongo, tuliweka mpaka thamani hapa. Sasa kama ile sheria ngumu haitekelezeki aja atuambie au aje tuifute. Mimi nitakuja kuwahoji ikifika bajeti ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, nataka fedha zilizokusanywa za kodi za majengo. Nitakuja kuwa mkali kweli kweli hapa, kwa sababu kuna fedha hazikukusanywa na kwa sababu kuna fedha zinahitajika ndani ya serikali ili zisaidie maendeleo ya nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, tukiwa tunatunga sheria halafu hatuzitekelezi, ndio pale niliposema hata sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutakuwa *money laundry*, tunasema tutafanya, lakini utekelezaji haupo.

Nitatoa mfano mdogo. Mhe. Mwenyekiti, mimi naishukuru sana serikali kwa kupitia Mufti Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, alitoa mapendekezo na kwa bahati nzuri alipotoa yale mapendekezo hakuchukua muda akayafanyia kazi. Alisema nitahakikisha wenyeviti wote wa Baraza pamoja na wewe Mwenyekiti, tutawapeleka China kwenda kujifunza. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mufti Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, katika hilo jopo la mwanzo lililokwenda China na mimi nilikuwemo. Mhe. Mwenyekiti, kule tumejifunza mambo mengi sana na bahati nzuri na Mwanasheria Mkuu pamoja na Katibu wetu wa Baraza la Wawakilishi walikuwemo.

Kwa kweli wenzetu China wanasema yale maendeleo yao, basi wao wenyewe wanashangaa wanasema ni miujiza. Kwa nini ikawa ni miujiza? Kwa kuwa wanachokiamua ndicho kinachotekelezwa, yaani kile kinachoamuliwa ndicho kinachotekelezwa. Kwa hivyo, na sisi wakatuambia Zanzibar mbona mnazo sheria nzuri nyinyi na kama mtazisimamia vizuri, basi mtafanikiwa.

Kutokana na hali hiyo alitutolea na mfano, alisema kama mtashughulikia maeneo mawili karafuu na uvuvi, Mhe. Mwenyekiti Zanzibar itaweza kusimamia uchumi wake tena vizuri, kwa mazao mawili tu haya yataendeleza uchumi wa Zanzibar.

Lakini alitueleza tatizo lenu ni katika usimamizi wa sheria zenu vile vile alitutolea mfano. Kwa mfano, Sheria za Mazingira mnashindwa kuzisimamia vizuri na tukiangalia kweli, kwa sababu tunapitisha sheria nyingi za mazingira zinabakia kwenye vitabu na utekelezaji hakuna. Vile vile watu wanavunja ovyo pamoja na jeuri juu na sisi tupo *watchdog* tunaangalia vipi, kumbe vile ni *sleeping dog* sio *watchdog*. Mhe. Mwenyekiti, kama ni *watchdog* sheria uliyoitunga unatakiwa uisimamie.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, wenzetu maendeleo yao ni kwa sababu wanasimamia sheria. Kwa mfano, Sheria ya Rushwa China ipo, lakini ukiwauliza hukumu yake nini hawakwambii, kwa sababu wanajua ile sheria inavyofanyakazi na wala kule mtu halirushwa, kwani watu wanasimamia sheria zao. Je, hapa Mhe. Mwenyekiti?

Kwa hivyo, mimi narejea tena Zanzibar hatuna matatizo ya sheria, isipokuwa Zanzibar tunayo matatizo ya utekelezaji pamoja na usimamizi wa sheria zetu.

Kwa maana hiyo, tumejifunza mambo mengi kule na ndio maana tunapokuja huku tunaona tumekwenda kujifunza nini na tunakuja kufanya nini. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri baada ya kurudi safari ile Mhe. Mwanasheria wetu Mkuu akaona kuna baadhi ya mambo aanze kuyafanyia marekebisho, nadhani ndio akaanza na haya marekebisho ya sheria.

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, ambaye yeye ndiye aliyekabidhiwa mahakimu wote, basi hivi sasa tusaidiane hii kazi, ili wale wafanyakazi zao kwa uadilifu kwa hizi sheria tunazozitunga hapa ziende vizuri na ziweze kusimamiwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache nataka niseme nampongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini yale mapendekezo yangu ya *One Stop Centre*, Mahakama Maalum au Mahakama Mahsusi itakuwa inashughulikia Madawa ya Kulevya. Nadhani nitaweza kuunga mkono kwa asilimia mia moja sheria hii.

Kwa kweli sikwenda kuangalia ile sheria iliyofungwa na iliyoengezwa kwa sababu sikupata muda huo, Mhe. Mwenyekiti kama unavyojua leo ninajukumu kubwa, hivyo sikupata utulivu. Kwa hivyo, baada ya hayo

machache Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ndogo chache nimalizie ya kuweza kuchangia kidogo mambo mawili matatu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kufanya masahihisho mengi katika mswada, ambao uliowasilishwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu juu ya marekebisho mbali mbali ya sheria. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kamati imefanyakazi kubwa na hasa wao ndio waliotunga hiyo sheria yenyewe. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nimeona kwamba hata jina la sheria hii limekuwa likibadilika mbali ya sheria zinabadilishwa. Kwa mfano, kulikuwa na Sheria Nam. 6 mwaka 2003, pia kuna Sheria ya Nam. 9 ya mwaka 2009, na hivi sasa, lakini hata lile jina la sheria yenyewe linaonekana kuwa bado hatujafikia pahala.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Sheria ile iliyopita ya Madawa ya Kulevya ya mwaka 2009, basi inasema kwamba Sheria hii itajulikana kama ni Sheria ya Madawa ya Kulevya, Kuzuia, Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya mwaka 2009. Lakini tukiangalia marekebisho haya ya sheria nayo yamekuja na jina jengine kwa suala hilo hilo inayosema Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Madawa ya Kulevya.

Vile vile kwa upande wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala nayo ikabadilisha jina ikarekebisha ikasema Sheria ya Kudhibiti Utumiaji Haramu wa Usafirishaji wa Dawa za, yaani wameishia za sijui za nini na wao wametuacha solemba hawakutumalizia. Kwa hivyo, inaonekana hata jina la sheria hii imekuwa ni vigumu na ndio maana utekelezaji wake umekuwa ni mgumu na kila wakati yanakuja marekebisho.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti na mimi nipendekeze jina la sheria hii iitwe Sheria ya Udhibiti wa Uingizwaji, Usafirishwaji na Utumiaji wa Madawa Haramu ya Kulevya, kwa sababu hata hili jina ambalo Mhe. Mwanasheria Mkuu ambalo amelikubali lililopitishwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala lina kitu muhimu sana ambacho kimeachwa. *(Makofi)*

Kwa mfano, unaposema Sheria ya Kudhibiti Utumiaji Haramu na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya, lakini kuna uingizwaji kitu hiki tumekiacha, kwa sababu dawa zile zinaingizwa na baadaye zinasafirishwa. Vile vile kuna

watumiaji, kwa kweli kuna maeneo matatu ambayo madawa haya, kama vile zinaingizwa, watumiaji pamoja na wale wanaoziondosha hapa kwa ajili ya kuzisafirisha.

Kwa hivyo, nadhani maeneo hayo pia yawepo kwamba Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji, yaani kudhibiti uingizwaji, Usafirishaji, yaani kutoka hapa kwenda nje, pia na Utumiaji wa Madawa yale yanayoweza kutumika hapa. Mhe. Mwenyekiti, napendekeza kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu akubali kuwa tutumie neno hilo au jina hilo la sheria.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia kifungu cha 4(g) cha marekebisho ya mswada naomba kunukuu.

Kifungu cha 4(g) kinaeleza hivi:-

> "Kufuta maneno ya kufungia mwisho wa kifungu cha tafsiri".

Mhe. Mwenyekiti, nipoangalia mswada kulikuwa hakuna haja ya kuwa na maelezo hayo, isipokuwa tu liwepo neno linalosema kufuta neno la mwisho la kifungu cha tafsiri kifungu cha 2(2), kwa sababu hiki kifungu kina jina lake ni kifungu cha 2(2)(ii) kuliko kusema kufuta maneno ya kufungia mwisho wa kifungu cha tafsiri. Kwa hivyo, ni vyema kuweka namba ambayo itasaidia na kwa sababu sheria zinakuwa zinakwenda kwa namba.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwenye kifungu cha 4(f) naomba kunukuu.

Kifungu cha 4(f) kinaeleza hivi:-

> "Kufuta tafsiri ya maneno Ofisa wa Polisi"

Kwa kweli mimi najiuliza kwa nini tafsiri ya maneno hayo yaondoshwe katika sheria na wakati kwenye sheria tayari kuna maelezo ambayo yametaja Maofisa wa Polisi katika sheria. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje kutueleza ni kwa nini Ofisa wa Polisi aondoshwe katika marekebisho ya mswada huu, yaani tafsiri ya maneno Ofisa wa Polisi.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 4(1) cha Sheria Mama ambacho kinazungumzia kuanzishwa kwa tume naomba kunukuu.

Kifungu cha 4(1) cha Sheria Mama kinaeleza hivi:-

> "Kutakuwa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti wa Dawa za Kulevya, ambayo itakuwa na jukumu la kufafanua, kuendeleza na kuratibu Sera za Serikali kwa ajili ya kudhibiti matumizi ya mabaya ya dawa haramu".

Lakini paingizwe na neno la uingizwaji na usafirishwaji wa dawa za kulevya liongezwe, pamoja na kudhibiti matumizi ya usafirishaji, lakini kifungu hiki ambacho tume itakuwa miongoni mwa kazi zake iwemo na kudhibiti uingizwaji wa haya madawa ya kulevya.

Lakini kifungu cha 4(2)(k) naomba kunukuu.

Kifungu cha 4(2)(k) kinaeleza hivi:-

> "Kamishna wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar".

Kwa hivyo, badala ya Kamishna na hapa tunaye Naibu Kamishna. Kutokana na hali hiyo tufanye marekebisho kwamba badala ya kuwa na Kamishna wa Idara ya Uhamiaji tuwe na Naibu Kamishna wa Idara ya Uhamiaji kama alivyo Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa na Naibu Kamishna wa Forodha.

Mhe. Mwenyekiti, pia kifungu cha 4(a)(1)(c) neno Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama ilivyopendekeza na kamati baada ya neno mtu. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imebadilisha neno na kusema Mwanasheria Mkuu wa Serikali badala ya neno mtu.

Vile vile na mimi napendekeza badala ya kutumia neno mtu, basi napendekeza iwe afisa kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hata Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imependekeza kwamba maeneo mawili haya yote awepo Mwanasheria wa Serikali, hivyo hii ya mwanzo nakubaliana nayo kuwa badala ya mtu awepo Mwanasheria wa Serikali.

Lakini hapa kwenye Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka basi kusiwe na Mwanasheria wa Serikali, isipokuwa awepo Afisa kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hata kama atakuwa ni mwanasheria pamoja na vyeo vyake vyengine haina tatizo.

Nikiendelea kwenye kifungu cha 4(1)(f) badala ya kuwa na mtu mmoja, basi iwe Afisa mmoja kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Halikadhalika

kwenye kifungu cha 4(1)(e) kuwe na Afisa kutoka Idara ya Forodha, badala ya kuandika mtu kutoka Idara hii ya Forodha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tunapoandika au tunapoipa nguvu sheria kuandika afisa maana yake ile tume inakuwa na nguvu, kuliko kuandika mtu, kwa sababu anaweza kupelekwa mfanyakazi yeyote, lakini unapoandika afisa maana yake atatafutwa yule afisa wa ngazi ya juu, ambaye atakuwa anashiriki katika tume ile.

Kwa hivyo, yale maeneo ambayo yameandikwa neno mtu katika taasisi za serikali, basi ni vyema tukaandika afisa, ili wale wahusika watafute afisa anayehusika kwa ajili ya kumpeleka eneo hilo kuliko ilivyo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu cha 10 cha Sheria mama naomba kunukuu.

> Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinaeleza hivi:-
>
> "Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinarekebishwa na kufutwa kijifungu cha (2)".

Namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze hicho kifungu cha 10(2) cha Sheria Mama kinaeleza vipi na sababu za kufutwa kifungu hicho.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye mswada unaohusiana na Fedha Haramu. Nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, kwamba Sheria hii ya Mswada wa Fedha Haramu tuliwahi kuupitisha katika kikao kilichopita na moja kati ya eneo ambalo lilizusha utata ilikuwa ni kifungu cha 10 cha sheria ile.

Katika kifungu hicho sheria ilitoa mamlaka kwa Kamati inayoitwa *Financial Intelligent Unity (FIU)*, ambayo kamati hii imeundwa kwa mujibu wa Sheria za Bunge na tulitaka tuipe mamlaka kwamba kamati ile ifanye kazi hapa Zanzibar.

Lakini katika marekebisho haya pia inaonekana kuna sura ya aina hiyo ya kuipa mamlaka kamati hiyo pamoja na kwamba sheria haikueleza muundo wake ukoje na wajumbe wake wako vipi, kwa sababu kamati hiyo haikuundwa hapa. Sasa bado inaonekana eneo hili lina kasoro.

Mhe. Mwenyekiti, kasoro nyengine ambayo ni kubwa ni pale ambapo tunaposema kwamba kitengo hiki kilichoundwa na Sheria za Bunge au chombo hiki si chombo cha muungano. Kwa hivyo, suala hili linahitaji kuangaliwa kwa umakini, kwa sababu sisi Zanzibar hapa kwa mujibu wa mswada ule tumesema tutakuwa na Afisi Ndogo ya *FIU*, sasa sijui afisi hii

ndogo itakuwa na uhusiano gani kati ya afisi hii na hiyo ya Jamhuri ya Muungano ambayo imepitishwa na Sheria ya Bunge.

Kutokana na hali hiyo, bado kuna haja ya maelezo ya ziada kutoka kwa Mhe. Mwanasheria kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho ni kwa nini *unity* hii ambayo imepitishwa na Bunge ipewe mamlaka ya moja kwa moja kufanyakazi hapa. Hivi muundo wake uko vipi? Zanzibar ina wajumbe wangapi katika kamati hiyo? Je, ina sura ya muungano?

Kwa hivyo, hayo ndio mambo ambayo namuomba Mhe. Mwanasheria kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi tunahitaji kupata maelezo ya kina, ili tuweze kuukubali mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Salmin Awadh Salmin kutokana na mchango wako na *Inshaallah* Mhe. Mwanasheria Mkuu amechukua.

Waheshimiwa Wajumbe, nina ombi moja nataka kuomba kwenu. Pamoja na utaratibu kwamba kwenye Kanuni hakuna eneo ambalo linazuia Mhe. Mjumbe kuchangia baada ya waziri, lakini kuna taratibu pia. Kwa hivyo, ninaomba Waheshimiwa Wajumbe tuwe na utaratibu wa kuchangia mwanzo na wakati anaponyanyuka Mhe. Waziri basi iwe anaendelea pamoja na majumuisho na kumaliza hoja ile ambayo itakuwa tumeikusudia katika mswada. *(Makofi)*

Pili Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile shughuli zetu za uchangiaji zimefikia hapa na Mhe. Mwanasheria Mkuu ameomba apewe nafasi ya kwenda kutafakari zaidi na kuweza kuja kutoa majumuisho ya jumla hapa kesho tutakapojaaliwa.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 25/10/2011 saa 3:00 asubuhi)

\’